# Kiswahili

## Kidato cha 4

# Michepuo Mingine
# Mwongozo wa Mwalimu

***© 2024 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi***

*Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi. Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi wakati yaliyomo yamenukuliwa.*

*Chapa ya Pili 2024*

**DIBAJI**

Mwalimu mpendwa,

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kwa kutoa mwongozo wa mwalimu kwa kidato cha nne katika michepuo mingine.

Mwongozo huu ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unamwezesha mwanafunzi kuendeleza mawazo yake na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi. Wanafunzi, kwa msaada wa mwalimu, watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yao binafsi bali pia hata kwa taifa.

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu. Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, ili kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako kama mkufunzi litakuwa :

- Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa

- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikiano ya wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu; Kushirikisha wanafunzi kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinafsi;

- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano;

- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani;

- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti;

- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi,

- Kuutumia mwongozo kutakusaidia katika kazi yako ya kufundisha kwani yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Ingawa mwongozo huu wa mwalimu una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini

Napenda, kwa moyo wote, kutoa shukrani zangu kwa watu wote walioshiriki kutoa mchango wao wa kuboresha mwongozo huu wa mwalimu, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (REB/CTLRD) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanzishwa

Pongezi maalum ziwaendee walimu wa ngazi tofauti kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili.

Maoni au mchango wowote wa mawazo unakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo mengine yatakayofuata baadaye.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB.**

# SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa mwalimu. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu za kwanza ni kwa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Pia napenda kutoa shukrani kwa walimu wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Aidha, natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu kushiriki katika kukiandaa na hata kukikamilisha kitabu hiki.



**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana ( CTLRD)**

# YALIYOMO


DIBALI....................................................................III

SHUKRANI....................................................................V

MADA KUU YA 1: MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI.................................................... 1

1.1. Uwezo Upatikanao katika Mada: ..............................................1

1.2. Ujuzi wa Awali 1

1.3. Masuala Mtambuka ..............................................................1

1.4. Mwongozo kuhusu Kidokezo cha Mada......................................1

1.5. Orodha ya Masomo na Tathmini ..............................................1

SOMO LA 1: Mazungumzo Hospitalini ....................................2

1.1. Ujuzi wa Awali/Utangulizi.................................................... 2

1.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji............................................... 3

1.3.Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji ...................................... 3

1.4 MAJIBU............................................................................ 4

SOMO LA 2: USAFI WA MAZINGIRA YA HOSPITALI.................. 9

2.1. Ujuzi wa Awali ...................................................................9

2.2. Zana au vifaa vya Kujifunzia...................................................9

2.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji........................................9

2.4 MAJIBU ............................................................................10

SOMO LA 3: ADABU HOSPITALINI....................................... 14

3.1. Utangulizi/Marudio.............................................................14

3.2. Vifa vya Kujifunzia .............................................................14

3.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji.......................................14

3.4 Majibu .............................................................................15

3.5Muhtasari wa Mada ..............................................................19

3.6. Maelezo ya Ziada ...............................................................19

3.7. Tathmini ya Mada ya Kwanza .................................................19

3.8 Soma maswali yafuatayo na kujibu:.......................................... 20

3.9. Mazoezi ya Ziada ...............................................................21

SOMO LA 4: MICHEZO SHULENI ........................................... 23

4.1. Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi ........................................23

4.2. Zana za Kujifunzia ....................................................................23
4.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji........................................23
4.4 Majibu .......................................................................................25
SOMO LA 5: FAIDA ZA MICHEZO ............................................28
5.1. Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi........................................... 28
5.2. Zana za Kujifunzia..................................................................... 28
5.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji........................................ 28
5.4Majibu ........................................................................................ 29
SOMO LA 6: MASHINDANO .................................................... 35
6.1. Ujuzi wa Awali ............................................................................35
6.2. Zana za Kujifunzia ....................................................................35
6.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji........................................ 36
6.4 MAJIBU ......................................................................................37
6.5. Muhtasari wa Mada .................................................................. 42
6.6. Maelezo ya Ziada....................................................................... 42
6.7.Tathmini ya Mada ya Pili ........................................................... 42
6.8. Mazoezi ya Ziada........................................................................43

MAADA KUU YA 3: UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI KATIKA KISWAHILI.......................................... 45
MADA NDOGO: MUHTASARI, FANI NA MAUDHUI ................. 45
SOMO LA 7: MUHTASARI........................................................49
7.1. Ujuzi wa Awali .......................................................................... 49
7.2. Zana za Kujifunzia..................................................................... 49
7.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji........................................ 50
7.4 MAJIBU ...................................................................................... 50
SOMO LA 8: FANI KATIKA HADITHI SIMULIZI .......................56
8.1. Ujuzi wa Awali .......................................................................... 56
8.2. Vifaa vya Kujifunzia .................................................................. 56
8.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji........................................ 56
8.4 MAJIBU ...................................................................................... 58

SOMO LA 9:MAUDHUI KATIKA HADITHI SIMULIZI ............... 63

9.1. Ujuzi wa Awali ...........................................................................63

9.2. Vifaa vya Kujifunzia .......................................................................63

9.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji.......................................63

9.4 MAJIBU ............................................................................................ 65

9.5. Muhtasari wa Mada ....................................................................... 70

9.6.. Maelezo ya Ziada.............................................................................. 70

9.7. Tathmini ya Mada ya Tatu ............................................................. 70

MADA KUU YA 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO .......................................................... 72

MADA NDOGO: MIDAHALO NA MIJADALA ............................ 72

SOMO LA 10: MDAHALO......................................................... 76

10.1. Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi ........................................ 76

10.2. Zana za Kujifunzia ......................................................................... 76

10.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji ..................................... 76

10.4. Kusoma na Uufahamu .................................................................77

SOMO LA 11: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MDAHALO .86

11.1. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji ...................................... 86

11.2. Kusoma na Ufahamu ..................................................................... 86

11.3 Kuandika...... 95

SOMO LA 12: MJADALA.........................................................96

12.1. Ujuzi wa Awali/Utangulizi ......................................................... 96

12.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji .................................................. 96

12.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji........................................ 96

12.4. Kusoma na Ufahamu ...................................................................... 97

SOMO LA 13: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MJADALA.. 104

13.1. Ujuzi wa awali/ Utangulizi.......................................................104

13.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji ................................................104

13.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji....................................104

13.4. Majibu .......105

13.5. Muhtasari wa Mada ....................................................................... 111

13.6. Maelezo ya Ziada.......................................................... 111
13.7. Tathmini ya Mada ya Nne.......................................................... 111
MADA KUU YA TANO: UTUNGAJI.......................................... 115
MADA NDOGO: INSHA ZA MASIMULIZI AU ZA KUBUNI Uwezo Upatikanao katika Mada ..................................................... 115
SOMO LA 14: MAANA YA INSHA ............................................ 118
14.1. Utangulizi/Marudio ..........................................................118
14.2. Vifaa vya kujifunzia ..........................................................118
14.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji ..................................118
14.4 MAJIBU....... 119
SOMO LA 15: AINA ZA INSHA ..............................................128
15.1. Ujuzi wa Awali/Utangulizi .......................................................... 128
15.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji .......................................................... 128
15.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji.......................................... 128
15.4. Majibu .......129
SOMO LA 16: UTUNGAJI WA INSHA ZA MASIMULIZI 138
16.1. Utangulizi/Marudio .......................................................... 138
16.2. Vifaa vya Kujifunzia.......................................................... 138
16.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji .................................. 138
16.4. Majibu .......139
16.5.Muhtasari wa Mada.......................................................... 146
16.6. Maelezo ya Ziada .......................................................... 146
16.7. Tathmini ya Mada ya Tano.......................................................... 146
16.8. Mazoezi ya Ziada .......................................................... 146

SEHEMU III: MADA

# MADA KUU YA 1: MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

1

## MADA NDOGO YA 3: MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA HOSPITALI

### 1.1. Uwezo Upatikanao katika Mada:

Kusikiliza kwa makini, kusoma vifungu vya habari na kutumia msamiati muhimu katika mazingira ya hospitali; kuzingatia matumizi ya viambishi -nge-, -ngeli- na -ngali-.

### 1.2. Ujuzi wa Awali

Hii ni mada ya kwanza katika kidato cha nne, michepuo isiyokuwa ya lugha. Mada hii inazungumzia "Msamiati katika mazingira ya hospitali". Tayari wanafunzi wa kidato hiki wana ujuzi wa awali wa kutosha kuhusu msamiati utumiwao katika sehemu mbalimbali. Sehemu hizo ni kama sokoni, nyumbani na shuleni, kilimo na ufugaji, hotelini na kadhalika. Kupitia mada hii, wanafunzi wanapanua ujuzi wa msamiati wao. Msamiati wa mazingira ya hospitali ni mojawapo wa msamiati wa matumizi ya kila siku. Kwa hiyo, si kitu kipya kwa wanafunzi hawakuelimishwa msamiati unaotumiwa mahali maalumu.

### 1.3. Masuala Mtambuka

Kupitia mada hii, mwalimu aonyeshe nafasi ya mwanamke na hadhi yake katika jamii. Hapa mwalimu atakuwa na jukumu la kuhimiza wanafunzi kuheshimu usawa wa jinsia kimaendeleo. Kitu kingine, mwalimu ataonyesha wanafunzi namna wanavyoweza kuzalisha mali katika kazi yoyote wanayoifanya. Hivi vyote vitafanyika katika hali ya amani na maadili mema.Kutokana na hali ya hapo juu, itachochewa elimu kwa wote/ elimu isiyo na ubaguzi ili kufanikisha maendeleo shirikishi endelevu.

### 1.4. Mwongozo kuhusu Kidokezo cha Mada

- Mwalimu anatoa mwongozo wa kutoa jibu kwa kazi. Itakuongoza kufahamu mambo muhimu unayostahili kutilia maanani wakati wa kufunza somo fulani. Ni sharti urejelee kitabu cha mwanafunzi kila unapofunza lolote lililoandikwa kitabuni humo. Baada ya kufunza jambo hilo ni sharti uwaongoze wanafunzi kuyarudia uliyoyafunza kwa kuyarejelea vitabuni mwao.

- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia kazi nyingine zilizotayarishwa. Kumbuka kuwa yamo baadhi ya mambo katika mwongozo huu ambayo hayamo katika vitabu vya wanafunzi. Mambo haya ni nyongeza yako ya kukutayarishia kazi yako.

### 1.5. Orodha ya Masomo na Tathmini

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (kutoka muhtasari: maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| 1. Msamiati katika mazingira ya hospitali | Maarifa na ufahamu: kutamka na kuandika majina vifaa na wafanyakazi wa hospitalini.<br><br>Stadi: kutumia msamiati sahihi kuhusu mazingira ya hospitali katika mawasiliano rahisi.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kuheshimu mazingira, vifaa na wafanyakazi wa hospitalini. | 7 |
| 2.Usafi hospitalini | Maarifa na ufahamu: kueleza umuhimu wa usafi hospitalini.<br><br>Stadi: Kufanya usafi kwa kuboresha afya<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kuimarisha usafi katika mazingira mbalimali. | 8 |
| 3. Adabu hospitalini | Maarifa na ufahamu: kuonyesha mwenendo mzuri hospitalini.<br><br>Stadi: kufuata sheria za hospitalini. | 7 |
| | Maadili na mwenendo mwema: kukuza adabu hospitalini. | |
| Tathmini ya mada2 | | |
| Vipindi vya mada zote24 | | |

## SOMO LA 1: Mazungumzo Hospitalini

### 1.1. Ujuzi wa Awali/Utangulizi

Somo hili linajishughulisha na "Msamiati katika mazingira ya hospitali"ambapo huzungumziavifaa pamoja na wafanyakazi wa hospitalini. Mwalimu ataanza somo na kueleza maana ya hospitali na watu tunaowakuta hospitalini kama kiini cha somo lenyewe. Wanafunzi wataeleza wanayoyajua kuhusu hospitali na wafanyakazi wanaowajua ili kumwezesha mwalimu kupata mwanzo wa somo kutokana na wanayoyajua.Mojawapo ya maswali mwalimu anayoweza kumuuliza mwanafunzi ni kama yafuatayo:

- Hospitali ni nini
- Taja vifaa vitano vitumiwavyo hospitalini, kisha eleza umuhimu wake.
- Ainisha kazi na majukumu ya wafanyakazi wapatikanao hospitalini.
- . Andika aya moja kwa kuelezea umuhimu wa usafi hospitalini.
- Baadhi ya wagonjwa huonyesha mienendo isiyofaa hospitalini. Jadili

## 1.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya watu wanaowasiliana.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa vitakavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Hapa mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji.

## 1.3.Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake hivi akitilia mkazo mbinu zifuatazo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne. Ni vizuri kutozidi idadi ya watu watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inafanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana. Baada ya kazi, mwalimu aombe makundi kuwasilisha matokeo kwa darasa. Kazi katika makundi itiliwe mkazo kwa kusaidia wanafunzi kushirikiana na kujifunza kutoka kwa wenzao.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake. (Asome kifungu cha habari

mwenyewe au afanye zoezi mwenyewe).

- **Maswali na majibu**: Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzake iwezekanavyo. Mwalimu ajaribu kuweka maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati yake na wanafunzi ama wanafunzi na wanafunzi. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wote wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali na wao wamjibu, na vile vile wanafunzi wamwulize mwalimu na wanafunzi wengine wajibu, mwisho wake mwalimu naye atoe majibu yake.
- **Maelezo ya mwalimu:** Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake, kisha atambuwe ujuzi unaohitaji maelezo yake binafsi. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee vya kutosha wanafunzi wake somo kwa kusisitizia kasoro aliyoitambua. Ni vizuri kufanya hivi kwa kuwapa pia wanafunzi fursa ya majadiliano kuhusu maelezo yake.

## 1.4 MAJIBU

**ZOEZI LA 1:** (ukurasa wa 15)

Wanafunzi watazame michoro kwenye ukurasa husika kisha watoe maoni yao kuhusu watu, majengo, vifaa ambavyo hupatikana katika mazingira ya hospitali au zahanati.

### 1.4.2. Majibu ya Maswali ya Ufahamu

**ZOEZI LA 2:** (ukurasa wa 18)

1. Wanaozungumza katika kifungu ni Daktari, Muuguzi na wanafunzi wanaozuru hospitali.

2. Kwa kuitembelea hospitali inayozungumziwa wanafunzi walikuwa na lengo la kujielimisha kuhusu vifaa na wafanyakazi wa hospitali.

3. Wanafunzi hao walikuwa katika kidato cha nne.

4. Msimamizi wa wanafunzi hao ni Bella (kwa maneno mengine ni kiranja.)

5. Ndiyo, wanafunzi hawa walipokelewa vizuri. Mpokezi wageni aliwaitia Daktari Mkuu pamoja na Muuguzi wake ambao waliwaelezea kila kitu walichotaka kujua. Maneno ya wanafunzi wenyewe wanaonyesha kwamba wamefurahi.

6. “Asiyefika kwa mfalme hudanganywa mengi”. Msemo huu unamaanisha kwamba usipotembea hutajua ukweli wa mambo. Usipotembelea mahali fulani, kila yeyote aliyekuwa hapo anaweza kukudanganya.

7. Baada ya kupata maelezo tofauti kuhusu hospitali, wanafunzi walimwahidi Daktari kwamba watafanya kila kiwezekanacho nao wageuke madaktari, wasaidie wagonjwa.

8. Kulingana na namna mazungumzo yalivyoendelea, wanafunzi walielewa walivyoonyeshwa. Walishukuru kwa maelezo waliyopewa, yaani waliridhika.

**ZOEZI LA 3:** (ukurasa wa 16)

Wanafunzi waelekezwe jinsi ya kufanya kazi hii kwa kuchagua neno moja katika maneno yaliyopendekezwa.

1. c. Ziara ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Ntende kwenye hospitali.

2. d. Vifaa vya hospitalini.

3. b. Kuzalia wajawazito

4. d. Wagonjwa hospitalini.

5. c. Kufungia kidonda

### 1.4.2. Msamiati kuhusu mazingira ya hospitali

**ZOEZI LA 4:** (ukurasa wa 19)

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kueleza maneno waliyopewa. Mwalimu achunguze kwamba wanafunzi wanaeleza maneno ipaswavyo.

1. Kudunga: kuchoma kwa kitu chenye ncha.

2. Matibabu: dawa na huduma inayotolewa kwa kumtibu mgonjwa.

3. Mgonjwa: mtu aliye na maradhi au maumivu fulani katika mwili wake.

4. Hali mahututi: hali ya mgonjwa kukaribia kufa.

5. Kupenyeza: kulazimisha kitu kiingie mahali penye uwazi mdogo.

6. Kuhifadhi: kuweka mahali pa salama.

7. Uchafu: hali ya kutokuwa safi, taka.

8. Mjamzito: mwanamke mwenye mimba.

9. Kujifungua: kuzaa.

10. Dharura: shughuli au jambo la haraka linalotokea bila ya kupangwa au kutazamiwa.

Katika kutumia maneno haya katika sentensi, mwalimu atawaongoza wanafunzi kutumia maneno yaliyoelezwa katika sentensi kamili na zenye maana.

**ZOEZI LA 5**: (ukurasa wa 19)

Mwalimu awaongoze kuhusisha maneno yanayopatikana katika sehemu A na maana zake katika sehemu B kwa kutumia mshale au kwa kuandika neno na maelezo yake.

1. h.

2. a.

3. b.

4. f.

5. c.

6. g.

7. e.

8. i.

9. j.

10. d.

**ZOEZI LA 6:** (ukurasa wa 20)

Wanafunzi wataelekezwa namna watakavyochagua neno moja na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.

1. chumba cha matibabu ya dharura

2. plasta

3. kuhifadhia baadhi ya dawa

4. sindano

5. eksirei.

### 1.4.3. Sarufi: Matumizi ya kiambishi -nge-

**ZOEZI LA 7:** (ukurasa wa 20)

Wanafunzi wajadili kuhusu maana ya sentensi hizi zenye kiambishi nge.Mwalimu awasaidie kutoa maelezo ipaswavyo.

1. Tungetembelea hospitali hii mwaka jana, tungejua haya yote tayari.
    - Hii inamaanisha kwamba sisi hatukuitembelea hospitali hii mwaka jana, na kwa hali hiyo hatukujua mambo ya hospitali. Msemaji hapa anajuta kuwa wao hawakutembelea hospitali.

2. Mngeenda kuyatembelea mashirika mengine, mngeelewa zaidi kuhusu vifaa tofauti na majina maalumu ya wafanyakazi.
    - Kwa maneno mengine, kauli hii inamaanisha kwamba wanafunzi hawa wakiyatembelea mashirika mengine, wataelewa zaidi kuhusu vifaa tofauti na majina maalumu ya wafanyakazi. Ni ushauri.

3. Sisi tungekuwa kama nyinyi, tungewasaidia wagonjwa wa aina tofauti kama mnavyofanya.
    - Hii inamaanisha kwamba sisi si kama nyinyi, na kwa hiyo hatuwezi kuwasaidia wagonjwa kama mnavyofanya. Hili ni juto.

**ZOEZI LA 8:** (ukurasa wa 20)

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wajadili kuhusu maana ya sentensi yenye kiambishi -nge-. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi anashiriki.

## Mifano ya sentensi hizo:

1. Tungekuwa na muda wa kutosha, tungezungumzia mengi kuhusu mazingira ya hospitali.
2. Watoto wale wangejifunza vizuri, wangepewa zawadi nyingi.
3. Angejua Kiswahili vizuri, angeajiriwa kama mwalimu wa Kiswahili.
4. Tungeamka mapema, tungemuona kiongozi.
5. Wangezingatia mawaidha ya mwalimu, wangeepuka na adhabu waliyopewa.

**ZOEZI LA 9:** (ukurasa wa 22)

Mwalimu aombe kila mwanafunzi kukamilisha sentensi kwa kutumia kiambishi –nge- kwa maneno yao. Mwalimu awaombe kuandika majibu yao ubaoni ili awasaidie kusikosoelea.

1. Tungepanda miti kwenye milima, mashamba yetu yasingeharibiwa na mmomonyoko wa ardhi.
2. Wangejua nia yangu katika kutetea haki za wanawake,wangeungana namini katika harakati hizi.
3. Ungeonana na daktari, ungeshauriwa kutotumia dawa za kulevya.
4. Barabara zote zingekuwa za lami, kila eneo nchini Rwanda,lingekuwa na wasafiri wengi.
5. Wanafunzi wangeelewa somo vizuri, wangefaulu mitihani yao.
6. Wazazi wangesikia shauri kutoka walimu wa watoto wao, wangewasaidia watoto kuyarudia masomo.
7. Wangejua kuwa usafi hospitalini ni kitu muhimu sana, wasingetupa taka ovyo.
8. Wangejuwa kwamba malaria husababishwa na mbu, wangetumia chandarua kila usiku.
9. Wangechezea kiwanjani mwao, wangefunga magori mengi.
10. 1Wangejua Kamali ametoka hospitalini, wangemjulisha habari za harusi za dada Mugeni.

### 1.4.4 Matumizi ya Lugha:

**ZOEZI LA 10:** (ukurasa wa 22)

Mwanafunzi ahusishe vifaa katika kundi A na majina katika kundi B akisaidiwa na mwalimu.

1. sindano
2. vidonge
3. kipimajoto
4. mizani
5. bendeji
6. machela

**ZOEZI LA 11:** (ukurasa wa 23)

Kwa kufanya zoezi hili, mwanafunzi atataja zahanati aliyoitembelea (wakati na mahali ilipo) kwa kusisitizia majengo, vifaa alivyoviona na wafanyakazi aliowakuta zahanati.

### 1.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**ZOEZI LA 12:** (ukurasa wa 23)

Mwalimu atawapa nafasi wanafunzi ya kuwasilisha maigizo yenyewe. Lazima wanafunzi watumie majina ya vifaa vya hospitali na ya wafanyakazi. Mwalimu ampe kila mwanafunzi fulsa ya kuwasilisha. Mwalimu aongoze kazi ya wanafunzi na kuhakikisha kwamba wote wanashiriki kwenye kazi hiyo.

### 1.4.6. Kuandika

**ZOEZI LA 13:** (ukurasa wa 23)

Wanafunzi watunge mazungumzo kuhusu vifaa na wafanyakazi wa hospitalini wakizingatia matumizi ya kiambishi "-nge-". Hapa, mwalimu aombe wanafunzi kuelekeza fikra zao kwenye matumizi ya msamiati wa hospitali.

# SOMO LA 2: USAFI WA MAZINGIRA YA HOSPITALI

## 2.1. Ujuzi wa Awali

Mwalimu aulize wanafunzi mmoja kwa mmoja maswali tofauti kuhusu somo lililotangulia kwa kuchunguza ikiwa wanakumbuka vifaa na wafanyakazi watumikao hospitalini. Baada ya kujibu maswali hayo, mwalimu aambie wanafunzi kuchukua vitabu vya Kiswahili na kutazama mchoro.Kisha awaulize wanafunzi maswali kuhusu mchoro walioutazama.

Mwalimu anaweza kuwauliza maswali yafuatayo:

- Ni watu gani unaowaona kwenye mchoro?
- Watu unaowaona kwenye mchoro wanafanya nini?
- Unaowaona wanatumia vifaa gani?

Kutokana na maswali aliyouliza na majibu aliyotolewa, mwalimu aombe wanafunzi wajaribu kufumbua somo linahusu nini.

## 2.2. Zana au vifaa vya Kujifunzia

- Mchoro wa watu wanaosafisha mazingira hospitalini,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Kamusi ya Kiswahili sanifu,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu.
- Ubao,
- Chaki,
- Kalamu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu wanafunzi wanaohitaji msaada maalumu.

## 2.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Mwalimu aandike kichwa cha somo ubaoni, pamoja na malengo mahususi ya somo husika. Baada ya kuunda makundi ya wanafunzi kulingana na idadi ya vitabu vilivyoko, mwalimu awaombe wanafunzi wafungue kwenye ukurasa husika na kusoma kwa kimya kifungu cha habari kuhusu "Usafi hospitalini" huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao.

Hatimaye mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu walichosoma kuhakikisha kuwa wamekielewa. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya na kuelewa, mwalimu awaombe wanafunzi mmoja baada ya mwingine kusoma kwa sauti inayosikika kifungu kilichopo. Mwalimu aongoze wanafunzi kueleza maana ya maneno mapya yaliyomo kifunguni. Halafu mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao wafanye mazoezi yapatikanayo kwenye kitabu cha mwanafunzi na mwalimu atoe msaada kunapohitajika. Mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi katika makundi yao kisha awaongoze kusahihisha ubaoni.

## 2.4 MAJIBU

**ZOEZI LA 1:** (ukurasa wa 24)

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watazame mchoro kwenye ukurasa husika kisha waeleze wanayoyaona yanayohusiana na usafi hospitalini.

### 2.4.1. Maswali ya Ufahamu

1. b.

2. Hapa mwalimu achunguze ikiwa mwanafunzi amezungumzia usafi wa mwili, nguo, vifaa, malazi, vyakula na vinywaji. Kwa mfano: Vyakula na vinywaji vikiwa safi magonjwa mbalimbali yataepukika.

3. Mazingira yakiwa safi hatutakuwa wagonjwa wakati huo hatutatumia pesa zetu kwa kugharamia matibabu kutokana na magonjwa. Pesa hizo zitatumiwa kwa shughuli nyingine za kimaendeleo..

4. i) nzi: husambaza magonjwa mbalimbali kama vile kipindupindu ambacho ni ugonjwa wa hatari unaoambatana na dalili ya kuharisha na kutapika mfululizo..

ii) mbu: husambaza ugonjwa wa malaria.

5. Ugonjwa wa kipindupindu husababishwa na nzi anapogusa kinyesi cha binadamu na kisha kukipeleka katika chankula au maji ya kunywa.

6.i) jalala:  sehemu ya kuhifadhi taka nyingi.

ii) bwelasuti: aina ya vazi maalumu ambalo huvaliwa juu ya nguo za kawaida ili kukinga na uchafu hasa wakati wa kufanya kazi.

7. Wadudu wengine wanaosababishwa na uchafu ni kombamwiko, chawa, kiroboto, kunguni, papasi, na nzi.

Tanbihi: Mwalimu atachunguza majibu ya kila mwanafunzi kutokana na mdudu aliyetaja kwa sababu wadudu ni wengi.

### 2.4.2. Msamiati kuhusu Usafi Hospitalini

**ZOEZI LA 2:** (ukurasa wa 26)

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi katika makundi yao. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kutoa majibu kama vile: Usafi nyumbani ni jambo linaloweza kutiliwa maanani na kila mtu.Wadudu ndio wanyama wanaoweza kuambukiza magonjwa kwa urahisi.Mwalimu achunguze ikiwa sentensi za wanafunzi ni sahihi kisarufi.

**ZOEZI LA 3:(ukurasa 26)**

Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi wawili wawili kuhusisha maneno na maana zake. Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi katika kundi alitoa mchango wake.

1. d.

2. e.

3. a.

4. b.

5. c

**ZOEZI LA 4**: (ukurasa wa 27)

Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Wawasilishe kazi yao kisha mwalimu akosoe makosa.

1. huchangia parefu

2. wangezingatia

3. vifaa

4. viroboto

5. bwelasuti

6. nyasi

7. viroboto wa panya

8. nyoka

**ZOEZI LA 5:** (ukurasa wa 27)

Wanafunzi wawili wawili, tajeni majina ya vifaa vifuatavyo ambavyo hupatikana katika mazingira ya hospitali pamoja na umuhimu wake.

1. ufagio: kuondolea taka sakafuni au ardhini

2. sabuni: kufulia, kuogea au kusafishia vitu

3. kitambaa cha maji: hutumiwa kwa kujifutia maji.

4. viatu vya daktari: hutumiwa kwa minajili ya kutochafusha mahali wanapofanyia kazi.

5. debe la taka: hutumiwa kwa kutilia uchafu.

6. chandarua: kumkinga mtu asiumwe na mbu anapolala.

7. glovu: kumkingia vidole ili asijeruhiwe au asichafuliwe na vitu tofauti.

9. choo: hutumiwa mtu anapotaka kujisaidia.

2.4.3. Sarufi:Matumizi ya Kiambishi -ngeli-

**ZOEZI LA 6:**(ukurasa wa 28)

Mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi hili kibinafsi. Mwalimu asahihishe makosa yanayoweza kujitokeza.

1. Wanafunzi wangelisoma vizuri, wangelifaulu mtihani wa taifa.

2. Mungu huwapenda watu; asingeliwapenda, asingeliwaumba.

3. Tusingeliandika vitabu, tusingelipata vitabu vya kufundishia.

4. Wao wangelikuwa Wakristo, wangeliwasaidia walemavu.

Sentensi hizi ingawa zinatumia -ngeli- badala ya -nge- hazitofautiani kimaana na zile za awali. Yaani tunaweza kutumia kiambishi kimoja badala ya kingine bila kubadilisha ujumbe wa sentensi.

**ZOEZI LA 7** (ukurasa wa 29)

Wanafunzi wakamilishe sentensi kwa maneno yao.


Hii ni mifano ya jinsi wanavyoweza kukamilisha sentensi hizi.

1. kingelitumiwa na wageni
2. kisingelitumiwa na wageni
3. usingeliliwa na watu wengi
4. ingeliwafaidi
5. isingeliwafaidi
6. angelishinda
7. ningeliwahudumia wagonjwa
8. tungelinunua magari
9. ungelitusaidia
10. wangelipika pilau

## 2.4.4 Matumizi ya Lugha

**ZOEZI LA 8:** (ukurasa wa 30)

Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Wawasilishe kazi yao. Mwalimu asahihishe makosa.



**ZOEZI LA 9**: (ukurasa wa 30)

Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi watatu watatu. Wanafunzi wafanye zoezi na kuwasilisha mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa.

- **Glovu:** Kitu kama soksi kinachovaliwa mkononi ambacho hutengenezwa kwa mpira, ngozi au kitambaa na kwa kawaida huwa na nafasi kwa kila kidole.
- **Machela:** Kitu kama kitanda, agh. hutumiwa kubebea mtu aliye mgonjwa au maiti.
- **Dobi:** Mtu anayefanya kazi ya kufua na kupiga pasi nguo za watu kwa malipo.
- **Sabuni:** Mchanganyiko wa vitu vinavyotokana na mafuta na aina mojawapo ya magadi na ambayo hutumiwa kwa kufulia, kuogea au kusafisha vitu.
- **Nesi:** Mwuguzi wa wagonjwa hospitalini.
- **Makasi:** Kifaa kinachotengenezwa kwa madini, agh. ya chuma, chenye visu viwili vilivyounganishwa kwa msumari mdogo na tundu mbili za kuingizia vidole, kinachotumiwa kukatia kitu k.v. nguo au nywele.
- **Plasta:** Kitu kama gome gumu kilichotengenezwa kwa unga maalumu na kitambaa kinachofungwa sehemu ya mwili iliyovunjika ili kushikanisha mifupa iliyovunjika.

### 2.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10:** (ukurasa wa 31)

Zoezi hili linaweza kufanywa na mwanafunzi binafsi au kundi la wanafunzi. Mwalimu atathmini ikiwa mawazo makuu yamezungumziwa. Kwa mfano:

- kutojali usafi wa mazingira kwa watu wengi,

- usafi wa hospitali ni nini?

- namna ya kusafisha mazingira ya hospitali,

- wajibu/mchango wa kila mtu.

### 2.4.6. Kuandika

**ZOEZI LA 11:** (ukurasa wa 31)

Mwalimu awaambie wanafunzi (kila mmoja) kutunga kifungu chenye mada ifuatayo “Umuhimu wa usafi hospitalini kwa kutumia maneno : usafi, kuhara, wadudu, vyoo, mazingira, uchafu

# SOMO LA 3: ADABU HOSPITALINI

## 3.1. Utangulizi/Marudio

Mwalimu aanze somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi wake. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu ajue hali za wanafunzi na baadaye awaulize maswali machache kuhusu somo lililopita. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kujibu maswali hayo na kuwachangamsha kidogo hivi akielekeza maswali yake kwenye somo jipya. Baadaye, mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kuwapa kazi hii:

- *Tazameni mchoro hapo juu kisha mtoe maoni yenu kuhusu kile kinachoonekana kwenye mchoro huo.*

## 3.2. Vifa vya Kujifunzia

Kwa minajili ya somo kuweza kufika kwenye malengo yake, mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo lake. Mwalimu atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Michoro au picha za maeneo mbalimbali ya hospitali,
- Kompyuta,
- Projekta ya kuonyesha picha kutoka mtandao ikiwa yupo,
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule na upatikanaji wa vifaa mbalimbali. Mwalimu kwa ubunifu wake anaweza kuandaa vifaa mbalimbali vya kumsaidia kufanikisha somo lake.

## 3.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake hivi akitilia mkazo mbinu zifuatazo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne. Ni vizuri kutozidi idadi ya watu watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inafanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana. Baada ya kazi, mwalimu aombe makundi kuwasilisha matokeo kwa darasa. Kazi katika makundi itiliwe mkazo kwa kusaidia wanafunzi kushirikiana na kujifunza kutoka kwa

wenzao.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake. (Asome kifungu cha habari mwenyewe au afanye zoezi mwenyewe).
- **Maswali na majibu:** Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzake iwezekanavyo. Mwalimu ajaribu kuweka maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati yake na wanafunzi ama wanafunzi na wanafunzi. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wote wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali na wao wamjibu, na vile vile wanafunzi wamwulize mwalimu na wanafunzi wengine wajibu, mwisho wake mwalimu naye atoe majibu yake.
- **Maelezo ya mwalimu:** Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake, kisha atambuwe ujuzi unaohitaji maelezo yake binafsi. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee vya kutosha wanafunzi wake somo kwa kusisitizia kasoro aliyoitambua. Ni vizuri kufanya hivi kwa kuwapa pia wanafunzi fursa ya majadiliano kuhusu maelezo yake.

## 3.4 Majibu

**ZOEZI LA 1:** ( ukurasa wa 32)
Mwalimu awaombewanafunzi kutazama mchoro husika kisha wajadili wanayoyaona kwenye mchoro.

### 3.4.1. Kusoma na Ufahamu

### Maswali ya ufahamu

1. Watu wanaozungumziwa katika kifungu hiki ni Mugisha, Semana, Daktari Mkuu, vijana wawili waliokuwa wanagombana na polisi.

2. Watu hawa walikuwa hospitali.

3. Tangazo linalozungumziwa linahusu sheria zinazotarajiwa kuzingatiwa na mtu yeyote anayekuwepo hospitalini

4. Tangazo hilo lilikuwa limebandikwa kwenye ukuta. Semana ndiye alisoma tangazo.

5. Vitu ambavyo haviruhusiwi hospitalini ni hivi vifuatavyo: kugombana, kutukana, kuiba, kuwadharau watu wengine, mtu yeyote wa nje haruhusiwi kuingia katika kungawi, kuvuta sigara, kupiga kelele wakiwa katika wodi, kuingiza na kutumia pombe pamoja na dawa za kulevya.

6. Hivi ni vyumba ambamo wahudumiwa huhitaji faragha kwa kuwa wao huvuliwa nguo

wakati huo huo. Na wana owahudumia huhitaji uhuru wowote wa kutoambiwa neno lolote wanapoingia chumbani humo.

7. Kitu kilichosababisha vijana wawili kugombana ni kuwa mmoja alisingizia mwingine kuwa amemwibia chupa ya pombe.

8. Wao walivunja sheria ya pili (ambayo inakataza watu kugombana) na sheria ya nane (ambavyo inakataza kuingiza pombe hospitalini).

9. Vijana hao waliamuliwa kupelekwa kwenye kituo cha polisi waadhibiwe.

10. Jambo linalokudhihirishia kuwa Mugisha alisikitishwa na mapigano ya vijana hao ni kuwa tangu siku hizo aliamua kuwaonya watu wote waheshimiane na kuzingatia maagizo ya Madaktari ili wasipate adhabu zisizostahili.

11. Mugisha na nduguye walifurahia uongozi wa hospitali yao kwa sababu uongozi wa hospitali ulitilia mkazo kuwahimiza watu kuwa na maadili na mienendo mizuri.

12. Ndugu yake Mugisha alisema kuwa kugombana ni tabia ambayo inafaa kupigwa marufuku.

### 3.4.2. Msamiati kuhusu Adabu Hospitalini

**ZOEZI LA 2:**( ukurasa wa 3)
Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafu5nzi wawili. Kila kundi liwasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu akosoe makosa yanayoweza kujitokeza.

1. **Mwiko**: kitu ama jambo analozuiwa mtu kufanya kwa kuogopa kudhurika.

2. **Marufuku:** hali ya kuzuia jambo lisifanywe kamwe.
3. **Benchi**: bao la kukalia.
4. **Ghafla:** kwa kushtukia/bila ya kutarajia.
5. **Afya**: hali nzuri ya mwili/bila ya maradhi.
6. **Mhudumu:** mtu afanyiae kazi mtu mwengine.
7. **Kujeruhi**: tia jeraha.
8. **Kugombana:**kuzuana rabsha au fujo kwa kutoeana maneno makali.

**ZOEZI LA 3:** ( ukurasa wa 35)

*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwalimu akosoe makosa.*
1. kuvunja sheria
2. heshima
3. maadili mema
4. kupiga kelele
5. kugombana

**ZOEZI LA 4**:( ukurasa wa 35)

*Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Wawasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu akosoe makosa yanayoweza kujitokeza.*

1. hawakuwatenganisha
2. kuhudumiwa
3. kutazama
4. pombe
5. wasingalipigana
6. kuvuta
7. benchi
8. sheria

**ZOEZI LA 5:**( ukurasa wa 36)

*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwanafunzi afanye zoezi hili. Mwalimu asahihishe makosa yanayoweza kujitokeza.*

| Mambo yanayokatazwa katika tangazo | Mambo yanayoruhusiwa kufanywa katika tangazo |
|---|---|
| 1) kupigana<br>2) kuingiza pombe<br>3) kuvuta sigara kwenye watu wengi<br>4) kutukana | 1) kuheshimu<br>2) kuwa na moyo wa huruma<br>3) kuwasaidia wasiojiweza<br>4) kuwa na usafi |

### 3.4.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi -ngali-

**ZOEZI LA 6:**( ukurasa wa 35)

*Mwalimu ayaunde makundi kulingana na idadi ya wanafunzi darasani. Kila kundi liwasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa.*

1. Ninyi mngalikuwa na muda wa kutosha, **tungali**zungumzia mengine mengi kuhusu adabu.

- Sentensi inamaanisha kwamba ninyi hamkuwa na muda wa kutosha kwa hiyo hatukuzungumzia mengine mengi kuhusu adabu. (kuna juto katika sentensi hii).

2. Watoto wale **wangali**jifunza vizuri, w**angali**pewa zawadi nyingi.

- Maana ya kauli hii ni kwamba watoto wale hawakujifunza vizuri na hali hiyo ilisababisha kutopewa zawadi nyingi. (kuna juto katika sentensi hii).

3. Wanafunzi w**asingali**kuwa na alama za kutosha, wasingalifanya mtihani wa taifa.

- Maana yake ni kuwa wanafunzi walikuwa na alama za kutosha ambazo ziliwawezesha kufanya mtihani wa taifa.

4. Sisi tu**singali**fika mapema, tusingalifanya kazi nyingi.

- Maana ya sentensi hii ni kwamba tulifika mapema na tukafanya kazi nyingi.

**ZOEZI LA 7:** ( ukurasa wa 37)
*Wanafunzi wakamilishe sentensi kwa maneno yao.*
*Hii ni mifano ya jinsi wanavyoweza kukamilisha sentensi hizi.*
1. yasingaliongezeka
2. Dereva huyu asingaliendesha gari kwa kasi
3. nisingalipata
4. watoto wangu wasingalikosa karo
5. dada na mabibi zetu wangaliachwa nyuma katika nyanja zote
6. wangaliniunga mkano
7. angalikutibu haraka
8. wangalikuwa na afya bora
9. kungalikuwa na wageni wengi kutoka nchi za kigeni

**ZOEZI LA 8:**( ukurasa wa 37)
*Zoezi hili lifanywe kibinafsi. Kila mwanafunzi afanye zoezi hili. Mwalimu asahihishe makosa.*
1. Tusingalipanda miti ya kutosha, tusingalizuia mmomonyoko kupasua mlima huu.

2. Bwana yule asingalijua usawa wa kijinsia, asingalikuwa na maendeleokatika familia yake.

3. Usingalikuwa na moyo wa kiutu, usingalimhudumia mwanafunzi mlemavu yeyote darasani.

4.Wanafunzi wasingalisoma kwa bidii , wasingalishinda mitihani kwa urahisi.

### 3.4.4. Matumizi ya Lugha

**ZOEZI LA 9**:( ukurasa wa 37)
*Mwalimu atawaomba wanafunzi kutunga sentensi moja kati ya maneno waliyopewa katika kitabu cha mwanafunzi. Wanafunzi watatunga sentensi kwa kujali matumizi ya alama na vituo. Kwa mfano, wanaweza kutunga sentensi kama zifuatazo:*
1. Tafadhali mwalimu! Nahitaji maelezo zaidi iwapo mtu anahitajika kuwa na adabu awapo sokoni.

2. . Naomba mniruhusu nitetee haki za wanyamapori!

3. Wanafunzi wenzangu waliniunga mkono nikawaambia,asante!

4. Nilipewa pole nilipokuwa ninaumwa.
5. Samahani kwa kuchelewa kufanya ulivyoniambia!

6. Wageni walipofika nyumbani walibisha hodi.
7. Karibu! Ingia ndani!
8. Mdogo anamwamkia mkubwa kwa kusema shikamoo!
9. Shukrani zangu ziwaendee walionisaidia.
10. Jibu la shikamoo ni marahaba.

### 3.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**ZOEZI LA 10:** ( ukurasa wa 38)
*Mwalimu awaagize wanafunzi katika makundi kujadiliana kuhusu mada zifuatazo:*
1. Namna watoto wanaweza kuimarisha adabu mbele ya wazazi nyumbani kwao.
2. Adabu ni msingi wa uhusiano mwema kati ya mtu na mtu mwingine. Eleza.
Wanafunzi wanaweza kutaja umuhimu wa adabu na namna wanavyoweza kuimarisha wanapoishi na wanapotembea.

### 3.4.6. Kuandika

**ZOEZI LA 11:** ( ukurasa wa 38)
Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kufanya kazi za kuandika. Mwalimu achunguze ikiwa mwanafunzi amezungumzia mambo yanayohusiana na adabu na ameandika bila makosa ya kimaandishi na ya kisarufi. Mwalimu asahihishe kazi zote zilizofanywa na wanafunzi.Mwalimu asisitize kuhusu hati nadhifu na inayosomeka kwa urahisi. Mwalimu akumbuke kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali yaliyotajwa.

## 3.5Muhtasari wa Mada

Mada hii ya kwanza "Msamiati katika mazingira ya hospitali" ina vipengele vitatu yaani masomo makuu matatu yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo vidogo kama vile: mchoro, kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, matumizi ya lugha, kusoma na kuandika, sarufi na maelezo muhimu. Somo la kwanza linaeleza majina ya vifaa na wafanyakazi wa hospitalini. Somo la pili linaeleza usafi wa mazingira ya hospitali. Somo la tatu linaeleza adabu hospitalini.

## 3.6. Maelezo ya Ziada

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mwalimu. Sehemu hii inamsaidia mwalimu kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada.

## 3.7. Tathmini ya Mada ya Kwanza

Hii ni kazi ya kupima maarifa, ufahamu na stadi ambazo mwanafunzi amepata kutokana na yale aliyojifunza katika sura husika. Mwalimu asahihishe hadharani mazoezi yote ili wanafunzi waweze kujua ni makosa gani ambayo wameyafanya.

## 3.8 Soma maswali yafuatayo na kujibu:

1. Vitu muhimu vinavyopatikana katika mazingira ya hospitali au zahanati ni kama: machela, vidonge, sindano, ambulensi, bwelasuti, ..........

2. Sehemu za hospitali ni kama: maabara, chumba cha dawa, kungawi, chumba cha upasuaji, chumba cha matibabu ya kina, ................

3. Wafanyakazi wa hospitalini ni kama: Daktari Mkuu, muuguzi, mfamasia, dobi, karani, ............

Majukumu yao ni kutibu na kuwasaidia wagonjwa hospitalini au zahanati.

4. Mambo muhimu yanayotakiwa kupendekezwa hospitalini kwa ajili ya usafi ni haya yafuatayo: kusafisha vyumba vya wagonjwa, kutengeneza bustani zinazozunguka hospitali, kutumia dawa za kuulia wadudu wenye kuambukiza watu magonjwa mbalimbali, .................

5. Tunaweka chandarua juu ya kitanda kwa minajili ya kujilinda kuumwa na mbu unaoambukiza ugonjwa wa malaria. N kuendeleza usafi ilikujiepusha na uingiaji magonjwa yanayoambukiza.

6. Si vizuri kwa wagonjwa kuchangia taulo moja kwa sababu mmoja akiwa na ugonjwa fulani kwenye ngozi yake, ugonjwa huo utaambukizwa kwa mgonjwa mwingine. Hii ndiyo njia nzuri ya kutumiwa ili kuepukana na madhara yanayoweza kujitokeza.

- *Mwalimu awaelekeze wanafunzi kujadili hasara zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya taulo moja kwa watu zaidi ya mmoja katika aya nne kwa kutumia Viambishi vya -nge- , -ngeli- na – ngali- .*

## II. Eleza maana za sentensi zifuatazo kwa kuzingatia hali ya masharti inayojidhihirisha:

1. Ningejua kuwa madawa ya kulevya huharibu afya kwa kiwango hiki, ningeshirikiana awali na ngazi za usalama.

- Sentensi hii inamaanisha: Mimi sikujua kwamba dawa za kulevya huharibu afya kwa kiwango hiki, na hali hiyo ilisababisha mimi kutoshirikiana na ngazi za usalama. (Sentensi hii inaonyesha juto)

2. Tungalisaidiana na polisi dhidi ya bidhaa bandia, tungaliboresha afya nchini.

- Maana ni kwamba tukisaidiana na polisi dhidi ya bidhaa bandia, tutakuwa tunaboresha afya nchini. (sentensi hii inaonyesha pendekezo)

3. Angelitumia kondomu, asingeliambukizwa na UKIMWI.

- Sentensi hii inamaanisha kwamba yeye hakutumia kondomu na

akaambukizwa na UKIMWI. Kuambukizwa na UKIMWI kwake kulisababishwa na kutotumia kondomu kwake. (Sentensi hii inaonyesha juto)

**III. Kanusha sentensi zifuatazo kwa kuzingatia mabadiliko ya maana yake:**

1. Tusingelipanda miti ya kutosha, tusingelizua mmomonyoko kupasua mlima huu.

2. Bwana yule asingalijua usawa wa kijinsia, asingalikuwa na maendeleo ya kumudu katika familia yake.

3. Usingekuwa na moyo wa kiutu, usingemhudumia mwanafunzi mlemavu yeyote darasani.

4. Nchi yetu isingelifunga macho juu ya ueneaji wa ugonjwa wa UKIMWI, watu wengi wasingeliathiriwa.

5. Wanasiasa waliopanga mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi wangelifikiria kesi za kisheria dhidi yao, wangaliogopa kuwashirikisha raia.

IV.
1. debe la taka
2. glovu
3. marashi/manukato
4. karatasi ya usafi

## 3.9. Mazoezi ya Ziada

### 3.9.1. Mazoezi ya urekebishaji

*Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia msamiati huu (dawa za kulevya, maabara, jalalani, kukojoa, karatasi ya usafi).*

1.Unaposikia haja ndogo inakatazwakukojoamahali pasipofaa.
2.Takataka zote kutoka maeneo ya hospitali ni lazima zitupwejalalani
3. **Dawa za** kulevya ni tishio kubwa kwa afya ya binadamu hasa kwa wagonjwa.
4. Unapokwenda haja kubwa ni lazima kutumia karatasi ya usafi na kunawa miko-no baadaye.
5. Hairuhusiwi kuingia kiholela katikamaabarawakati ambapo wewe si mkazi wa hapo.

### 3.9.2. Mazoezi jumuishi

**Eleza matumizi ya kila kifaa kati ya hivi vifuatavyo:**

a)Bendeji: **hufungia jeraha, kidonda au mahali palipoumia.**
b)Kipimajoto: **kupimia joto**.
c)Kipimamwili: **kusikiliza mapigo ya moyo na upumuo wa mapafu ya mgonjwa.**
d)Sindano: **kupenyezewa dawa katika mwili wa mtu aua mnyama.**
e) Machela: **kubebea mtu aliye mgonjwa au maiti.**

### 3.9.10. Mazoezi nyongeza

**Kamilisha kifungu kifuatacho kwa kutumia maneno yafuatayo: mifugo, mvua, huhitajika, lishe, kunyunyizia, hukonda, maeneo, maisha, njaa, wenyeji.**

**Maji**

Maji ni uhai. Maji …**huhitajika**………….katika ……**maisha**……….yetu ya kila siku. Hivyo basi tunahitaji maji ya kunywa, kupikia, kuoshea na kupatia ………**mifugo**………..wetu.
Maji ni muhimu katika kilimo. Mimea haiwezi kustawi bila ya kuwepo maji hasa ya mvua ama ya …………**kunyunyuzia** …………Ma**neo**……………….. ya nchi ambayo hayana……**mvua**………..au mito hayavutii watu wengi kuishi humo. …………**Wenyeji**…………..wa sehemu hizo hukabiliwa na ………**ukame**………..miaka nenda miaka rudi. Baadhi yao hufa kwa ……njaa………….. Wengine wao ……**hukonda**……..na kuwa wembamba kama sindano kwa ajili ya kukosa…………**lishe**………………bora.

## SOMO LA 4: MICHEZO SHULENI

### 4.1. Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu michezo shuleni. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Maswali haya yatakuwa na uhusiano wa karibu na michezo.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu msamiati wa michezo kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha mwanafunzi.Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo :

- Unaona nini kwenye mchoro?
- Ni shughuli zipi unazoziona kwenye michoro?
- Kuna uhusiano gani kati ya kichwa cha habari na michoro?

### 4.2. Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Ubao,
- Chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

### 4.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo mambo yafuatayo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumushirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/ mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).

- **Maswali na majibu:** mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.

- **Maelezo ya mwalimu:** mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

- **Majadiliano:** mbinu hii itawapa wanafunzi uwezo wa kujadiliana kuhusu kazi watakayopangiwa na mwalimu.

- **Utafiti:** mbinu hii itawaruhusu wanafunzi kutafuta maelezo zaidi kuhusu kazi watakazopangiwa na mwalimu. Wataweza kutafuta habari mbalimbali katika vitabu vya maktabani au kwa kutumia tovuti. Wataweza tena kujadiliana na watu wengine wa nje ya darasa lao.

## 4.4 Majibu

**Zoezi la 1**: *ukurasa wa 30*
Wanafunzi wawasilishe wanaoyaona kwenye mchoro na baadaye wayawasilishe mbele ya darasa. Mwalimu awasaidie ipaswavyo walio na matatizo maalumu.

### 4.4.1. Maswali ya Ufahamu

1. Shule zinazozungumziwa katika kifungu hiki ni Shule ya Sekondari ya Menge na Shule ya Sekondari ya Mudehe.

2. Mchezo wa mpira wa miguu una majina mengi kama: soka, kabumbu, na kandanda.

3. Uongozi wa shule yetu ulichangia kwa kuimarisha michezo mbalimbali katika shule yetu. Tuliruhusiwa kufanya mkutano kila Jumamosi kwa minajili ya kuzungumzia habari za michezo mbalimbali na umuhimu wa michezo. Zaidi ya hayo, viongozi walitununulia jezi, viatu vya mpira, mipira, nyavu na vifaa vingine ambavyo vinahitajika katika michezo.

4. Michezo mingine tuchezayo shuleni ni mpira wa wavu, mpira wa kikapu na mingineyo.

5. Kalisa ndiye hodari wa taarifa zote za michezo na hupewa muda wa kuwasimulia wenzake jinsi ambavyo wachezaji hufaidika kwa vipawa vyao katika shughuli za michezo.

6. Timu ya Shule ya Sekondari ya Menge ni hodari kuliko timu ya Shule ya Sekondari ya Mudehe. Shule hiyo ilifunga timu ya Sekondari ya Mudehe mabao mawili kwa nunge. Pia ilishinda mashindano ya mkoa. Zaidi ya hayo ilijinyakulia kombe la kitaifa.

7. Kati ya timu mbili zilizocheza, moja tu (timu ya Shule ya Sekondari ya Menge) ndiyo iliibuka mshindi, wakati ambapo ile nyingine iligeuka mshinde. Timu zote mbili haziwezi kushinda zote. 8. Kwa sababu timu zote mbili zilitoka sare, yaani mchezo ulimalizika wakiwa na sufuri kwa sufuri. Kwa hiyo iliwalazimisha kupiga mikwajo ya penati, timu kutoka Kusini ikapata mikwaju mitatu dhidi ya mikwaju miwili ya timu ya kutoka Mkoa wa Mashariki.

9. Timu kutoka Mkoa Kusini na timu kutoka Jiji la Kigali.

10. Ushindi wa timu ya Menge ulitokana na kujituma kwa upande wa wachezaji, na kulikuwa na mashabiki wengi waliokuwa wanawaunga mkono na kuwatia hamasa wachezaji.

11. Michezo ya riadhani michezo ya viungo vya mwili kama vile kukimbia, kuruka, kuogelea, kutupa mkuki.

12. Mashabiki/watazamaji.

### 4.4.2. Msamiati kuhusu Michezo Shuleni

**Zoezi la 2**:(*ukurasa wa 46)*
*Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Wanafunzi wawasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa.*
1. f
2. h
3.k
4. b
5. i
6. a
7. c
8. g
9. j
10. e
11. d

**Zoezi la 3: (***ukurasa wa 47)*
*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwalimu asahihishe makosa yanayoweza kujitokeza.*

1. pumziko/mapumziko
2. mtangazaji
3. mchezaji
4. mshindi
5. mazoezi
6. kiongozi
7. mshindi

Zoezi la 4:(ukurasa wa 47)
Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwalimu asahihishe makosa.
1. timu
2. michezo
3. riadha
4. soka, kabumbu, kandanda
5. mtangazaji

### 4.4.3. Sarufi: Matumizi ya Majina ya Ngeli ya li- ya-

**Zoezi la 5:**(ukurasa 47)
*Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Wanafunzi wawasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe.*
1. ya-
2. li-
3. ya-
4. ya-
5. ya-

### 4.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 6**:(ukurasa 48)
*Mwalimu ayaunde makundi ya wanafunzi watatu watatu. Wanafunzi wafanye kazi na kuiwasilisha mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa yanayoweza kujitokeza.*

**Zoezi la 7:** (ukurasa 48)
*Mwalimu ayaunde makundi kulingana na idadi ya wanafunzi darasani. Wanafunzi wafanye zoezi na kuwasilisha kazi mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe.*

1. Walianza kucheza baada ya refa kupuliza filimbi.
2. Watu wengi hupenda mpira wa miguu.
3. Baada ya mapumziko, kipindi cha pili kilianza.
4. Michezo ina faida nyingi.
5. Timu ya Gikondo iliongeza mashambulizi zaidi.

### 4.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 8:** (ukurasa 49)
*Kwa ajili ya kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza kupitia zoezi hili, litafanyiwa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, huku mmoja akisoma kifungu husika kwa sauti kubwa na haraka kama mtangazaji habari, mwengine akisikiliza kwa makini ili aweze kuzungumzia darasa yaliyotokea katika mchezo unaozungumziwa. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi katika kundi anashiriki.*

### 4.4.6. Kuandika

**Zoezi la 9:** (ukurasa 49)

*Wanafunzi watunge kifungu kuhusu mpira wa miguu wa timu mbili kwa kutoa hoja na maelezo kamili kwa kutumia majina ya ngeli ya Li-Ya. Mwalimu apitie vifungu vya wanafunzi kwa kutizama makosa ya kisarufi na matumizi ya msamiati.*

**Mambo ya kuzingatiwa:**

Matamshi bora ya maneno ya Kiswahili
Utumiaji wa majina ya Li-Ya- kama vile bao, kundi, jina, lango, chenga, shuti, ……

# SOMO LA 5: FAIDA ZA MICHEZO

## 5.1. Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na faida za michezo katika maisha ya binadamu. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Maswali haya yatakuwa na uhusiano wa karibu na michezo.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu msamiati wa michezo kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo :

- Unaona nini kwenye mchoro?
- Ni faida gani tunazozipata tunapocheza?

## 5.2. Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Ubao,
- chaki,
- Vifaa kama mpira wa kucheza kandanda, mpira wa kikapu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

**Tanbihi:** Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 5.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu  atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo mambo yafuatayo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/ mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).
- **Maswali na majibu**: mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mwalimu:** mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.
- **Majadiliano**: mbinu hii itawapa wanafunzi uwezo wa kujadiliana kuhusu kazi watakayopangiwa na mwalimu.
- **Utafiti**: mbinu hii itawaruhusu wanafunzi kutafuta maelezo zaidi kuhusu kazi watakazopangiwa na mwalimu. Wataweza kutafuta habari mbalimbali katika vitabu vya maktabani au kwa kutumia tovuti. Wataweza tena kujadiliana na watu wengine wa nje ya darasa lao.

## 5.4Majibu

### Zoezi la 1: (ukurasa 50)

Wanafunzi watoe majibu kutokana na wanayoyaona kwenye mchoro wakishirikishwa na mwalimu.

### 5.4.1. Maswali ya Ufahamu

1. - Michezo huisaidia miili ya binadamu kuwa imara na kuwa bila magonjwa kama vile kisukari, mfadhaiko, unene wa kupindukia, na kadhalika.

- Michezo hujenga miili ya binadamu na kuifanya iwe mikakamavu.
- Michezo hutajirisha.
- Michezo hufurahisha wachezaji wenyewe na wengine wanaoitazama.
- Unapopata muda wa kupumzika na kujistarehesha unaweza kuongeza kiwango

chako cha

kufikiri na uwezo wako wa kutenda kazi kwa ufanisi au kusuluhisha matatizo muhimu yanayojitokeza katika maisha ya kila siku.

**Tanbihi:** faida za michezo ni nyingi kuliko zilizotajwa hapo juu inambidi mwalimu atazame majibu ya kila mwanafunzi.

2. Madhara yanayoweza kumpata mtu asiyecheza ni kama ugonjwa wa kisukari, na ugonjwa wa shinikizo la damu.

3. Michezo huhusisha pande mbili (mtu na mtu, kundi la watu na kundi jingine, nchi moja na nchi nyingine). Urafiki hujengeka wakati watu wanapokutana kwa ajili ya kitu kimoja wanachokipenda.

4.Watu wanaojisingizia kuwa hawana kipawa cha mchezo, wanaweza kuonywa kuwa mchezo huhitaji mazoezi tu na kujitahidi , na ina faida katika maisha kwa kujenga miili yetu na kuifanya iwe mikakamavu.

5. Aina za michezo zilizozungumziwa katika kifungu hiki ni hizi zifuatazo: mpira wa miguu, mpira wa wavu, mpira wa kikapu, kuogelea, michezo ya riadha, kuendesha baiskeli, ndondi, mieleka na michezo mingine.

6. Michezo, hasa michezo ya kimataifa, ni mojawapo ya njia ya taifa kujulikana duniani. Kwa mfano, mataifa mengi sasa yameisha julikana kwa uhodari wa wanariadha wao, au wachezaji wengine katika nyanja tofauti. Michezo ya kimataifa ikichezewa nchi fulani, kwa mfano, kutakuwa na wageni wengi kutoka nchi nyingine watakaokuja kuitazama michezo hiyo na kuwashabiki wachezaji kutoka nchi zao, na bila shaka watahitaji kulazwa hotelini, mahali ambapo watalazimishwa kulipa pesa za kigeni.

7. Michezo isiwe kitu cha kufanya mara moja tu ifanywe mara nyingi iwezekanavyo, na ndipo urafiki wa kudumu utajengeka.

8. Watu wengi wameisha julikana kwa uhodari wao katika michezo maalumu, na wanapata pesa nyingi kwa kazi yao hiyo ya kuburudisha watu. Baadhi yao tayari wamegeuka matajiri.

9. Ukizunguka ulimwenguni, mahali popote, utasikia habari za watu waliotajirishwa na michezo. Wao wamewahi kujijengea majumba makubwa katika miji mikuu na kujinunulia magari ya bei ghali. Hawa hupatikana katika nyanja zote za michezo.

### 5.4.2. Msamiati kuhusu Faida za Michezo

**Zoezi la 2:**(ukurasa 52)

Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Wawasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa.

1. mikakamavu
2. uhodari
3. huimarisha
4. hupumzika
5. magonjwa
6. kisukari
7. huwachangamsha
8. uhusiano
9. mwanamchezo

**Zoezi la 3:**(ukurasa 53)

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sentensi watakazotunga ziwe sahihi. Lazima sentensi za wanafunzi zitumie msamiati uliotajwa. Kwa mfano:

- - Mwenyezi Mungu aliwaumba binadamu kwa mfano wake.
- - Nafsi chungu nzima zilipotea katika mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi.
- - Wachezaji wa taifa moja walicheza na taifa jingine.
- - Mimi ninajivunia kuwa raia wa Rwanda.
- - Watazamaji wengi hustareheshanafsi zao wanapoangalia michezo..
- - Wafanyakazi walialikwa kushiriki katika kongamano.
- - Mama na mtoto wake wana uhusiano wa karibu.
- - Mielekani michezo mizuri kwa wasichana.
- - Yeye alikuwa na mwili wenyeukakamavu ambao ulimpatia ushindi.

### 5.4.3. Sarufi: Majina ya Ngeli ya LI-YA-

**Zoezi la 4:**(ukurasa 53)

Mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma kifungu cha habari kuhusu "Faida za michezo" kisha waorodheshe vivumishi vilivyotumiwa katika kifungu. Wanafunzi watachagua vivumishi vya ngeli ya LI-YA-.

Kwa mfano: - Mazoezi **ya** michezo.

- Taifa **lake**....

**Zoezi la 5:**(ukurasa 53)

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga wakitumiamajina ya ngeli ya Li-Ya- pamoja na vivumishi vyake wakifuata mifano waliyopewa katika Kitabu cha Mwanafunzi

Kwa mfano: - Mawe **yake** yameibwa.

-Jeshi **lenyew**elimepata tunu.

- Mabao **yale** yaliingia mfululizo.

**Zoezi la 6:**(ukurasa 54)

Zoezi hili liwe la kibinafsi. Kila mwanafunzi afanye zoezi. Mwalimu akosoe makosa.

1. Majembe yamenikata vibaya.
2. Jiwe limewekwa kando ya barabara.
3. Ondoa jani hili.
4. Jino limeng'oka.
5. Mabega yetu yanatuuma.
6. Majengo haya makubwa ni mapato ya wachezaji hao hodari.
7. Timu za shule zetu zimenunuliwa mabasi yenyewe kama zawadi.
8. Magari mapya yatatumiwa kusafirisha wachezaji.

**Zoezi la 7:** (ukurasa 54)

Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Wawasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa.

1. hili
2. hilo
3. hilo
4. yamekauka
5. la
6. mapya
7. haya
8. lenyewe
9. dogo
10. yao

**Zoezi la 8:**(ukurasa 55)

Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwalimu asahihishe makosa.

1. Magari makubwa hayataelekea mjini Karongi leo.
2. Jino langu bovu halikung'olewa jana.
3. Meno yangu mabovu hayakung'olewa jana.
4. Kawa langu dogo halijakifunika chungu chako kikubwa.
5. Makawa yangu madogo hayajavifunika vyungu vyenu vikubwa.
6. Jitu lile baya halimpigi mtoto bila sababu.
7. Majitu yale mabaya hayawapigi watoto bila sababu.
8. Shati langu halijachafuka.
9. Majina yao hayakuandikwa upya.
10. Hili ni jambo lisilotuhusu sisi.

### 5.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 9:** (ukurasa 56)

Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Wawasilishe kazi kisha mwalimu afanye marekebisho.

1. kustarehe

2. uhusiano

3. riadha

4. uhodari

5. kujenga mwili

6. mazoezi

### 5.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10:**(ukurasa 57)

Mwalimu anaweka wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wajadiliane katika makundi yao. Baadaye mwalimu anahakikisha kwamba kila mwanafunzi ndani ya kundi moja ana mtazamo mmoja kuhusu faida za michezo.Mwisho wake, mwalimu anawapa wanafunzi muda wa kutosha wa kujitayarisha na kuwasilisha faida za michezo mbele ya darasa.

### 5.5.6. Kuandika

**Zoezi la 11:**(ukurasa 57)

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao, kutunga kifungu cha habari kuhusu "Hali ya Michezo ya Wanawake Nchini Rwanda" wakitumia majina ya ngeli ya Li-Ya-. Mwalimu awaongoze kunapohitajika.

**Dhamira hizi ni muhimu kupatikana katika utungaji:**

- Michezo huisaidia miili ya binadamu kuwa imara na kuwa bila magonjwa;
- Michezo hujenga miili ya binadamu na kuifanya iwe mikakamavu;
- Michezo hufurahisha;
- Michezo hupumzisha;
- Michezo ni chanzo cha kujitajirisha.

# SOMO LA 6: MASHINDANO

## 6.1. Ujuzi wa Awali

Somo hili linajishughulisha na mashindano, yaani mapambano baina ya pande mbili au zaidi katika michezo. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Maswali haya yatakuwa na uhusiano wa karibu na michezo.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu msamiati wa michezo kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha mwanafunzi Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo:

- Unaona nini kwenye mchoro?
- Ni faida gani tunazozipata tunapocheza?

## 6.2. Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Ubao,
- Chaki,
- Vuvuzela,
- Vifaa kama mpira wa kucheza kandanda, mpira wa kikapu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

**Tanbihi:** Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 6.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo mambo yafuatayo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/ mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).
- **Maswali na majibu:** mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mwalimu**: mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.
- **Majadiliano**: mbinu hii itawapa wanafunzi uwezo wa kujadiliana kuhusu kazi watakayopangiwa na mwalimu.
- **Utafiti:** mbinu hii itawaruhusu wanafunzi kutafuta maelezo zaidi kuhusu kazi watakazopangiwa na mwalimu. Wataweza kutafuta habari mbalimbali katika vitabu vya maktabani au kwa kutumia tovuti. Wataweza tena kujadiliana na watu wengine wa nje ya darasa lao.

### 6.3.1. Kusoma na Uufahamu:Kifungu kuhusu Mashindano

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha habari kilichopo huku wakiandika msamiati mpya wanaoupata kutoka kifungu hicho.Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu, awaombe kusoma kwa sauti. Mwalimu akumbuke umuhimu wa kusahihisha matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Hatimaye, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha habari walichokisoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa.

### 6.3.2. Ujifunzaji wa Msamiati kuhusu Kifungu

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujibu maswali ya ufahamu, mwalimu awasaidie kuelewa kila swali na baadaye kutoa

majibu kwa wanafunzi.Mwalimu baada ya kusahihisha maswali ya ufahamu, anaongoza kazi ya kutafuta maana ya msamiati. Wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wanatumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu kutafuta maana ya msamiati. Swali jingine ni kuchaguwa kwenye msamiati neno sahihi kati kwa kukamilisha sentensi. Kwa hivyo,mwalimu azunguke katika makundi yote.

### 6.3.3. Sarufi

Kwa kufundisha somo la sarufi, mwalimu atawaomba wanafunzi kuandika sentensi kutoka kifungu cha habari zenye majina ya ngeli ya Li-Ya- na kujadiliana maana zake. Kwa kuendelea kutoa maelezo, mwalimu atawaomba kutunga sentensi tano na kukamilisha sentensi.

### 6.3.4. Matumizi ya Lugha

Mwalimu awaombe wanafunzi wajipange katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili kujadiliana kuhusu mashindano waliyowahi kuhudhuria. Wanafunzi waelezane mashindano mbalimbali yaliyotokea mahali fulani. Baadaye, kila kundi lieleze waliyozungumzia. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Kutokana na majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaombe wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno yanayotumiwa katika mashindano kama fainali, nusu fainali, penati, .....

### 6.3.5. Kusikiliza na Kuzungumza

Hapa mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ambapo atawaomba kusoma mmoja baada ya mwingine. Hapa mwalimu atachunguza mambo muhimu yafuatayo: matumizi ya lugha kwa ufasaha; matumizi ya msamiati na sentensi zenye maana. Ni vyema mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshimara tu yanapojitokeza ili kuwazoeza wanafunzi kutamka kwa usahihi herufi, silabi, maneno na sentensi za Kiswahili.

### 6.3.6. Kuandika

Mwalimu atawaongoza wanafunzi kuandika majina ishirini ya ngeli ya li-ya- kisha waonyeshe umoja na wingi wake.Hapa mwalimu atachunguza kama mwanafunzi anaandika sentensi sahihi, matumizi ya sarufi kwa ufasaha, na kadhalika.

## 6.4 MAJIBU

**Zoezi la 1:** (ukurasa wa 58)

Wanafunzi wajadili wanayoyaona kwenye mchoro. Wanafunzi waitafakari picha iliyotumiwa na wapewe dakika za kutosha za kuitafakari picha husika. Mwalimu awaache wanafunzi watoe maoni yao kuhusu picha iliyotumiwa. Mwalimu akumbuke

kuwasaidia ipaswavyo wanafunzi wenye matatizo mbalimbali.

### 6.4.1 Maswali ya ufahamu

1. Wachezaji mashuhuri waliozungumziwa katika kifungu cha habari pamoja na sifa zao:

- Kalisa: anajulikana kwa kupiga chenga nzuri.
- Karake: anajulikana kwa kushika mpira na kuandika goli kwa kutumia kichwa.
- Mpenzi: anajulikana kwa kurudisha mpira kiwanjani.
- -Kamoso: anajulikana kwa kupiga shuti kubwa

2. Timu ya Jikondo ilionyesha uhodari zaidi kuliko timu ya Gichumbi: wachezaji mashuhuri wote wanaozungumziwa katika kifungu hiki ni wa timu ya Jikondo. Timu hiyo ndiyo iliibuka mshindi (magoli matatu kwa sufuri).

3. Katika kipindi cha kwanza cha mchezo huu, wakati Kalisa wa timu ya Jikondo alitaka kupiga chenga, mchezaji mmoja wa timu ya Gichumbi aliunawa mpira, kitendo kilichosababisha mpira kupelekwa mbele ya mlango wa timu ya Gichumbi, na ndipo goli la tatu la timu ya Jikondo liliingia.

4. Wachezaji wa timu ya Gichumbi walionekana kuwa dhaifu katika kipindi cha pili kwa sababu walikuwa wameisha pigwa magoli mawili katika kipindi cha kwanza cha mchezo huu. Pia, wachezaji wa timu ya Jikondo walijionyesha kuwa hodari kuliko wachezaji wa timu ya Gichumbi.

5. Timu ya Jikondo ilifunga timu ya Gichumbi mabao matatu kwa bila.

6. Timu ya jikondo ilikuwa inasifiwa kwa jina la “Mshindi”.

7. Timu ya Jikondo ilipewa jina la Mshindi kulingana na uzoefu wake wa kushinda timu nyingine, na uhodari wa wachezaji wake. Ni timu bingwa.

8. Katika kipindi cha kwanza, timu hii iliingiza mabao mawili na ikaingiza bao moja katika kipindi cha pili.

9. Ni Karake wa timu ya Jikondo aliyeingiza bao kwa kutumia kichwa.

10. Ukiingia katika mashindano, unataraji vitu viwili: kushinda au kushindwa. Ukitaka kushinda tu na hutaraji kushindwa, unaposhindwa wewe huvunjika moyo, na hali hiyo inaweza kusababisha wewe kutoingia tena katika mashindano.

### 6.4.2. Msamiati kuhusu Mashindano

**Zoezi la 2:** (ukurasa wa 60)

Zoezi hili lifanywe kibinafsi. Mwalimu arekebishe makosa.

1. d

2. g

3. f

4. a

5. b

6. h

7. e

8. c

**Zoezi la 3:** (ukurasa wa 60)

Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwalimu asahihishe makosa.

1. penati

2. ushindi

3kocha

4. mlinda mlango

5. mwamuzi

6. hodari

### 6.4.3. Sarufi: Matumizi ya Vivumishi vya Kuuliza, vya Idadi na vya Sifa.

Mwalimu ayaunde makundi ya wanafunzi watatu watatu. Wawasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa.

| **vivumishi vya idadi** | **vivumishi vya sifa** |
| --- | --- |
| - chenga tatu | - Shuti kali |

- goli la kwanza

- mabao matatu

- goli la pili

**Zoezi la 4:** (ukurasa wa 61)

Zoezi lifanyike kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Kila kundi liwasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa.

1. yapi
2. mawili
3. lipi
4. mengi
5. zuri
6. matatu
7. lenyewe
8. lipi?
9. yake
10. lilifungwa

### 6.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 5:**(ukurasa wa 63)

Mwanafunzi apange maneno kwa utaratibu unaofaa ili yaweze kuleta maana katika sentensi kamili. Mwalimu aongoze kazi ya wanafunzi na kuhakikisha kwamba wote wanashiriki kwenye kazi hiyo.

**Kwa mfano:**

1. Wachezaji wake walikuwa wanapasiana mpira haraka haraka.
2. Timu ya Rubavu ilishinda timu ya Bugesera magoli matatu kwa sufuri.
3. Suala la michezo linazungumziwa mno siku hizi shuleni.

4. Wanafunzi wanatumia majina ya ngeli ya Li-Ya- katika umoja na wingi.

5. Haya ni matokeo ya mimea tuliyoipanda.

### Zoezi la 6:(ukurasa wa 64)

Mwalimu awaombe wanafunzi kutumia maneno katika sentensi sahihi na zenye maana. Mwalimu anasaidia wanafunzi kutumia msamiati unaofaa.

1. kushangiliwa

2. mashabiki

3. furaha tele

4. kipindi cha kwanza

5. kupasiana mpira

6. kuandika goli

## 6.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

### Zoezi la 7:(ukurasa wa 64)

**Mwalimu aombe** wanafunzi kufanya makundi ya wanafunzi watatu watatu, wajadili kuhusu "Umuhimu wa Michezo" akitilia mkazo kwenye jinsi michezo inavyogeuza maisha ya binadamu.Mwalimu awakumbushe kutumia majina ya ngeli ya Li-Ya-. Kisha wanafunzi wawasilishe mawazo yao mbele ya wenzao.

## 6.4.6. Kuandika

### Zoezi la 8:(ukurasa wa 64)

Zoezi hili liwe la kibinafsi. Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi watunge kifungu kifupi kuhusu" Timu mbili"kwa kuzingatia matumizi ya alama za uakifishaji.

## 6.5. Muhtasari wa Mada

Mada hii ya pili **"Msamiati katika Mazingira ya Michezo"** ina vipengele vitatu yaani masomo makuu matatu yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo vidogo kama vile: mchoro, kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, matumizi ya lugha, kusoma na kuandika, sarufi na maelezo muhimu. **Somo la kwanza** linaeleza msamiati unaohusiana na michezo. **Somo la pili** linaeleza faida za michezo. **Somo la tatu** linaeleza mashindano katika michezo.

## 6.6. Maelezo ya Ziada

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mwalimu. Sehemu hii inamsaidia mwalimu kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada.

## 6.7.Tathmini ya Mada ya Pili

Mwalimu atatathimini majibu yanayotolewa na wanafunzi kulingana na maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha mwanafunzi

I.

a) maadili

b) daraja

c) mashindano

d) chenga

II. Faida zinazijitokeza katika michezo kwa kulinganisha mchezo wa kandanda na mchezo wa kikapu ni kama :-Kuimarisha mwili, kutajirisha wachezaji , kuburudisha wachezaji watazamaji wanaoshirikia mchezo.

III. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutunga kifungu cha habari kuhusu michezo wakitumia maneno yafuatayo ambayo hutumiwa katika uwanja wa michezo. ahakikisha pia kwamba

wametumia maneno walau manne ya ngeli ya li-ya kwa kupiga mstari chini yake.

- Kuvisha kanzu - Kutoa bomba
- Mpira kuwa mwingi - Kukokota ngoma
- Kukata mbuga - Mpira kuambaamba nje
- Kuunawa mpira - Kuotea
- Harusi - Kuunyaka mpira

- Refa - Washika vibendera

## 6.8. Mazoezi ya Ziada

### 6.8.1. Mazoezi ya Urekebishaji

Taja majina ya watu wafuatao katika kikundi

a. Anayecheza michezo. (**Mchezaji**)

b. Anayedaka mpira golini. (**Mlindamlango**)

c. Anayepuliza filimbi uwanjani. (**Refa**)

d. Wachezaji wa kundi moja. (**Timu**)

1. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia majina ya ngeli ya li-ya- yanayofaa.

### 6.8.2. Mazoezi jumuishi

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia majina ya ngeli ya li-ya- yanayofaa.

a. Jana, timu ya Rayon Sport FC iliifunga Bugesera FC............................matatu kwa bila. (**mabao**)

b. Wanyarwanda wengi wanaipenda sana nyama iliyokaangwa kwa kutumia..................................................ya Mukwano. (**Mafuta**)

c. Kipofu ni mtu ambaye hawezi kutumia ...............................yake mawili, yaani asiyeona kutokana na kuugua, ajali au kuzaliwa hivyo. (**Macho**)

### 6.8.3. Mazoezi nyongeza

Orodhesha maneno sita yanayohusiana na michezo

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | J | E | Z | I | M | G | O | L | I |
| W | R | R | V | R | E | F | A | P | Y |
| A | T | T | P | P | C | Z | M | M | T |
| N | Y | Y | Y | Y | H | D | A | K | A |
| J | J | J | M | P | I | R | A | W | W |
| A | G | O | L | I | K | I | P | A | N |

**Jibu**

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | J | E | Z | I | M | G | O | L | I |
| W | R | R | V | R | E | F | A | P | Y |
| A | T | T | P | P | C | Z | M | M | T |
| N | Y | Y | Y | Y | H | D | A | K | A |
| J | J | J | M | P | I | R | A | W | W |
| A | G | O | L | I | K | I | P | A | N |

# MAADA KUU YA 3: UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI KATIKA KISWAHILI

3

## MADA NDOGO: MUHTASARI, FANI NA MAUDHUI

Uwezo Upatikanao katika Mada: Kuelewa na kufuata mtindo wa kuandika muhtasari wa hadithi aliyoisikiliza au kuisoma; kuchambua hadithi za Kiswahili kwa kuzingatia fani na maudhui yanayojitokeza katika hadithi; kusimulia hadithi rahisi za masimulizi; kujua mabadiliko ya kisarufi katika matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU-

Ujuzi wa Awali

Kupitia masomo waliyofundishwa katika lugha nyingine (Kinyarwanda, Kiingereza na fasihi ya Kiingereza) wanafunzi hawa wana ujuzi wa jumla kuhusu sifa za muhtasari mzuri na mambo muhimu ya kuzingatiwa tunapoitolea insha fani na maudhui.

### Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada

Katika masomo ya mada hii vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha, mazoezi ya kuandika, kuzungumza, na katika mazoezi au kazi za sarufi; mwalimu atawaongoza wanafunzi katika ujifunzaji na kushughulikia masuala mtambuka yafuatayo:

### 1. Mafunzo kuhusu Amani na Maadili

Kwa kupitia njia ya vifungu vya hadithi simulizi vilivyoandaliwa katika mada hii, mwanafunzi atasaidiwa kujenga uhusiano mwema na wengine. Mwalimu atatumia kila fursa akitumia vifungu vyenyewe, maswali ya ufahamu na mazoezi ya kisarufi, kushughulikia suala mtambuka la amani na maadili.

Maadili yanayojitokeza katika vifungu hivyo ni kama: kutowanyanyasa wale wasio na nguvu za kimwili kama sisi, kutowachukia walio na vipaji tusivyokuwa navyo, na kutulia kila mara tunapopata shida/tatizo linalozidi uwezo wetu wa kulitatua.

### 2. Elimu Jumuishi:

makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu kama vile: wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu/ulemavu wa mwili, wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza, na kadhalika.

Kumbuka kuwa wanafunzi wenye matatizo kama haya ni kama wengine; walikuja shuleni ili wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima wewe mwalimu uwasaidie ipasavyo.

### 3. Mazingira na Maendeleo endelevu

Mwalimu kupitia mazoezi ya msamiati na sarufi, anaweza kueleza umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa maisha ya watu.

### 5. Usawa wa Jinsia

- - Mwalimu katika mifano yote, ni lazima kutoa mifano inayoonesha usawa wa jinsia;
- - Katika mazoezi ya kutunga sentensi, ni vizuri kutunga sentensi ambazo zinaeleza na zinatoa maelezo kuhusu usawa wa jinsia;
- - Kazi katika makundi, ni vizuri kupanga wasichana na wavulana katika kundi moja ili darasani pasiwe na kundi la jinsia moja.
- Mwongozo kuhusu Zoezi la Utangulizi wa Mada
- - Kwa kutangulia mada, mwalimu atauliza maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua kuhusu mada hii.
- - Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia masomo tofauti, mazoezi, vifungu, na kazi nyingine zilizotayarishwa kwenye mada hii.

## Orodha ya Masomo na Tathmini

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (kutoka muhtasari: maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| 1. Muhtasari katika Fasihi Simulizi | Maarifa na ufahamu: kukumbuka mwongozo wa kufuata katika utoaji wa muhtasari wa hadithi.<br><br>Stadi: kuandika muhtasari wa hadithi aliyoisoma au kuisikiliza.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kuendeleza ujuzi katika kufanya muhtasari. | 11 |
| 2. Fani katika hadithi simulizi | Maarifa na ufahamu: kuorodhesha mambo muhimu yanayojitokeza katika uchambuzi wa fani.<br><br>Stadi: kutoa mambo muhimu yanayojitokeza katika fani ya hadithi aliyochambua.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kufurahia utanzu wa hadithi na kujisikia hamu ya kuiga mazuri katika kazi za sanaa au fasihi. | 12 |

| | | |
|---|---|---|
| 3. Maudhui katika hadithi simulizi | Maarifa na ufahamu: kuorodhesha mambo muhimu yanayojitokeza katika uchambuzi wa maudhui.<br><br>Stadi: kutoa mambo muhimu yanayojitokeza katika fani ya hadithi aliyochambua.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: tabia ya kuzingatia maelekezo na maagizo yatolewayo katika hadithi simulizi. | 11 |
| Tathmini ya Mada | | 2 |
| Vipindi vya mada zote | | 36 |

## SOMO LA 7: MUHTASARI

### 7.1. Ujuzi wa Awali

Somo lililopita lilijishughulisha na mashindano, yaani mapambano baina ya pande mbili au zaidi katika michezo. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Maswali haya yatakuwa na uhusiano wa karibu na michezo.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu msamiati wa michezo kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo:

- Unaona nini kwenye mchoro?
- Ni faida gani tunazozipata tunapocheza?

### 7.2. Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Ubao,
- Chaki,
- Vuvuzela,
- Vifaa kama mpira wa kucheza kandanda, mpira wa kikapu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

Tanbihi: Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 7.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo mambo yafuatayo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/ mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).
- **Maswali na majibu:** mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mwalimu:** mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.
- **Majadiliano:** mbinu hii itawapa wanafunzi uwezo wa kujadiliana kuhusu kazi watakayopangiwa na mwalimu.
- **Utafiti:** mbinu hii itawaruhusu wanafunzi kutafuta maelezo zaidi kuhusu kazi watakazopangiwa na mwalimu. Wataweza kutafuta habari mbalimbali katika vitabu vya

maktabani au kwa kutumia tovuti. Wataweza tena kujadiliana na watu wengine wa nje ya darasa lao.

## 7.4 MAJIBU

**Zoezi la 1:**(ukurasa wa 69)

Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, watazame michoro kwenye ukurasa husika kisha watatoa maoni yao kuhusu wanachokiona kwenye mchoro pamoja na kueleza kinachozungumziwa kwenye mchoro. Baadaye, wachangie wanayoyaona na makundi mengine. Mwalimu awaelekeze kuhusu hadithi simulizi kutokana na majibu wanayoyatoa.

### 7.4.1. Maswali ya Ufahamu

1. Hadithi hii ina wahusika watatu: Tulia, Mfalme na Mwendawazimu

2. Tulia alikuwa anajishughulisha na kazi ya uhunzi.

3. Mfalme alipomwita Tulia alimuamrisha kumtengenezea mtu mwenye uhai aliye na uwezo wa kuzungumza na kutembea.

4. Hapana. Tulia hakukubali kutekeleza amri ya Mfalme. Alijibu kwa sauti ya kutetemeka na kusema, "Sultan mheshimiwa, ingawa nina maarifa mengi katika kazi yangu, siwezi kamwe kutengeneza mtu aliye na uhai."

5. Tulia alijihisi vibaya alipofika nyumbani kutoka kwa Mfalme. Alishikwa na kizunguzungu akaamua kukaa chini, aliweka kichwa chake katikati ya miguu yake na machozi yakatiririka kama mvua kwenye mashavu yake.

6. Tulia alipokuwa katika hali mbaya nyumbani kwake, mwendawazimu alimtembelea.

7. Tulia ali posema "Nimekwisha kufa mie ingawa sijaingia kaburini", alikuwa anamaanisha kuwa alipewa kazi ambayo hawezi kufanya na akishindwa kazi hiyo ahukumiwe kifo.

8. Mwendawazimu alimshauri Tulia aende kwa Mfalme akamwambie atoe mitungi mia moja ya machozi ya watu na magunia mia moja ya jivu la nywele za watu na amwelezee kwamba hivyo ndivyo vinavyotumiwa kwa kutengeneza mtu.

9. Ndiyo, Tulia alifuata mawaidha ya Mwendawazimu.

10. Ndiyo, tatizo lililokuwa kati ya Tulia na Mfalme lilitatuliwa kwa sababu Mfalme alishindwa kutoa rasilimali za kumtengeneza mtu. Na kwa hiyo, hangeweza kumuua Tulia.

### 7.4.2. Msamiati kuhusu Kifungu

**Zoezi la 2:**(ukurasa wa 71)

Mwalimu atawaomba wanafunzi kueleza kila neno na kulitumia katika sentensi. Mwalimu atasahihisha makosa ya kimaandishi.

1. mhunzi: mtu anayefanya kazi ya kufua vitu vya madini ya chuma au bati.

2. kutia fora: fanya kuwa na hamu ya kufanya jambo bora zaidi.

3. mfalme: mtawala wa kiume wa asili ya urithi.

4. maskani: makazi.

5. kuamini: kubali ya kuwa jambo fulani ni la kweli.

6. sultani: mtu aliye na cheo kikuu katika utawala wa kifalme hususan Uarabuni.

7. kutetemeka: kuchezesha mwili kwa hofu.

8. kichaa: mwendawazimu.

9. kuwasili:kufika mahali ulipoazimia kwenda baada ya mwendo au safari.

10. hasira: chuki/kinyongo.

11. kizunguzungu: hali ya kujisikia kichwa kinazunguka.

12. mtungi: chombo kilichotengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi, chenye mdomo mdogo na tumbo kubwa, hutumika kwa kubebea au kuhifadhia maji.

13. jivu: ni vumbi la kitu kilichoteketezwa kwa moto.

14. kuabudu: kuomba kwa unyenyekevu mkubwa, hasa kwa Mungu.

15. sala: maombi kwa Mwenyezi Mungu.

Baada ya kutoa maelezo ya maneno hapo juu, mwalimu atawaomba mmoja mmoja kuyatumia katika sentensi zenye maana. Wanafunzi wataandika sentensi zao kwenye ubao ili mwalimu asahihishe kunapokuwa makosa ya kimsamiati. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kutunga sentensi zifuatazo:

- Kaka yangu alichagua kuwa mhunzi alipoulizwa kazi atakayoifanya baada ya masomo ya muda mfupi.
- Hapo zamani, Rwanda ilikuwa inaongozwa na mfalme.
- Mtoto alipoumwa na mbu alianza kutetemeka kama dalili ya ugonjwa wa malaria.
- Wanafunzi walipowasili walitayarishiwa mahali pa kufanyia mazoezi, walitoa sala kwa Mwenyezi Mungu.

**Zoezi la 3:**(ukurasa wa 72)

Zoezi hili ni la binafsi, mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi kwa makini. Mwanafunzi ahusishe maneno na maana zake kwa kutumia mshale. Mwalimu asahihishe kila mwanafunzi na kuwasaidia.

1. C

2. F

3. A

4. G

5. B

6. E

7. D

### 7.4.3. Sarufi: Majina ya ngeli ya Pa-

**Zoezi la 4:**(ukurasa 72)

Mwalimu awalekeze wanafunzi kufanya zoezi kibinafsi. Atasahihisha zoezi kwa kila mwanafunzi na kusahihisha makosa yatakayojitokeza.

Maneno ambayo yameandikwa kwa rangi iliyokoza yanapatikana katika ngeli ya majina ya Pa-.

**Zoezi la 5:** (ukurasa wa 75)

Zoezi hili lifanywe binafsi. Wanafunzi wawasilishe kazi mwanafunzi mmoja baada ya mwingine. Mwalimu awaelekeze kwa majibu sahihi.

1. Mahali pake panapendeza.

2. Nimetembea pahali pabaya pasipo na mazingira bora.

3. Ziwani Kivu kuna pahali pengi pa kutembelea.

4. Nilimkuta katika baa, mahali pabaya sana.

5. Mukamana hapendi kukaa pahali pachafu.

6. Waislamu wana pahali pao pa kusalia.

**Zoezi la 6:** (ukurasa wa 75)

Mwalimu aombe wanafunzi kufanya kazi hii binafsi. Mwalimu arekebishe makossa ya kimaandishi na kimazungumzo.

1.pazuri

2.safi

3. pabaya

4. pachafu

5. patakatifu

6. pakavu

7. pamoja

8. penye

### 7.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 7:** (ukurasa wa 75)

Mwalimu awaagize wanafunzi kufanya kazi binafsi. Mwalimu amwombe mwanafunzi kusoma kifungu cha habari "Mhunzi Tulia" kisha afanye muhtasari wa kifungu cha habari kimaandishi na baadaye asimulie hadithi mbele ya darasa. Mwalimu arekebishe makosa ya kimaandishi na kimasimulizi yaliyojitokeza. Na baadaye mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi ndani ya kundi moja ana mtazamo mmoja kuhusu hatua za kufanya muhtasari wa hadithi. Mwisho mwalimu anawapa wanafunzi muda wa kutosha wa kuigiza mitazamo hiyo mbele ya darasa.

**Zoezi la 8:** (ukurasa wa 76)

Wanafunzi wajibu maswali katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha watoe maelezo kamili. Mwalimu awaelekeze kwa kuwasilisha mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi na kimaandishi.

1. Muhtasari ni ustadi au ufundi wa kuisoma habari, kuielewa vizuri na kuweza kuieleza au kuiandika upya kwa ufupi au kwa maneno machache ukiyalinganisha na yale ya awali lakini bila kupotosha ujumbe wa habari ya kwanza. Kwa maneno mengine muhtasari ni ufupisho wa maelezo.

2. Muhtasari mzuri unapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

- Muhtasari unapaswa kuwa na mawazo makuu yanayoeleweka.

- Muhtasari mzuri unapaswa kuwa theluthi moja ya kazi yote.

- Lugha inayotumiwa ni lazima iwe lugha ya mkato (matumizi ya nahau na methali).

- Muhtasari unaweza kuwa katika aya moja au nyingi.

- Muhtasari mzuri unapaswa kumwezesha msikilizaji au msomaji kupanua msamiati.

- Muhtasari mzuri lazima uwe bunifu (yaani matumizi ya maneno yako mwenyewe).

Mwalimu achunguze majibu ya wanafunzi namna walivyotumia msamiati na awasaidie kunapohitajika.

### 7.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 9:**(ukurasa wa 77)

Mwalimu awaambie wajadiliane katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na majadiliano yao wayawasilishe mbele ya darasa.Mwalimu asahihishe makosa ya kimaandishi na kimatamshi. Mwalimu awaelezee kwamba kichwa cha habari kinazungumzia mhunzi na yanayozungumziwa yanajikita zaidi kwenye kazi ya uhunzi aliyoifanya Tulia.

### 7.4.6. Kuandika

**Zoezi la 10:**(ukurasa wa 77)

Wanafunzi wasome hadithi "Mhunzi Tulia" kisha watunge kifungu cha habari kwa kutoa hoja na maelezo kamili kwa kutumia majina ya ngeli ya pa-. Baada ya kuandika wanafunzi wawasilishe muhtasari wao mbele ya darasa. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo na kuwapa msaada maalumu. Mwalimu awatie motisha wanafunzi.

# SOMO LA 8: FANI KATIKA HADITHI SIMULIZI

## 8.1. Ujuzi wa Awali

Mada hii inajishughulisha na fani katika hadithi simulizi. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Maswali haya yatakuwa na uhusiano wa karibu na fasihi.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu mambo yanayohusiana na fasihi kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro.

## 8.2. Vifaa vya Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Ubao,
- Chaki,
- Chati na jedwali,
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji ujifunzaji na uangalifu maalumu.

Tanbihi: Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 8.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo mambo yafuatayo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi

yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/ mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).
- **Maswali na majibu:** mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mwalimu:** mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.
- **Majadiliano:** mbinu hii itawapa wanafunzi uwezo wa kujadiliana kuhusu kazi watakayopangiwa na mwalimu.
- **Utafiti:** mbinu hii itawaruhusu wanafunzi kutafuta maelezo zaidi kuhusu kazi watakazopangiwa na mwalimu. Wataweza kutafuta habari mbalimbali katika vitabu vya maktabani au kwa kutumia tovuti. Wataweza tena kujadiliana na watu wengine wa nje ya darasa lao.

### 8.3.1. Kusoma na ufahamu:Kifungu kuhusu Hadithi Simulizi

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha habari kilichopo huku wakiandika msamiati mpya wanao upata kutoka kifungu. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu, awaombe kusoma kwa sauti. Mwalimu akumbuke umuhimu wa kusahihisha matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Hatimaye, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha habari walichokisoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa.

### 8.3.2. Ujifunzaji wa Msamiati kuhusu Kifungu

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujibu maswali ya ufahamu, mwalimu awasaidie kuelewa kila swali na baadaye kutoa majibu kwa wanafunzi. Mwalimu baada ya kusahihisha maswali ya ufahamu, anaongoza kazi ya kutafuta maana ya msamiati. Wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wanatumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu kutafuta maana ya msamiati. Swali lingine ni kuchaguwa kwenye msamiati neno sahihi kati kwa kukamilisha sentensi. Kwa hivyo, mwalimu azunguke katika makundi yote.

### 8.3.3. Sarufi

Kwa kufundisha somo la sarufi, mwalimu atawaomba wanafunzi kuandika sentensi kutoka kifungu cha habari zenye majina ya ngeli ya M- na kujadiliana maana zake. Kwa kuendelea kutoa maelezo, mwalimu atawaomba kutunga sentensi tano na kukamilisha sentensi.

### 8.3.4. Matumizi ya Lugha

Mwalimu awaombe wanafunzi wajipange katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili kujadiliana kuhusu mashindano waliyowahi kuhudhuria. Wanafunzi waelezane mashindano mbalimbali yaliyotokea mahali fulani. Baadaye, kila kundi lieleze waliyozungumzia. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Kutokana na majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaombe wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno yanayotumiwa katika mashindano kama fainali, nusu fainali, penalti, .....

### 8.3.5. Kusikiliza na Kuzungumza

Hapa mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ambapo atawaomba kusoma mmoja baada ya mwingine. Hapa mwalimu atachunguza mambo muhimu yafuatayo: matumizi ya lugha kwa ufasaha; matumizi ya msamiati na sentensi zenye maana. Ni vyema mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi mara tu yanapojitokeza ili kuwazoeza wanafunzi kutamka kwa usahihi herufi, silabi, maneno na sentensi za Kiswahili.

### 8.3.6. Kuandika

Mwalimu atawaongoza wanafunzi kuandika majina ya ngeli ya M-. Hapa mwalimu atachunguza kama mwanafunzi anaandika sentensi sahihi kwa kutumia majina ya ngeli husika, matumizi ya sarufi kwa ufasaha, na kadhalika.

## 8.4 MAJIBU

**Zoezi la 1:** (ukurasa wa 78)

Mwalimu awaweke katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha awaombe wanafunzi kueleza wanachokiona kwenye mchoro na kujadiliana kati yao.

### 8.4.1. Maswali ya Ufahamu

1. Wahusika wanaozungumziwa katika hadithi hii ni Kobe, Nyani na mkewe Kobe.

2. Nyani alimdanganya Kobe akisema kuwa shoka lake lilikuwa linarudisha nyuma juhudi yake kwa kuwa lilikuwa butu, huku akitaka Kobe amwazime lake.

3. Hapana, shoka la Nyani halikuwa butu. Huo ulikuwa ujanja tu, ili apewe shoka la Kobe.

4. Hapana. Nyani hakumrudishia Kobe shoka lake.

5. Kobe alipofika nyumbani kwa Nyani alipokelewa vizuri, kwa kupewa chakula na kinywaji.

6. Akisaidiwa na mkewe, Kobe alijigeuza kuwa kitoweo ambacho kililiwa na Nyani. Alipofika tumboni mwa Nyani alimletea maumivu huku akimwambia ampatiee shoka lake.

7. Nyani alimdanganya Mzee Kobe akisema kuwa alimwazima mjomba wake shoka lile naye akamuarifu kuwa mwizi aliivamia nyumba yake akaliiba.

8. Nyani alipeleka shoka la Mzee Kobe mahali alipochukulia kitoweo na Kobe akaenda na shoka lake.

9. Tabia ya Nyani haikubaliki katika jamii. Uhusiano wa kudumu na wenzetu hujengeka tunapowatendea mema, kinyume na kuwachezea shere.

10. "Akili ni nywele, kila mtu ana zake". Nyani alijifikiri mwenye akili nyingi kuliko Kobe, kumbe alikuwa anajidanganya mwenyewe. Si vizuri kuwachezea shere wenzetu, kwa sababu tukiendelea na tabia hiyo mbaya, sisi wenyewe tutajifunza somo gumu.

11. Ukataji wa miti una athari kubwa katika mazingira. Hii ni kwa kuwa unachangia katika uharibifu wa mazingira. Uharibifu wa mazingira unapokuwepo husababisha hata kutokea kwa ukame, joto kuongezeka, na kuwepo kwa upungufu wa hewa ya oksijeni. Mvua ainapokosekana pia huwa kunatokea baa la njaa. Njaa pia inaweza kusababisha hata vifo kwa binadamu na wanyama.

12. Kulipa kisasi ni jambo lisilokubalika. Badala ya kulipa kisasi Mzee Kobe angepaswa kwenda kumshitaki Nyani katika vyombo vya sheria. Kulipa kisasi kunaweza kusababisha uhasama wa kudumu baina ya pande mbili. Hivyo ni muhimu kuepukana na visasi.

### 8.4.2. Msamiati Kuhusu Kifungu

**Zoezi la 2:** (ukurasa wa 81)

Kazi hii ifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi watatu watatu. Watumie kamusi kwa kueleza maana ya msamiati mpya, na kuutumia katika sentensi. Mwalimu achunguze kazi zinazofanywa na wanafunzi na kuwaomba wafanye mawasilisho. Mwalimu arekebishe makosa yanayoweza kujitokeza.

1. kujikokota: kujaribu kutenda jambo polepole kwa ulegevu tena pasipo nguvu za kutosha.

2. shoka butu: shoka lisilokwa na makali.

3. kulalamika: kueleza kutoridhika na jambo fulani.

4. kukaa kitako: kukaa chini.

5. -epesi: -sio ngumu.

6. njama: maafikiano au mapatano ya kufanya jambo baya dhidi ya mtu au watu wengine.

7. mvivu: mtu asiyependa kufanya kazi.

8. dalili: alama ya kuonyesha hali au kitendo fulani kitakachofanyika.

9. kutoa kauli: kutamka/kusema.

10. kitoweo: kitu kama vile mchuzi, mboga, samaki au nyama kinachotumiwa kwa kulia chakula.

11. madhara: kitu chenye kuleta uharibifu au athari mbaya.

12. kusikitika: kuwa na hali ya huzuni kwa ajili ya jambo baya lililotendeka au kwa sababu ya hali fulani iliyoko.

**Zoezi la 3:** (ukurasa wa 81)

Zoezi hili lifanywe na kila mwanafunzi binafsi. Mwalimu awaombe wanafunzi kuchagua maana ya maneno kutoka kisanduku. Mwalimu arekebishe makosa.

1. c.

2. a

3. f

4. b

5. g

6. e

7. d

### 8.4.3. Sarufi: Matumizi ya Majina ya Ngeli ya M-\

**Zoezi la 4:**(ukurasa wa 82)

Kazi hii ni ya kipeke. Wanafunzi waeleze majibu yao na wayawasilishe mbele ya darasa. Mwalimu awasaidie wanafunzi ipaswavyo.

Maneno yanayopigiwa kistari ni vivumishi vya kuonyesha vimeambatana na nomino za ngeli ya M-.

**Zoezi la 5:** (ukurasa wa 84)

Mwalimu awaelekeze wanafunzi na kuwasaidia ipaswavyo. Kazi ifanywe na kila mwanafunzi binafsi na baadaye aeleze jibu lake mbele ya darasa.

1. mwetu
2. pazuri
3. humu
4. ambamo
5. mle
6. humu
7. ambamo
8. mupi

### 8.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 6:**(ukurasa wa 85)

Kazi hii ni ya makundi. Mwalimu aunde kundi la wanafunzi watatu watatu kisha wawasilishe majibu yao mbele ya darasa. Mwalimu awaongoze kufanya mawasilisho.

1. Wahusika katika hadithi hii ni wanyama.

2. - Nyani: ni mwivu, mjanja, mchoyo na mlafi.

   - Kobe: mpenda kazi, msaidizi, mvumilivu na mwenye akili.

   - Mkewe Kobe: mtiifu.

3. - Wakati hadithi hii ilipotokea haujulikani. Ni hadithi simulizi na ya kubuni.

   - Ilitokea katika kijiji kimoja.

Tanbihi: Wakati na mahali katika hadithi hii ni pa kubuni.

**Zoezi la 7:**(ukurasa wa 88)

Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwanafunzi aelekezwe jinsi ya kufanya zoezi hili kwa kutumia mshale na kuhusisha maneno na maana zake. Mwalimu asahihishe zoezi na kuwarekebisha wanafunzi.

1. D. Kazi kupamba moto: Kuendelea kwa kutumia nguvu nyingi zaidi.
2. E. Kujikokota na shoka: Kata miti pole pole.
3. A. Kukaa kitako: Kuketi
4. B. Kulegeza makoo: Kunywa
5. F. Kupiga mbeu ya shibe: Kutosheka na chakula baada ya kukila.
6. C. Kuchezea mtu shere: Kumfanyia mzaha.

### 8.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 8:**(ukurasa wa 88)

Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha awaambie wajadili kuhusu mawazo makuu yanayojitokeza katika hadithi "Kobe na Nyani". Baadaye wawasilishe mawazo waliyoyaorodhesha mbele ya wenzio darasani.

### 8.4.6. Kuandika

**Zoezi la9:** (ukurasa wa 88)

Mwalimu awaombe wanafunzi kutunga kifungu cha habari kuhusu hadithi simulizi moja ya Kinyarwanda wanayoijua. Wakitumia majina ya ngeli ya m-. Mwalimu awaongoze na awasaidie kunapohitajika.

# SOMO LA 9:MAUDHUI KATIKA HADITHI SIMULIZI

## 9.1. Ujuzi wa Awali

Mada hii inajishughulisha na maudhui katika hadithi simulizi. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Maswali haya yatakuwa na uhusiano wa karibu na fasihi.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu mambo yanayohusiana na fasihi kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro.

## 9.2. Vifaa vya Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Ubao,
- Chaki,
- Chati na jedwali,
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kawasaidia wanafunzi wanaohitaji ujifunzaji na uangalifu maalumu.

**Tanbihi:** Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 9.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili, mwalimu atatilia mkazo mambo yafuatayo:

**Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.

**Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/ mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).

**Maswali na majibu**: mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.

**Maelezo ya mwalimu**: mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

**Majadiliano**: mbinu hii itawapa wanafunzi uwezo wa kujadiliana kuhusu kazi watakayopangiwa na mwalimu.

**Utafiti**: mbinu hii itawaruhusu wanafunzi kutafuta maelezo zaidi kuhusu kazi watakazopangiwa na mwalimu. Wataweza kutafuta habari mbalimbali katika vitabu vya maktabani au kwa kutumia tovuti. Wataweza tena kujadiliana na watu wengine wa nje ya darasa lao.

### 9.3.1. Kusoma na ufahamu hadithi

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha habari kinachohusu fasihi simulizi "**Wafalme Wawili**" huku wakiandika msamiati mpya wanaoupata kutoka kifungu. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu, awaombe kusoma kwa sauti. Mwalimu akumbuke umuhimu wa kusahihisha matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Hatimaye, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha habari walichokisoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa.

### 9.3.2. Ujifunzaji wa Msamiati kuhusu Hadithi

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujibu maswali ya ufahamu, mwalimu awasaidie kuelewa kila swali na baadaye kutoa majibu kwa wanafunzi. Mwalimu baada ya kusahihisha maswali ya ufahamu, anaongoza

kazi ya kutafuta maana ya msamiati. Wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wanatumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu kutafuta maana ya msamiati. Swali jingine ni kuchaguwa kwenye msamiati neno sahihi kwa kukamilisha sentensi. Kwa hivyo, mwalimu azunguke katika makundi yote.

### 9.3.3. Sarufi

Kwa kufundisha somo la sarufi, mwalimu atawaomba wanafunzi kuandika sentensi kutoka kifungu cha habari zenye majina ya ngeli ya Ku- (ukurasa75) na kujadiliana maana zake. Kwa kuendelea kutoa maelezo, mwalimu atawaomba kutunga sentensi tano na kukamilisha sentensi.

### 9.3.4. Matumizi ya Lugha

Mwalimu awaombe wanafunzi wajipange katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili kujadiliana kuhusu mawazo muhimu yanayozungumziwa kwenye hadithi. Baadaye, kila kundi lieleze waliyozungumzia. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Kutokana na majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaombe wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia nahau na misemo tofauti iliyotumiwa katika hadithi.

### 9.3.5. Kusikiliza na Kuzungumza

Hapa mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ambapo atawaomba kusoma mmoja baada ya mwingine. Hapa mwalimu atachunguza mambo muhimu yafuatayo: matumizi ya lugha kwa ufasaha; matumizi ya msamiati na sentensi zenye maana. Ni vyema mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi mara tu yanapojitokeza ili kuwazoeza wanafunzi kutamka kwa usahihi herufi, silabi, maneno na sentensi za Kiswahili.

### 9.3.6. Kuandika

Mwalimu atawaongoza wanafunzi kuandika sentensi kwa kutumia majina ya ngeli ya ku-kisha wayajadili. Hapa mwalimu atachunguza kama mwanafunzi anaandika sentensi sahihi, matumizi ya sarufi kwa ufasaha, na kadhalika.

## 9.4 MAJIBU

**Zoezi la 1:** (ukurasa wa 89)

Wanafunzi wazungumzie mchoro husika hapo wakijadiliana wanachokiona kwenye mchoro.

### 9.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Ni kwa sababu kuwa wanyama hao hawakuwa na mfalme, na walipotazama kwenye misitu mingine, waliona kwamba wanyama wengine wana wafalme, wakafikiri kwamba wanyama hao wana maisha bora kuliko wao kisha wakajichagulia mfalme.

2. Wanyama waliohudhuria mkutano wa kuchagua mfalme ni: Nguruwe, Simba,Tembo, Chui, Twiga, Ngiri, Sungura, Nguchiro, Fisi, Nyoka, Mbogo, ndege wote na samaki.

3. Alipewa fursa ya kuelezea wanyama wengine sababu yeye ndiye anapaswa kuchaguliwa kuwa mfalme, huku akijaribu kufahamisha kwamba yeye ana tabia nzuri nyingi zaidi kushinda wanyama wengine

4. Alisema maneno yaliyopendwa na wanyama wengine, akisema kuwa akichaguliwa kuwa mfalme wao, atalinda usalama wao, mabibi zao na watoto wao. Hakutakuwa na mnyama kutoka misitu mingine atakayewashambulia. Hata binadamu hataingia hapo tena.

5. Aliwaambia kuwa kazi ya kulinda usalama wao ni kazi ngumu sana na inamlazimisha kula chakula kizuri kila siku. Akawaambia "Mimi sitaendelea kula nyasi kuanzia leo. Hiyo inamaanisha kwamba kila siku ninahitaji wanyama watakaoniletea chakula ili nile vizuri!"

6. Wanyama wote hawakufurahia utawala wa mfalme Tembo aliyekuwa anawavunjia matumaini kwa sababu ya ukatili na ubinafsi wake.

7.Tembo alimchukia sana Sungura kwa kuwa yeye hakumpikia chakula na anataka afe na njaa.

8.Mfalme Tembo aliposema "Nitamfundisha somo moja ambalo hatasahau maishani mwake" alimaanisha kwamba atampa adhabu kali sana, ambayo haiwezi kusahaulika .

9. i) Kilikuwa kivuli chake lakini yeye hakujua.

ii) Alijitupa chubwi ndani ya maji kupigana na "mfalme" ambaye hakuwepo. Na baadaye wanyama walimwokoa kwa kumtoa majini akiwa na maumivu sana.

10. Mfalme Tembo alijutia juu ya ukatili na maovu aliyowatendea wanyama wenzake na aliomba msamaha wanyama wengine kwa matendo yake aliyowafanyia na kuwanyanyasa sana.

11. Aliyeteuliwa kuwa mfalme baada ya Mfalme Tembo, niSimba.Mtazamo wake katika uongozi ulikuwa kukomesha tabia zote mbaya na mienendo mingine

isiyofaa miongoni mwa wanajamii wote. Tena kuweka sheria za uheshimiano kati ya wanajamii wote.

12. - Kifungu hiki cha habari kinafundisha wanajamii kuwa si vizuri kuwatendea wengine matendo mabaya kutokana na kipawa ulicho nacho kwa sababu ubaya unaweza ukakurudilia na tuombe msamaha juu ya maovu na matendo mabaya tunayowatendea wenzetu.

- Tujizoeze kutatua matatizo yetu ya kila siku kabla hatujachelewa, na tusifikiri mtu mwingine ndiye atakayetatua matatizo yetu.

- Tusiharakishe kumwamini yeyote kwa msingi wa maneno aliyosema tu. Tutazame vitendo

kwanza. Vitendo vizuri ni muhimu kuliko maneno tu.

### 9.4.2. Msamiati kuhusu Wafalme Wawili

**Zoezi la 2:**(ukurasa wa 92)

1.mfalme: mtawala mwanamume aliyepata nguvu za utawala kwa njia ya urithi au uwezo fulani kama vile ushujaa.

2. uhuru: hali ya kutotawaliwa na mtu au nchi nyingine. Hali ya kufanya mambo bila ya kuingiliwa.

3. kushawishi: kufanya mtu akubaliane na wewe au jambo ulilonalo

4. tegeni masikio: sikilizeni kwa makini.

5. Litaathiri: kuwa na madhara kwa kila mmoja

**Zoezi la 3:** (ukurasa wa 92)

1. kutetemeka

2. mwendawazimu

3. ilipofika

4. akili

5. mtoni

6. haogopi

7. amemdharau

8. msituni

9. alimforea

10. raia

### 9.4.3. Sarufi: Matumizi ya Majina ya Ngeli ya Ku-

**Zoezi la 4:** (ukurasa wa 93)

1. huku: kivumishi cha kuonyesha.

   kule: kivumishi cha kuonyesha.

2. huku: kivumishi cha kuonyesha.

3. huko: kivumishi cha kuonyesha.

4. huku: kivumishi cha kuonyesha.

   kule: kivumishi cha kuonyesha.

**Zoezi la 5:** (ukurasa wa 93)

1. Sokoni kupi kunapatikana bidhaa vyenye bei nafuu?

2. Mahali kusafi kunafurahisha.

3. Darasani kwangu kunavutia.

4. Msituni hapa kuna Simba mkali.

5. Mguuni wapi pamezungumziwa kuwa na kidonda?

9.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 6:** (ukurasa wa 95)

Mwalimu aambie wanafunzi kusoma hadithi tena na kueleza sifa za wahusika wakuu waliozungumziwa katika hadithi. Kwa kutoa majibu kama haya:

-Wahusika wakuu hadithini humu ni:

1. -Tembo: Tembo alikuwa mfalme wa wanyama ambaye huwa na sifa ya udikteta na uanyanyasaji .Yeye tena hupenda chakula kizuri pamoja na kuheshimiwa.

   - Simba: Ni mnyama mwenye nguvu, hadithini yeye ana sifa nzuri ya kutetea haki za wanyama wote. Wanyama wote katika uongozi wa Mfalme simba wanalingana na wanaheshimiana.

   - Sungura: Alitumiwa kama mnyama mwenye akili, aliye na hamu ya kuwasaidia

wengine na kuokoa maisha yao katika uongozi mbaya wa Mfalme Tembo.

2. Mgogoro uliojitokeza baina ya mfalme Tembo na wanyama wengini ni kutokubaliana kwa wanyama na Mfalme Tembo juu ya uongozi wake wa udikteka na ukatilili ulionyanyasasa wanyama walioongozwa.

3.Mambo yaliyozungumziwa katika hadithi ni :

- Ukatili wa mfalme Tembo,

-Tabia njema ya sungura ya kuwakomboa wanyama wenzake,

- Tabia ya kuomba msamaha unapomkosea mwenzakonau wenzako,

-Uongozi mzuri na fikra nzuri za mfalme simba kwa kuletea usawa baina ya wanyama wote.

-Uongzi wa kidemokrasia (kujadiliana juu ya maswala yanayoweza kutatuliwa katika jamii kama vinavyoonekana kwa jamii ya wanyama wa msituni).

-Na kaddhalika,......

### 9.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 7:** (ukurasa wa 97)

Mwalimu ayaunde makundi ya wanafunzi kulingana na idadi yao pamoja na idadi ya kazi husika. Wanafunzi wasome hadithi "Wafalme Wawili" kisha wajadili ikiwa kichwa kinabeba ujumbe unaozungumziwa.Kila kundi liwasilishe kazi yao mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa ya kisarufi na kimatamshi.

Jikite zaidi kwenye maelezo haya: Kichwa "Wafalme wawili" kinasadifu yanayozungumziwa katika hadithi: kwanza kulikuwa na mfalme mmoja, Mfalme Tembo, aliyekuwa anafanya chochote atakacho, bila kutaniwa na yeyote. "Mfalme" wa pili (kivuli cha mfalme wa kwanza kilichokuwa ndani ya maji) ndiye aliyekuwa mtatuaji wa mgogoro uliokuwa kati ya Mfalme Tembo na wanyama wengine.

### 9.4.6. Kuandika

**Zoezi la8:** (ukurasa wa 97)

Kazi hii ifanyike katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kushirikiana na kutoa maoni tofauti yanayoyagusia masuala mtambuka husika. Mwalimu awaongoze kutumia mambo muhimu yanayotumiwa katika utungaji, yaani utangulizi, mwili na hitimisho. Baadaye wawasilishe kazi yao mbele ya darasa.

## 9.5. Muhtasari wa Mada

Mada hii ya tatu "**UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI KATIKA KISWAHILI**" ina vipengele vitatu yaani masomo makuu matatu yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo vidogo kama vile: mchoro, kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, matumizi ya lugha, kusoma na kuandika, sarufi na maelezo muhimu. Somo la **kwanza** linajihusisha na muhtasari katika fasihi simulizi. Somo la pili linaeleza fani katika hadithi simulizi. Somo la tatu linaeleza maudhui katika fasihi simulizi.

## 9.6.. Maelezo ya Ziada

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mwalimu. Sehemu hii inamsaidia mwalimu kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada.

## 9.7. Tathmini ya Mada ya Tatu

I.

1 Mamba alikuwa akijulikana kwa uzuri wa meno yake.

2 Uzuri wa Mamba ulipotea alipokuwa akitafuna mawe akidhani ni karanga na akapoteza meno yake.

3 Sungura alimdanganya mamba kuwa alimletea zawadi nzuri apendayo ambayo ni karanga zilizojaa mfukoni kumbe kulikuwa na mawe tele. Mamba alipozitafuna kwa pupa meno yake yakang'oka kwani Sungura alikuwa ameweka mfukoni mawe mengi na karanga chache sana.

4 Kichwa cha hadithi "WIVU HAUFAI", huhusiana sana na yanayosimuliwa katika hadithi sana sana pale Sungura alipoitwa kwa mfalme kuhukumiwa na kuadhibiwa kwa wivu wake juu ya Mamba. Tena Sungura alidhani kuwa ni wakati mzuri wa kuoa msichana aliyempenda sana lakini, msichana huyo alipopata habari juu ya uadui na ukatili wa Suungura alikasirika sana na kumchukia Sungura aliyemfanya Mamba ageuke kibogoyo. Hapohapo akakubali kuolewa na Mamba .

5 - Tabia nzuri ni muhimu kuliko sura nzuri. Mamba alikuwa na uzuri wa meno, lakini alikuwa na kasoro kubwa: ULAFI. Msichana mmoja angemuoa Mamba, angejutia ulafi wake. Mtu hupendwa zaidi kutokana na tabia yake nzuri kuliko sura yake nzuri. Mamba asingekuwa mlafi, asingepoteza meno yake.

Si vizuri kumchukia yeyote kwa sababu ana kipaji tusicho nacho. Sungura alifanya vibaya kumchukia Mamba na kumfanyia ukatili. Tusiwe na wivu wowote dhidi ya yeyote. Badala yake tujenge urafiki wa kudumu.

6 Mamba kuchukiwa na Sungura kulitokana na wivu wa Sungura. Mamba alikuwa na meno mazuri yaliyovutia wasichana wote. Miongoni mwa wasichana waliotaka

kuolewa na Mamba, alikuwa mmoja ambaye Sungura alikuwa anampenda sana na hali ya Mamba kuonekana mrembo kuliko yeye haikumpendeza Sungura.

7.-Baada ya kung'oka kwa meno yake ,Mamba alipatwa na maumivu kwa muda mrefu na ikawa shida kubwa kwake kula nyama ingawa ndicho chakula chake cha kawaida.

- Kutokana na kung'oka kwa meno ya Mamba tena aliwahi kutocheka akiwa katika mikutano ya wanyama wenzake kwa sababu ya kasoro aliyonayo akidhani kuwa atachekelewa.

II.

1. E

2. G

3. A

4. F

5. D

6. C

7. B

III.

Mifano:

Alipomwambia kuwa anamwambia kuhusu sifa yake ya uvivu alitia chumvi sana.

IV. Jaza sentensi hizi kwa kutumia maneno katika mabano:

1. hapa

2. huku

3. humu

4. pa

5. humu

6. pengi

# MADA KUU YA 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO

4

## MADA NDOGO: MIDAHALO NA MIJADALA

Uwezo Upatikanao katika Mada: Kuweza kuelewa mwongozo wa midahalo na mijadala na kushiriki katika kazi za majadiliano kwa kuzingatia mada zilizotolewa kujadiliwa; kujiandaa na mdahalo kwa kutafiti na kuandika hoja atakazotumia, kujua jinsi ya kutoa amri kwa vitenzi.

### Ujuzi wa Awali

Katika kidato cha tatu wanafunzi hawa walikuwa na mada izungumziayo "Midahalo na mijadala kuhusu shughuli za maendeleo na uzalishajimali dhidi ya umaskini nchini." Mada hii iliwajengea uwezo wa: kujadili na kujitetea hadharani kulingana na mada ya midahalo na mijadala inayotolewa kwa kujenga hoja ithibitishayo dai. Pia, wanafunzi wanaweza kutoa maoni yao binafsi kuzingatia na kutetea au kupinga hoja ya mwenzake kwa njia ya mazungumzo.

### Kuingizwa kwa Maswala Mtambuka katika Mada

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha, kuandika, kuzungumza na katika mazoezi au kazi na sarufi; mwalimu anawaongoza wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia maswala mtambuka yafuatayo:

### 1. Mafunzo kuhusu Amani na Maadili Mema

a. Katika mdahalo na mjadala, watu hutarajiwa kutokasirika ovyo na kusikiliza wengine wakitoa hoja zao. Mdahalo huwafundisha wahusika kusikilizana na kuelewana kama njia mojawapo ya kujenga amani imara.

b. Kwa kutunga sentensi, mwalimu awaongoze kutunga sentensi zenye mafunzo yanayohusu amani na maadili mema.

### 2. Mila,Desturi na Kuzalisha Bidhaa kwa kuzingatia kwa Viwango

Kwa kufanya kazi yoyote,  kama kuandika inafaa kuchunguza kama unafuata taratibu za kuandika.

### 3. Elimu Jumuishi

**Makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu kama vile**: wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu, wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza, na kadhalika.

Kumbuka kuwa wanafunzi wenye matatizo kama haya ni kama wengine; walikuja shuleni ili wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima wewe mwalimu uwasaidie ipasavyo.

## 4. Elimu kuhusu Jinsia

Katika vifungu au katika mifano ya sentensi, mwalimu kwa kutumia lugha anawasaidia wanafunzi kuelewa matumizi ya kondomu na sababu za kuitumia kama kujikinga ukimwi na kuzaa watoto ambao una uwezo wa kutimiza huduma zote kwao.

## 5. Mazingira na Maendeleo Endelevu

Mwalimu kupitia mazoezi ya msamiati na sarufi, anaweza kueleza umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa maisha ya watu.

## 6. Usawa wa Jinsia

a. Mwalimu katika mifano yote, ni lazima kutoa mifano inayoonesha usawa wa jinsia;

b. Katika mazoezi ya kutunga sentensi, ni vizuri kutunga sentensi ambazo zinaeleza na zinatoa maelezo kuhusu usawa wa jinsia;

c. Kazi katika makundi, ni vizuri kupanga wasichana na wavulana katika kundi moja ili darasani pasiwe na kundi la jinsia moja.

## Muongozo kuhusu Zoezi la Utangulizi wa Mada

- Kwa kutangulia mada, mwalimu atauliza maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua kuhusu mada hii;

- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia masomo tofauti, mazoezi, vifungu, na kazi nyingine zilizotayarishwa kwenye mada hii.

Orodha ya Masomo na Tathmini

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| 10. Maana ya mdahalo | Maarifa na ufahamu: kufafanua dhana ya mdahalo.<br><br>Stadi: kujiandaa awali kabla ya mdahalo kwa utafiti na kupangilia hoja za mdahalo.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kuonyesha moyo wa heshima wakati wa majadiliano. | 8 |
| 11. Maandalizi na utekelezaji wa mdahalo | Maarifa na ufahamu: kukumbuka taratibu za kufuata wakati wa kutoa hoja katika makundi.<br><br>Stadi: kutumia lugha sahihi na yenye kuvutia.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kutokata tamaa na kutokasirika ovyo. | 9 |
| 12. Maana ya mjadala | Maarifa na ufahamu: kuelezea mtiririko wa hoja au majadiliano ili kujiepusha na marudio ya wazo au fikra.<br><br>Stadi: kuonyesha upande wa kuegemea katika kutoa hoja zake (mtetezi au mpinzani).<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kusikiliza mawazo ya watu wengine hata kama hawakubaliani nayo. | 8 |

| | | |
|---|---|---|
| 13. Maandalizi na utekelezaji wa mjadala | Maarifa na ufahamu: kuelezea jinsi ya kutoa amri kwa kutumia hali ya kushurutisha kwa vitenzi.<br><br>Stadi: kutumia ishara za mwili kulingana na hoja inayohusika.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kukubali katika kutokubaliana na kuheshimu mawazo ya watu wengine. | 9 |
| Tathmini ya mada | | 2 |
| Vipindi vyote vya mada ya 4 | | 36 |

## SOMO LA 10: MDAHALO

### 10.1. Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Somo hili linajishughulisha na majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja maalum yaani mdahalo. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu mdahalo kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

### 10.2. Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Michoro ya watu wanaozungumza,
- Ubao,
- Chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Ikiwezekana, hakikisha kuwa kuna vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Unapowapa wanafunzi kazi mbalimbali, hakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wamepewa kazi tofauti zitakazowawezesha kupata ujuzi uliokusudiwa. Baadhi ya wanafunzi wenye matatizo ya kiakili huenda wasiweze kuchora lakini wakawa na uwezo wa kutumia rangi mbalimbali chini ya usaidizi wako au wenzao. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

### 10.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili, mwalimu atatilia mkazo kwenye:

**Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.

**Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).

**Maswali na majibu**: mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.

**Maelezo ya mwalimu**: mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

### Kazi Tangulizi

*Haya ni maswali ya kumwingiza mwanafunzi katika somo hili kwa urahisi. Ni maswali yanayoamsha upekuzi au udadisi na hayahitaji majibu ya papo hapo kutoka kwa mwanafunzi. Ni ya kujibiwa akilini mwa mwanafunzi, yaani si kazi ya makundi. Pia si kazi inayohitaji utafiti wowote. Mwanafunzi akiyasoma kwa upekee atakuwa na fursa ya kujua somo linahusu nini. Halikadhalika hii ni kazi itakayomsaidia mwalimu kutangulia somo kwa urahisi. Wanafunzi wapewe muda wa kusoma maswali hayo.*

## 10.4. Kusoma na Uufahamu

"Kusoma na Ufahamu" ni mojawapo wa stadi zinazotarajiwa kwa mwanafunzi wa lugha. Usomaji mzuri wa kifungu husaidia kukifahamu, na ndiyo sababu mwalimu anapaswa kuwasaidia wanafunzi wanaposoma kifungu, kwa kuzingatia matamshi bora ya maneno,hasa maneno mapya, matumizi ya alama za uakifishaji, n.k.

### 10.4. MAJIBU

### Zoezi la 1: (ukurasa 103)

Mwalimu aweke katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha awaombe wanafunzi kuchunguza na kueleza shughuli zinazoendelea kwenye mchoro.

### 10.4.1. Kifungu: Mazungumzo Baina ya Wanafunzi

Kifungu "Mazungumzo kati ya Wanafunzi" ni mazungumzo. Inapendekezwa kisomwe na

wanafunzi watano, kila mmoja nafasi yake: kiranja wa darasa wa, Shupavu, mwanafunzi wa 1, mwanafunzi wa 2 na mwanafunzi wa 3. Mwalimu awe makini ili asahihishe makosa ya kusoma yanayoweza kujitokeza.

### 10.4.2. Maswali ya Ufahamu

Maswali haya ya ufahamu yafanyiwe katika makundi madogo madogo. Wanapojibu maswali ya ufahamu wanafunzi wanatarajiwa kutunga sentensi nzima, siyo neno moja tu. Wasimamizi wa baadhi ya makundi wawasilishe majibu yao darasani. Yafuatayo ni majibu ya maswali ya ufahamu yaliyopendekezwa.

1. Shupavu ni mwanafunzi wa kidato cha sita, mchepuo wa lugha.

2. Mwalimu aliwaambia wanafunzi wamwalike Shupavu.

3. Mwaliko wake ulikuwa na madhumuni ya kuwasaidia wanafunzi wa kidato cha nne kufahamu maana ya "mdahalo" na namna ya kufanya mdahalo. .

4. Watu wanaohusika katika mdahalo na kazi zao:

    i. **kiongozi (au mwenyekiti)** : Kazi yake ni kuuongoza mdahalo na kutangaza upande mshindi;

    ii. **katibu**:Kazi yake ni kuandika hoja zinazotolewa na kuzisomea hadhara;

    iii.**wasemaji wa pande mbili**; yaani watetezi wanaoiunga mkono mada inayojadiliwa na wapinzani wanaoipinga mada yenyewe;
    iv.**Wasikilizaji-washiriki**: Hawa wana kazi ya kusikiliza mazungumzo yanayofanywa na pande hizo mbili; yaani upande wa utetezi na upinzani ili baadaye waweze kutoa hoja zao kuhusu yaliyozungumziwa.

5. Ili upande fulani ufaulu katika mdahalo, ni lazima kujiandaa ipasavyo; yaani kufanya utafiti na kuzipanga hoja vizuri kabla ya mdahalo kuanza. Kuzipanga hoja kunazifanya fikra zisije zikarudiwarudiwa.

6. Mdahalo huchukuliwa kama mashindano ya hoja kwa sababu mwishoni mwa mdahalo kuna upande unaotangazwa kuwa ni mshindi.

7. Mdahalo ni muhimu katika maisha ya binadamu, hasa kwa wanafunzi wanaojifunza lugha yoyote. Katika njia hii, midahalo hukuza uwezo wa kufikiri, hali ya udadisi wa mtu na ustadi wake wa kutumia lugha husika.

8. Kwa minajili ya kujiandaa kwa mazungumzo ya mdahalo, ni lazima kila upande kwanza ufanyie utafiti mada itakayozungumziwa. Kuzipanga hoja vizuri kabla ya mdahalo kuanza kutasaidia kutorudiarudia fikra zilizotolewa awali.

9. Aina nyingine za mazungumzo zilizozungumziwa katika kifungu hiki ni:

i. mjadala: mazungumzo juu ya jambo maalumu yanayofanywa kwa kutolea hoja jambo hilo.

ii. kongamano: mjadala juu ya jambo fulani unaofanywa na mkusanyiko wa watu baada ya wazungumzaji maalum kuuanzisha.

10. Ili kila mshiriki afanikiwe katika mdahalo, anatarajiwa kuwa na tabia mbalimbali. Kwa mfano, wakati wa kuzungumza unapofika, ni lazima kila mzungumzaji ajitahidi: kutumia lugha sahihi ya kuvutia na ishara za mwili zinazolingana na hoja husika, kuonyesha moyo wa heshima na kutokasirika ovyo au kutokata tamaa. Pia ni lazima kujiamini ili wasikilizaji-washiriki wakuunge mkono. Ni vizuri kuonyesha urafiki na ushirikiano, kwani kushindana kwa hoja si wakati wa kupigana au kugombana.

### 10.4.3.. Msamiati kuhusu Maana ya Mdahalo

***Zoezi la 2:** (ukurasa wa 106)*

*Zoezi hili ni la mwanafunzi binafsi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutoa maana ya maneno waliyopewa. Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi amefanya zoezi kisha asahihishe majibu ya wanafunzi. Mwanafunzi ana uhuru wa kutumia maneno yake mwenyewe. Zifuatazo ni maana zilizopendekezwa:*

1. Hoja: fikira maalumu ya mtu au watu kuhusu jambo fulani.

2. Majadiliano: mazungumzo baina ya watu yanayohusu jambo fulani

3. Watetezi: watu wanaopigania haki za watu wengine.

4. Wapinzani: watu wenye mitazamo tofauti ya mambo na watu wengine.

5. Kuheshimu: kuonyesha mtu kuwa unamthamini, kumfanyia mtu adabu.

**Zoezi la 3:** *(ukurasa wa 106)*

*Zoezi hili lifanywe na kila mwanafunzi binafsi, na hapo ndipo mwalimu atahakikisha kuwa kila mwanafunzi ameweza kutunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyozungumziwa katika kifungu. Sentensi zinazofuata ni mifano tu, yaani wanafunzi watatunga zao binafsi.*

1. Ni lazima walimu na wanafunzi wazingatie taratibu za masomo kama zilivyopangwa na washiriki, na hapo ndipo watafanikiwa.

2. Idadi ya watu wanaosikiliza redio imepua siku hizi.

3. Ni mada ipi inayozungumziwa sasa?

4. Mashindano ya mwaka huu yaliandaliwa na kuongozwa na Wizara ya Elimu.

5. Timu yetu ilishindwa kwa mara ya pili! Haikujiandaa vizuri.

**Zoezi la 4:** *(ukurasa wa 106)*

*Katika zoezi hili,maneno ya kutumia kujaza sentensi ni baadhi ya maneno yaliyotumiwa katika kifungu cha ufahamu. Ni namna moja ya kufundisha msamiati. Kwa hiyo, mwalimu achukue fursa hii kueleza maana za maneno atakayoulizwa na wanafunzi, na ahakikishe kwamba wanafunzi wanafahamu maana za sentensi walizozijaza.*

1. yaheshimiwe
2. mawazo
3. kiongozi
4. mazungumzo
5. upekee
6. huchanganya
7. maalumu
8. hoja
9. wapinzani
10. ustadi

### 10.4.4.. Sarufi: Matumizi ya Hali ya Kushurutisha kwa Vitenzi

**Zoezi la 5:** *(ukurasa wa 107)*

*Vitenzi vilivyotumiwa katika zoezi hili ni vitenzi visivyo na upekee wowote. Vina kiishio -a katika hali yake ya kawaida na ni vya silabi zaidi ya moja. Matumizi yake ni rahisi kuliko vile ambavyo vina upekee wowote. Lengo kuu hapa ni kuwasaidia wanafunzi kujionea wenyewe mabadiliko yanayojitokeza tunavyoviandika vitenzi vyenyewe kwa wingi.*

1. zungumzia
2. teteeni
3. panga
4. angalieni
5. simama

6. changanueni

7. zingatia

8. hakikisheni

9. ongozeni

10. changia

**Zoezi la 6:** *(ukurasa wa 107)*

*Ingawa wanafunzi hawajaelezewa kwa urefu mabadiliko yanayojitokeza wakati wa kuviandika vitenzi vyenyewe katika hali kanushi, mifano waliyopewa katika kitabu cha mwanafunzi itawasaidia kuyaona mabadiliko hayo. Mifano zaidi ikihitajika, mwalimu mwenyewe ataitoa ili zoezi lifanywe vizuri.*

1. msizungumzie

2. usitetee

3. msipange

4. usiangalie

5. msisimame

6. usichanganue

7. msizingatie

8. usihakikishe

9. usiongoze

10. msichangie

**Zoezi la 7:** *(ukurasa wa 108)*

*Zoezi hili ni tofauti kidogo na mazoezi yaliyolitangulia.Mabadiliko ya vitenzi tunavyoviandika kwa umoja au kwa wingi husababisha kubadilika kwa maneno mengine katika sentensi. (mfano: sentensi ya 9).*

1. Jitayarishe kujadili mada uliyopewa na mwalimu.

2. Chagueni makundi mengi kati ya yale ya kuunga ama ya kupinga kauli zilizotolewa.

3. Ongozeni midahalo hii kama wenyeviti waliochaguliwa darasani.

4. Toa maoni yako kuhusu jambo linalozungumziwa sasa.

5. Hakikisheni mnatumia Kiswahili sanifu katika michango yenu.

6. Tangazeni pande zilizoshinda baada ya hoja kutoka pande zote mbili kusomwa.

7. Soma vizuri hoja yote kama ilivyotolewa na kila upande.

8. Jiepushe na tabia mbaya ya kukasirika ovyo.

9. Tumieni Kiswahili Sanifu mnapotoa hoja zenu.

10. Weka mkono juu ili uruhusiwe kusema kitu.

**Zoezi la 8:** *(ukurasa wa 108)*

*Zoezi hili linalenga kumsaidia mwanafunzi kuzoea kutumia vitenzi shurutishi katika hali kanushi kwa kuingiza kiambishi -si-. Lakini zaidi ya hayo, mwalimu awasaidie wanafunzi kuona kwamba maana za sentensi hizo za hali kanushi ni tofauti sana na zile za hali yakinishi, na mara nyingi hazina maadili (mfano: sentensi ya 5).*

1. Msijitayarishe kujadili mada mliyopewa na mwalimu.

2. Usichague kundi moja kati ya lile la kuunga ama la kupinga kauli iliyotolewa.

3. Usiongoze mdahalo huu kama mwenyekiti aliyechaguliwa darasani.

4. Msitoe maoni yenu kuhusu maambo yanayozungumziwa sasa.

5. Usitangaze upande ulioshinda baada ya hoja kutoka pande zote mbili kusomwa.

6. Msisome vizuri hoja zote kama zilivyotolewa na kila upande.

7. Msijiepushe na tabia mbaya ya kukasirika ovyo.

8. Msiweke mikono juu na msiruhusiwe kusema kitu.

**Zoezi la 9:** *(ukurasa wa 108)*

*Wanafunzi wajaze jedwali kwa kutumia vitenzi vyenye hali shurutishi. Mwalimu awaelekeze ipasavyo na asahihishe majibu wanayoyatoa wanafunzi. Jedwali ijazwe kama mfano huu.*

| Kawaida (Umoja) | Kukanusha (Umoja) | Kawaida (Wingi) | Kukanusha (Wingi) |
|---|---|---|---|
| **1. kimbia** | usikimbie | kimbieni | msikimbie |
| 2. sema | **usiseme** | semeni | msiseme |
| 3. chunga | usichunge | **chungeni** | msichunge |
| 4. leta | usilete | leteni | **msilete** |
| **5. cheza** | usicheze | chezeni | msicheze |
| 6. choma | **usichome** | chomeni | msichome |
| 7. pata | usipate | **pateni** | msipate |

### 10.4.5.. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 10:** *(ukurasa wa 109)*

*Hili ni zoezi linalohitaji kutafakari. Kwanza ni lazima mwanafunzi ajue maana ya kila neno ili atambue uhusiano wake au tafauti yake na maneno mengine. Pia ni lazima ajue neno hilo hutumiwa katika uwanja gani, na hapo ndipo atatambua neno lililo tofauti na mengine. Zoezi hili lifanyiwe katika makundi.*

1. kiungulia
2. maana
3. kinywaji
4. kutukana
5. daktari
6. mwanasheria
7. mwanya
8. wafugaji
9. kufanya mtihani
10. kuomba Mungu

**Zoezi la 11:** *(ukurasa wa 109)*

*Zoezi hili ni la kutathmini ikiwa mwanafunzi amefahamu mambo muhimu yaliyozungumziwa kuhusu "Maana ya Mdahalo". Mambo hayo yameishazungumziwa*

*katika kifungu cha ufahamu na "maelezo muhimu kuhusu maana ya mdahalo". Zoezi hili lifanywe na kila mwanafunzi binafsi.*

1. Ni kweli
2. Si kweli
3. Ni kweli
4. Si kweli

**Zoezi la 12:** *(ukurasa wa 110)*

**Wanafunzi katika makundi, wajaze matini ifuatayo kwa kutumia maneno mwafaka. Wanafunzi wajaze kwa kufuata mtindo huu.**

Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja maalumu. Katika mdahalo, aghalabu wazungumzaji wawili kwa kila upande, mwenyekiti wa mdahalo huwa na wajibu mkubwa kwa kufungua na kuendesha mdahalo, kuchunguza nidhamu, kuwachagua wazungumzaji kutoka katika hadhira ili kutoa hoja zao, kupigisha kura na kufunga mdahalo.

Pia huwepo katibu wa mdahalo, ambaye kazi yake kubwa huwa ni kuandika hoja zinazotolewa na wazungumzaji mbalimbali, na mwishoni kusoma muhtasari wa hoja hizo zilizotolewa katika mjadala kwa pande zote mbili, pamoja na kutangaza matokeo ya kura zilizopigwa.

### 10.4.6. . Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 13:** *(ukurasa wa 110)*

Hili ni zoezi la kumtayarisha mwanafunzi kwenye somo litakalozungumzia "Andalio la mdahalo", ambapo atajihusisha na zoezi la mdahalo wenyewe. Hapa mwalimu aangalie ikiwa mwanafunzi anaweza kutoa hoja zake fupi, kwa kupinga au kuunga mkono mada iliyotolewa. Matumizi ya Kiswahili sanifu yazingatiwe. Waunga mkono na wapinzani wapewe fursa ya kujieleza.

Ikiwa mwanafunzi anakubaliana na mada, atazungumzia uzuri wa jua na ubaya wa mvua. Ikiwa hakubaliani na mada, basi atazungumzia uzuri wa mvua na ubaya wa jua.

### 10.4.7.. Utungaji

**Zoezi la 14:** *(ukurasa wa 110)*

*Katika kifungu kumezungumziwa sababu zinazoweza kuufanya upande mmoja kufaulu au kushinda katika mdahalo. Kinyume cha maadili hayo ndicho husababisha kutofaulu/*

*kushindwa katika mdahalo.Kazi kubwa hapa ni kuzieleza katika aya tatu. Mwalimu aangalie ikiwa mwanafunzi ameandika aya tatu. Mengi kuhusu utungaji/uandishi wa insha yatazungumziwa katika somo la 16.*

Baadhi ya sababu zinazoweza kuelezwa na mwanafunzi ni kama zifuatazo:

i. kutotumia lugha sahihi ya kuvutia;

ii. kutotumia ishara za mwili zinazolingana na hoja husika;

iii. kutoonyesha moyo wa heshima na kukasirika ovyo au kukata tamaa;

iv. kutojiamini ili wasikilizaji-washiriki wakuunge mkono;

v. kutoonyesha urafiki na ushirikiano;

vi. kupigana au kugombana.

# SOMO LA 11: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MDAHALO

## 11.1. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika ufundishaji wa somo hili, mwalimu atazitumia mbinu zifuatazo:

- **Kazi katika makundi:** wanafunzi washirikishwe kwa kuwaweka katika makundi na kuwasilisha kazi zao mbele ya darasa. Mwalimu afanye masahahisho na awasaidie wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- **Mdahalo:** katika somo hili wanafunzi watunge midahalo na wawasilishe matokeo ya kazi hizo za utungaji mbeleni mwa wenzao kwa ajili ya kukuza stadi yao ya kutafakari, kuzungumza, kusikiliza, kutetea na kupinga.
- **Kazi binafsi:** itakapokuwa lazima kila mwanafunzi atapewa kazi/zoezi lake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari au kwa kufanya tathmini).
- **Fikiri-jozi-shiriki:** Baada ya maoni tofauti kutoka kwa wanafunzi, mwalimu anapata habari juu ya ujuzi wa awali wanafunzi wake walio nao kuhusu somo hili. Mwalimu asahihishe zoezi hili pamoja na kusahihisha makosa.

**Zoezi la 1:** *(ukurasa wa 111)*

***Zoezi lifanyiwe katika makundi, wanafunzi wajadili kuhusu maswali na baadaye waeleze wanayoyajua kuhusu maswali kutokana na masomo ya awali. Mwalimu ajibu maswali baadaye kwa kufananisha na majibu ya wanafunzi.***

1. Unaona nini kwenye mchoro huu?
2. Unafikiri mchoro huu unazungumzia nini?
3. Mchoro huu unakukumbusha nini katika maisha yako?

## 11.2. Kusoma na Ufahamu

### 11.2.1. . Maswali ya Ufahamu

***Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu. Mwalimu atarekebisha makosa yanayojitokeza katika majibu ya wanafunzi.Majibu pendekezo:***

1. Watu wanaotajwa katika mdahalo ni mwenyekiti katibu, watetezi, wapinzani na mdhibiti muda, wasikilizaji washiriki.
2. Madhara yanayosabishwa na dawa za kulevya ni kama vile:

   a) Kutumbukia katika mienendo mibaya kama uvivu, ugomvi, ujambazi, umalaya, unyanyasaji, ukatili na magomvi;

b) Kukosa akili timamu inayomwezesha kuwa na mipango mizuri kuhusu maisha yake;

c) Kubadilisha mwenendo wa kawaida unaotakiwa katika jamii;

d) Kujitia nguvu zinazowawezesha kufanya jambo lolote baya;

e)Kumbadili mtu kwa kila kitu anachofanya kuanzia fikira zake, mipango na utekelezaji wa shughuli zake;

f) Kupatwa na magonjwa ya aina mbalimbali ;

g) Kukosa nguvu za kufanya kazi yoyote katika kulijenga taifa lake ;

h) Kugeuka mzigo mkubwa kwa taifa zima na jamii;

i) Kuzorota au kusahau kazi;

j) Kushiriki na makundi ya wahalifu.

3. Toa majukumu ya wazazi kuhusu malezi ya watoto wao.

a) Kuwapa malezi mema.

b) Kuwa karibu ya vijana wao na kuwaonya, kuwakanya, kuwashauri kulingana na hali au matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii zao na mengineyo.

4. Watetezi hutetea kwamba dawa za kulevya huathiri vijana kiasi kwamba hawa vijana hugeuka na kujikuta katika hali ya uvivu, ugomvi, ujambazi, na maovu mengine mengi.

5. Shauri tunaloweza kuwapatia vijana wa leo ni kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya na kuheshimu majukumu yao kwa madhumuni ya kujiendeleza na kuendeleza nchi yao.

6. Kinachoweza kufanywa ili vijana wa leo wajiepushe na dawa za kulevya ni kuwasaidia vijana wa leo kuunda vilabu vya kupambana dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya, kuunda makampuni madogo madogo ili waweze kujiajiri badala ya kukaa bila kufanya kazi.

7. Dawa za kulevya zaweza kusababisha umaskini kwa sababu wakati watu wanapojiingiza katika matumizi ya dawa hizi hudhoofika kiasi kwamba hupoteza nguvu za kufanya kazi au nguvu za upangaji na utekelezaji wa miradi ya kujiendeleza na wote kugeuka wavivu. Hivi huathiri pato lingetokana na kazi.

8. Mtu huyu huathirika kwanza katika ubongo kama ilivyozungumzia na mwenzangu aliyenitangulia na kisha mwili wake hudhoofika. Madhara huzidi kuongezeka mpaka wakati anapoanza kukosa nguvu za kufanya kazi yoyote

katika kulijenga taifa lake na yeye kugeuka mzigo mkubwa kwa taifa zima na wanajamii wengine.

9. Matumizi mabaya ya teknolojia mpya na mitandao huweza kuwa tatizo miongoni mwa vijana kwa sababu vijana wa leo wanapopoteza muda kwa kuangalia mitandao ambayo huwafanya waige tabia mbovu za watu wasio na adabu na mienendo mizuri, ndipo wanapoathiriwa na tabia wanazoziiga. Kijana anapomaliza muda wake kwa kuangalia mitandao isiyomnufaisha kwa chochote au kutumia simu visivyo, ni dhahiri kwamba hataweza kuwa na mipango imara ya kuendeleza jamii yake.

10. Aina ya dawa za kulevya na maelezo yake:

a) Kokeni: ni aina ya dawa ambayo hupatikana katika hali ya ungaunga ulio mweupe na kutumiwa kwa njia ya kuvuta kwa pua au kuchanganywa na maji na baadaye kujidunga mwilini kwa kutumia sindano na inapoingia kwenye damu huenda kwenye ubongo na kuzuia ufyonzwaji wa vihisishi ambavyo husababisha ile hali ya furaha, mchangamfu na kujisikia mwenye nguvu.

b) Heroini: Ni aina ya dawa ya kulevya ambayo huweza kutumika kwa kuvuta kwa pua, kuvuta kama sigara na kwa kuchoma kwenye mshipa na kuingia katika damu na kuendelezwa neva na kukandamiza ufanyaji kazi wake kiasi kwamba yeye hujisikia mwenye furaha na raha na mwili huhema polepole.

c) Bangi: ni majani ya mbangi ambao ndani yake mna dawa inayosababisha namna ya ulevi unaotegemea kiasi cha dawa kinachoingia mwilini.

d) Miraa: ni dawa inayoitwa pia mairungi, mirungi, veve, gomba. Dawa hizi huchangamsha ubongo kwa kuleta hisia ya kujihisi vizuri na imani kwa muda na baada ya hisia hizi huwa kwa kawaida kuna kipindi cha kujihisi vibaya, au kudhoofika.

### 11.2.2. Msamiati kuhusu Mdahalo

**Zoezi la 2:** *(ukurasa wa 119)*

*Mwalimu atawaomba wanafunzi kuunda makundi ya wanafunzi wawili wawili na kufanya zoezi husika katika makundi wanayoyaunda. Hapa wanafunzi watatumia kamusi kwa kuelewa maana ya msamiati mpya na kuutumia katika sentensi. Katika zoezi hili ni wajibu wa mwalimu kuchunguza kama zoezi linalofanywa na wanafunzi katika makundi linaendelea ipaswavyo. Watakapomaliza kufanya zoezi mwalimu ataomba makundi mbalimbali kuwasilisha kazi zao mbele ya darasa. Mwalimu arekebishe makosa yanayoweza kujitokeza. Wakati wa utungaji wa sentensi mwalimu hupaswa kutoa mfano wa sentensi kama hivi:*

1. ***Upande wa utetezi*** wa mada yetu ulituelezea kwamba dawa za kulevya ni dawa zinazoangamiza vijana wa leo.

2. Walipomaliza kutoa hoja zao, walielezewa na upande wa ***upinzani*** kwamba malezi ni mojawapo ya nguzo za maendeleo.

3. Kila mzazi ana ***wajibu*** wa kumtunza mtoto wake hadi kiwango cha kumaliza masomo ya sekondari na ikiwezekana hata chuo.

4. Unyanyasaji wa wanawake ni ***janga*** kubwa katika jamii kwa sababu hali hii huathiri sana akili na haki za wanawake.

5. Wanafunzi wengi ***huhofu*** kwenda nje wakati wa usiku.

6. Uzalendo huwafanya binadamu kujiepusha katika mambo maovu kama vile uvivu, ***uzinzi***, matumizi ya dawa za kulevya na mengineyo.

7. Watoto ***wanapozama*** katika matumizi mabaya ya simu hujitumbukiza katika uasherati.

8. Akili ni ***johari***aliyopewa mwanadamu na Mungu..

9. Binadamu ***walitunukiwa*** mambo mengi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ikiwa ni pamoja na kutunza na kuendeleza maisha yake.

10. Kariza alizidisha muda wake wa kutoa hoja zao na ***mdhibiti-muda*** alimkataza kuendelea kutoa mchango wake..

**Zoezi la 3:** *(ukurasa wa 119)*

*Wanafunzi wajaze nafasi tupu kwa kutumia neno linalofaa kutokana na kifungu walichokisoma. Mwalimu awasaidie wanafunzi kwa kuwaelekeza .*

1. Kukukataza
2. Kutambulisha
3. Fursa
4. Kukumbusha
5. Uliridhika
6. Mitandao

**Zoezi la 4:** (ukurasa wa 119)

*Zoezi hili lifanywe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waelekezwe namna ya kuambatanisha maneno na maana yake kutoka sehemu B. Mwalimu arekebishe wanapokutana na matatizo.*

1. **c**

2. **d**

3. **j**

4. **b**

5. **a**

6. **h**

7. **i**

8. **e**

9. **g**

10. **f**

## 11.4. 3. Sarufi: Vitenzi vya Silabi Moja na Hali Shurutishi ya Vitenzi

**Zoezi la 5:** *(ukurasa wa 120)*

**Mwalimu ataomba wanafunzi kusoma kifungu cha habari na kubainisha sentensi zilizotolewa na kubainisha nia isiyobadili ya vitenzi vinavyoandikwa kwa rangi iliyokoza:**

**Kwa mfano: Mpe** msomaji mkuu fursa ya kutoa hoja zake.

**Jibu:** Mpe→ **Kupa**

Atakayekula→ **Kula**

Watakapokupwa→ **Kupwa**

Wamekula→ **Kula**

Hulia→ **Kula**

Umekunywa→ **Kunywa**

Kumekucha→ **Kucha**

**Zoezi la 6:** *(ukurasa wa 120)*

Mwalimu awaulize wanafunzi sifa zisizobadilika katika vitenzi walivyoainisha. Katika lugha ya Kiswahili kuna vitenzi ambavyo huwa na silabi moja. Vitenzi hivi vinapotumiwa huwa na miundo tofauti na vitenzi vingine vyenye silabi nyingi. Mwalimu awaelekeze kwa majibu sahihi. Vitenzi hivyo ni kama: kucha, kufa, kuja, kula, kunywa, kunya, kupa,

kupwa, kuwa. Vitenzi vyenye silabi moja huambatanishwa na kiambisha ku- katika hali mbalimbali ili sentensi zikubalike kuwa ni sentensi sahihi.

**Zoezi la 7:** *(ukurasa wa 120)*

*Zoezi hili lifanywe katika makunwdi ya wanafunzi wawili wawili. Mwalimu aongoze kwa kuiga mfano waliopewa kitabuni kisha awaombe wasahihishe zoezi na kuwaelekeza wanafunzi kwenye majibu sahihi.*

| Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| 1. Nita**kuja** kesho | Sitakuja kesho |
| 2. Nina**ku**nywa chai | Sinywi chai |
| 3. Mimi **hula** mkate | Mimi sili mkate |
| 4. Nime**kunywa** maji | Sijanywa maji |
| 5. Mama **anakuja** leo | Mama haji leo |

**Zoezi la 8:** *(ukurasa wa 121)*

***Zoezi hili lifanywe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili. Mwalimu aongoze kwa kuiga mfano waliopewa kitabuni kisha awaombe wasahihishe zoezi na kuwaelekeza wanafunzi kwenye majibu sahihi.***

| Hali yakinishi | Hali shurutishi |
|---|---|
| 1. Nitakuja kesho | Kuja kesho |
| 2. Ninakunywa chai | Kunywa chai |
| 3. Mimi hula mkate | Kula mkate |
| 4. Nimekunywa maji | Kunywa maji |
| 5. Mama anakuja leo | Kuja leo |

**Zoezi la 9:** *(ukurasa wa 121)*

***Zoezi hili lifanywe na kila mwanafunzi binafsi. Mwalimu aongoze kwa kuiga mifano waliopewa kitabuni hapo juu kisha awaombe wasahihishe zoezi na kuwaelekeza wanafunzi kwenye majibu sahihi.***

1. Kuja kesho asubuhi.
2. Kunywa chai ile ya rangi.
3. Kula chakula sasa hivi.
4. Nipe sahani hiyo.
5. Kupwa shimo lile.

**Zoezi la 10:** *(ukurasa wa 121)*

***Zoezi hili nalo liwe la kibinafsi. Mwalimu aombe wanafunzi kukamilisha sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa kama vile: walikufa, nipe, nile, zipwe, kutwa, nilipokuwa, kula, kimeliwa, tuliokuwa, kunywa.***

1. ***Nile***
2. ***Walikufa***
3. ***Kula***
4. ***Kunywa***
5. ***Nipe***
6. ***Zijae***
7. ***Nilipokuwa***
8. ***Kimeliwa***
9. ***Tuliokuwa***
7. ***Walikuja***

**Zoezi la 11:** *(ukurasa wa 122)*

***Zoezi hili liwe la mwanafunzi yeye binafsi. Mwalimu aombe kila mwanafunzi kutumia vitenzi alivyopewa katika mabano kwa kukamilisha sentensi alizopewa. Mwalimu azunguke darasani kuchunguza kwamba zoezi liko linafanywa vilivyo na wanafunzi na atoe maelezo muhimu kwa yeyote anahitaji kuelekezwa.***

1. **Tumekula**
2. **Alikufa**
3. **Kunywa**
4. **Kumekucha**
5. **Kuja**

### 11.2.4. Matumizi ya Lugha: Maandalizi na Utekelezaji wa Mdahalo

**Zoezi la 12:** *(ukurasa wa 122)*

***Zoezi hili ni la kibinafsi, kila mwanafunzi asome maelezo kuhusu maandalizi na utekelezaji wa mdahalo kisha ajibu maswali aliyopewa katika kitabu cha mwanafunzi. Mwalimu asahihishe makosa yatakayojitokeza kwa kila mwanafunzi kuhusu matumizi ya lugha.***

**Majibu yanayopendekezwa:**

1. Kanuni zinazoongoza maandalizi ya mdahalo ni kama vile:

a. Kuchagua mada ya kuzungumzia katika mdahalo: uchaguzi huu hufanyika kwa kupiga kura;

b. Kumchagua mwenyekiti wa mdahalo: mwenyekiti huchaguliwa kwa kupiga kura na atakayechaguliwa ni yule mwenye uwezo wa kuongoza na kuendesha mdahalo;

c. Kumchagua katibu wa mdahalo: mhusika huyu pia huchaguliwa, yeye ana wajibu ya kuandika na kuwasomea hadhira matokeo ya mdahalo;

d. Kumchagua mdhibiti-muda: huyu ana jukumu la kuchunguza kwamba kila mhusika anatumia muda wake wa kutoa hoja zake ipasavyo;

e. Kupanga wahusika kwa upande wa utetezi na upande wa

f. upinzani kama wasemaji wakuu wa pande hizo;

g. Kupanga namna ya kukaa kwa wahusika wa mdahalo upande wa utetezi na upande wa upinzani. Kitendo hiki huwafanya wahusika wakae pande mbili (upande wa kulia na upande wa kushoto) ambapo watabadilishana mawazo kwa urahisi;

h. Kupanga muda utakaotumiwa na wahusika wa pande hizo mbili.

2. Njia zinazotumiwa katika utekelezaji wa mdahalo

a. Mwenyekiti hufungua mdahalo kwa kuwatambulisha wahusika wa mdahalo akianzia kwake kama kiongozi wa mdahalo kisha katibu na washiriki wa pande mbili zitakazojadiliana yaani upande wa utetezi na upande wa upinzani;

b. Kabla ya kuanza kutoa hoja za pande mbili husika mwenyekiti huwakumbusha mada mahsusi itakayozungumziwa;

c. Mwenyekiti huwapatia wahusika wasikilizaji muda wa kutoa maoni yao kuhusu mada iliyokuwa inazungumziwa;

d. Kila mhusika hulazimishwa kuheshimu muda wake wa kutetea au kupinga mada husika na muda wa kunyamaza kwa kusililiza hoja za wengine;

e. Mwenyekiti huwapatia wasikilizaji washiriki muda wa kutoa maoni kuhusu mada inayojadiliwa;

f. Wahusika hupaswa kuheshimu amri ya mwenyekiti;

g. Mwenyekiti humpatia katibu fursa ya kuwasomea alivyoandika kama matokeo ya mdahalo;

h. Mwenyekiti husimamia zoezi la kupiga kura na kumuomba katibu aandike

idadi ya kura kwa kila upande ili kuonyesha upande ulioibuuka na ushindi na ule ulioshindwa;

i. Mwenyekiti hutangaza matokeo ya kura na kuwapongeza waliohudhuria na kufunga mdahalo.

3. Taja mifano ya mada zinazoweza kujadiliwa katika mdahalo ni kama zifuatazo:

a. Elimu ni nguzo muhimu katika maendeleo ya jamii.

b. Ufugaji waweza kuwafanya vijana kujiepusha na umaskini kwa urahisi.

c. Kuwekwa ndani kwa wanaofanya makosa ni njia yenyewe ya kuwarekebisha wanaofanya makosa.

d. Waganga ni watu muhimu maishani mwetu kuliko watu wanaofanya kazi nyingine. .

4. Mwanafunzi kwa kujibu swali hili atatilia mkazo kwenye umuhimu wa mdahalo katika ukuzaji wa uwezo wa kujieleza kwa lugha. Uwezo huo ni ule wa kimazungumzo, kifikra. Mwanafunzi atatetea fikra zake kimaelezo ili aweze kuwashawishi watakaosoma hoja zake.

**Zoezi la 13:** *(ukurasa wa 123)*

**Zoezi hili lifanywe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili. Mwalimu ataomba wanafunzi kufanya makundi kisha katika makundi husika wapange maneno waliyoyapewa kwa sentensi sahihi. Mwalimu achunguze kwamba wanafunzi wako wanafanya kazi vilivyo.**

**Majibu yanayopendekezwa:**

1. Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja maalum.

2. Katika mdahalo wazungumzaji wakuu huwa na kazi za kutoa maoni yao kuhusu mada fulani.

3. Utekelezaji wa mdahalo huzingatia makao ya mwenyekiti na katibu wake tena watetezi na wapinzani

4. Gongo likiingia bongo hukimbia

5. Penye ulevi ndipo penye matata

6. Penye mvinyo ndipo penye hatari

7. Cha mlevi huliwa na mgema.

**Zoezi la 14:** *(ukurasa wa 124)*

***Zoezi hili nalo lifanyike katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Mwalimu aombe wanafunzi kutafuta maneno kumi yenye maana kamili katika mraba waliwopewa.***

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | W | A | Z | O | X | T | K | U | I |
| I | N | A | M | R | I | R | T | U | T | O |
| N | A | J | I | B | U | K | E | H | U | T |
| A | S | I | K | M | D | A | H | A | L | O |
| J | Y | B | C | M | B | M | A | K | A | O |
| I | T | U | H | R | U | M | Y | I | O | E |
| L | Z | W | K | H | A | K | I | K | A | J |
| I | T | I | K | A | D | I | W | I | S | O |
| A | H | K | Y | K | U | H | U | S | U | I |
| E | T | N | M | H | O | J | A | H | G | T |
| M | A | J | A | D | I | L | I | A | N | O |

### 11.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 15:** *(ukurasa wa 124)*

***Zoezi hili lifanyike katika makundi ya wanafunzi sita kwa kila kundi, wanafunzi wachague mada ya mdahalo kati ya mada walizopewa. Mwalimu aombe makundi husika kutunga mdahalo kisha aombe wanafunzi kuwasilisha mdahalo waliotunga. Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi katika kundi ametoa hoja zake kuhusu mada katika pande zote mbili utetezi na upinzani.Baadhi ya mada zitakazochaguliwa:***

1. Utalii ni nguzo muhimu katika ujenzi wa nchi yetu.

2. Mali bila daftari hupotea bila habari.

## 11.3 Kuandika

**Zoezi la 16:***(ukurasa wa 124)*

***Mwanafunzi afanye zoezi hili binafsi. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kutunga mdahalo kuhusu mada zinazopatikana katika kitabu cha mwanafunzi wakizingatia kanuni za kutunga mdahalo.***

1. Matumizi ya teknolojia mpya ndiyo nguzo muhimu ya kurahisisha maendeleo ya jamii.

2. Kujiunga pamoja katika vyama vya kuzalisha mali hutajirisha.

# SOMO LA 12: MJADALA

## 12.1. Ujuzi wa Awali/Utangulizi

Kusoma somo hili si mara ya kwanza kwa wanafunzi wa kidato cha nne. Waligusia kwenye somo hili kidato cha tatu. Somo lililotangulia lilitilia mwangaza zaidi kuhusu mdahalo na andalio la mdahalo.

## 12.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vifuatavyo huweza kutumiwa na mwalimu wakati wa kufundisha somo hili:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Michoro tofauti inayohusiana na somo,
- Flipichati
- Karatasi manila

Mwalimu achague vifaa vingine husika kulingana na muktadha. Ajaribu kuwa mbunifu katika ufundishaji wake.

## 12.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika ufundishaji wa somo hili, mwalimu atumie mbinu zifuatazo:

- **Kazi ya kibinafsi:** itakapokuwa lazima kila mwanafunzi atapewa kazi/ zoezi lake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari au kwa kufanya tathmini).
- **Kazi za kimakundi:** wanafunzi washirikishwe katika kazi za kimakundi na kuwasilisha kazi zao mbele ya darasa. Mwalimu afanye masahahisho na awasaidie wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- **Mjadala:** katika somo hili wanafunzi wafanye mijadala ili kukuza stadi ya kusikiliza na kuzungumza.
- **Fikiri-jozi-shiriki:** Baada ya maoni tofauti kutoka kwa wanafunzi, mwalimu anapata habari juu ya ujuzi wa awali wanafunzi wake walio nao kuhusu somo hili. Mwalimu asahihishe zoezi hili pamoja na kusahihisha makosa.

**Zoezi la 1:** *(ukurasa wa 125)*

***Zoezi lifanyiwe katika makundi, wanafunzi wawaze kuhusu maswali na baadaye waeleze wanayoyajua kuhusu maswali kutokana na masomo ya awali. Mwalimu ajibu maswali baadaye kwa kufananisha majibu ya wanafunzi.***

1. Nini maana ya mjadala?

2. Ni watu wangapi wanaoongoza mjadala?

3. Ni tofauti gani inayojitokeza kati ya mdahalo na mjadala?

## 12.4. Kusoma na Ufahamu

### 12.4.2. Maswali ya Ufahamu

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, soma kifungu cha habari kwa ufasaha na kujibu maswali ya ufahamu. Mwalimu arekebishe makosa yanayojitokeza katika majibu ya wanafunzi.

Majibu pendekezo:

1. Mjadala ni mazungumzo juu ya jambo maalum ambayo hufanywa na watu kwa kutoa hoja zao kwa jambo fulani linalotakiwa ufafanuzi au ufumbuzi wa suala lililopo. Mjadala huhusisha watu wengi wanaotoa hoja kuhusu mada fulani.

2. Katika mjadala, kiongozi ana kazi ya kuongoza majadiliano kwa kupanga muda wa kuzungumza kwa kila msemaji anayeshiriki katika mazungumzo. Kutokana na hayo, hakuna msemaji ambaye anaruhusiwa kutoa hoja bila kumuomba fursa kiongozi wa majadiliano. Kama kuna wasemaji ambao wanataka kukiuka mada katika hoja zao, kiongozi wa mjadala huwarekebisha kwa kuwakumbusha mada inayotolewa hoja.

3.

- Mjadala hukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa majadiliano.
- Mjadala hukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani.
- Mjadala humwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari.
- Mjadala humsaidia mtu kutambua kipaji alicho nacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira na kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha. - Mjadala humzoeza mtu kusikiliza maoni ya watu wengine, kupinga au kutetea maoni na hoja zao.

- Mjadala hukuza uwezo wa maongezi kuhusu swala fulani na hupanua kiwango chao cha msamiati na hupunguza uoga wa kuongea hadharani.

4. Washiriki katika mjadala ni wa aina mbili. Kiongozi na washiriki (hadhira).

5. Kazi ya hadhira katika mjadala ni kusikiliza na kutoa mchango wao kuhusu suala linalojadiliwa.

6. Lengo la kila msemaji ni kutoa mawazo kwa nia ya kutatua tatizo fulani linalofafanuliwa na kujadiliwa kwa pamoja ili kutafuta ufumbuzi na suluhisho linalofaa na kupata namna bora ya kutenda mambo yanayozungumziwa. Katika mjadala hakuna kuwania ushindi; yeyote ambaye ana la kusema huruhusiwa na hutoa hoja kama apendavyo kuhusu mada ile inayohusika bila kukiuka ukweli uliopo.

7. Mifano ya mambo yanayoweza kujadiliwa katika mjadala ni elimu, madhara ya dawa za kulevya, maendeleo, Namna ya kijana kuweza kujiajiri, namna ya kukabiliana na itikadi ya mauaji ya kimbari, dhidi ya watutsi

8. Mjadala husaidia kujua lugha kwa sababu:

- mazungumzo yanayofanywa huwazoeza wengi kusikiliza na kupima maoni na hoja za wenzao, -
- hukufanya utumie lugha kwa kuzungumza kama njia moja ya kukuza uwezo wa mawasiliano, majadiliano, mahojiano,
- humwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri,
- hupanua kipaji alicho nacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira na kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha.

9. Maadili ya kukuza fursa ya kuelewana, hupanua njia ya amani, kuheshimiana kulingana na mawazo tofauti yanayotolewa na kila mzungumzaji.

10. Mjadala huwasaidia watu kuwasiliana na kuelewana moja kwa moja. Washiriki huongeza uwezo kwa njia tofauti za kuelewana juu ya jambo moja maalumu. Washiriki huuliza maswali ili kujua ukweli.

### 12.4. 3. Msamiati kuhusu Maana ya Mjadala

**Zoezi la 2**: *(ukurasa wa 127)*

***Mwalimu amwombe mwanafunzi kufanya zoezi hili kibinafsi. Mwanafunzi atumie kamusi kwa kuelewa maana ya msamiati mpya na kuutumia katika sentensi. Mwalimu achunguze kazi zinazofanywa na wanafunzi. Achague sampuli ya wanafunzi watatu wawasilishe kazi yao mbele ya darasa. Mwalimu arekebishe makosa yanayoweza kujitokeza. Mwanafunzi anaweza kutunga sentensi kama zifuatazo:***

1. Mutoni alifanya utafiti wa kutosha akapata **ufumbuzi** wa chanzo cha ajali za barabarani.

2. Binadamu hawezi kuishi bila hukumbwa na **migogoro**.

3. Wanafunzi walijichagulia wenyewe **kiongozi** wa darasa.

4. Wananchi walijadiliana kuhusu **suala** fulani kuhusu maendeleo.

5. **Hadhira** ilikubaliana kuhusu maendeleo.

6. Unapozungumza ni muhimu kuhakikiha hoja zako zinakuwa bayana.

7. Ni jukumu la kila mmoja wetu kufanya kazi kwa bidii.

Tunapaswa kutoa mchango wetu ili kufanikisha zoezi la ukarabati wa shule ya kijiji.

Majadiliano ni nyenzo muhimu ya kutatua migogoro katika jamii

Nilifurahi kuona nimesimama mbele ya hadhira iliyokuwa imechangamka.

**Zoezi la 3:** *(ukurasa wa 128)*

***Zoezi hili lifanywe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wakati wanapoelezwa namna ya kuambatanisha maneno na maana yake kutoka kundi B. Mwalimu arekebishe wanapopata matatizo.***

1. h
2. l
3. j
4. g
5. c
6. a
7. d
8. k
9. f
10. i
11. b
12. e

**Zoezi la 4:** *(ukurasa wa 128)*

***Wanafunzi wajaze nafasi tupu kwa kutumia neno linalofaa kutokana na kifungu walichokisoma. Mwalimu awasaidie wanafunzi kwa kuwaelekeza.***

1. kipaji
2. kiongozi
3. hadhira
4. kupanga
5. mahojiano
6. mjadala
7. mazungumzo
8. hoja
9. fursa
10. kuwashirikisha
11. mada

### 12.4.4. Sarufi: Hali Shurutishi ya Vitenzi

**Zoezi la 5:** *(ukurasa wa 129)*

***Mwalimu awaombe wanafunzi wawili wawili kutafuta maneno yenye viambishi tamati vyenye kiambishi tamati kisichokuwa -a. Wanafunzi wawasilishe kazi mbele ya darasa kwa kueleza maumbile yake. Mwalimu awaelekeze kwa majibu sahihi.***

Vitenzi hivyo ni kama: **kuhitaji, kushiriki, kushawishi, kufikiri, kukidhi**.

**Zoezi la 6:** *(ukurasa wa 130)*

***Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi watatu watatu. Mwalimu awaongoze kwa kuiga mfano waliopewa kitabuni kisha asahihishe zoezi na kuwaelekeza wanafunzi kwenye majibu sahihi.***

1. heshimuni
2. Saidiana
3. pangeni

4. somana

5. teteeni

6. Pigianeni

7. andikeni

8. dharauni

9. shirikiana

### 12.4.5.. Matumizi ya Lugha kuhusu Maana ya Mjadala

**Zoezi la 7:** *(ukurasa wa 131)*

***Wanafunzi wasome maelezo maluumu katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kisha wajadiliane kuhusu maswali yaliyoulizwa na baadaye wawasilishe majadiliano yao wakisaidiwa na mwalimu.***

***Majibu pendekezo:***

1. Si kweli. Mjadala unaongozwa na mtu mmoja au watu wawili ambao wanazusha mawazo na kuhakikisha ikiwa kuna mwenendo mwema kati ya washiriki wa mjadala huo.

2. Kiongozi wa mjadala ndiye anayetoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa.

3. Malengo ya mjadala mzuri:

- Kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa mjadala.
- Kukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani.
- Kumwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari.
- Kumwezesha mtu kutambua kipaji alicho nacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira.
- Kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha.
- Kumzoeza mtu kusikiliza na kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine.
- Kuwapa watu wasaa wa kuelewana na wengine kutoka maeneo mbalimbali.

Wanafunzi wajadili malengo matatu katikati ya haya yaliyotolewa. Mwalimu asahihishe kazi zao na kuwaelekeza ipasavyo..

4. Katika mjadala hakuna mshindi kwa sababu kila hadhira hutoa mchango wake kuhusu swala linalojadiliwa. Kila yeyote aliye na hoja huomba fursa ya kuzungumza. Mjadala si mashindano bali lengo la kila msemaji ni kutoa mawazo kwa nia ya kutatua tatizo fulani linalofafanuliwa na kujadiliwa kwa pamoja ili kutafuta ufumbuzi na suluhisho linalofaa na kupata namna bora ya kutenda mambo yanayozungumziwa. Kwa hiyo, hakuna kuwania ushindi; yeyote ambaye ana la kusema huruhusiwa na hutoa hoja kama apendavyo kuhusu mada inayohusika bila kukiuka ukweli uliopo.

5. Wahusika katika mjadala ni kiongozi ambaye ana jukumu la kuongoza majadiliano kwa kupanga muda wa kuzungumza kwa kila msemaji anayeshiriki katika mazungumzo. Hakuna msemaji anayeruhusiwa kutoa hoja bila kumuomba fursa kiongozi wa majadiliano. Pia, kiongozi huwarekebisha kwa kuwakumbusha mada inayotolewa hoja.

Hadhira hushiriki katika mazungumzo kwa kusikiliza na kutoa mchango wao kuhusu swala linalojadiliwa. Kila yeyote aliye na hoja huomba fursa ya kuzungumza.

**Zoezi la 8**: *(ukurasa wa 132)*

***Zoezi hili ni la kibinafsi, kila mwanafunzi aunde sentensi sahihi kutokana na maneno aliyopewa katika kitabu cha mwanafunzi. Mwalimu asahihishe kila mwanafunzi makosa yatakayojitokeza kuhusu matumizi ya lugha.***

1. Mjadala hukuza uwezo wa kushawishi watu katika hadhira.
2. Mawasiliano hutupa fursa ya kuelewana na wenzetu kutoka sehemu mbalimbali.
3. Ni lazima kupanga mawazo utakiwapo kutoa hoja.
4. Msemaji hutoa maoni yake anaporuhusiwa.
5. Mtu hawezi kujiendeleza wakati ambapo hajielimishi.

### 12.4.6. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 9:** *(ukurasa wa 132)*

***Zoezi hili lifanyike katika makundi ya wanafunzi watano watano. Watajadili mada walizopewa na kila kundi liwasilishe kazi yao. Mwalimu arekebishe makosa ya kimazungumzo yatakayojitokeza. Mwalimu ahakikishe kwamba amewashirikisha wanafunzi wote.***

**Mada ni hizi zifuatazo:**

1. Maendeleo nchini huyafanya maisha ya Wanyarwanda yabadilike kwa kiwango cha juu.
2. Mikakati ya kuepuka maambukizi na kujikinga ugonjwa wa malaria.

### 12.4.7. Utungaji

**Zoezi la 10:** *(ukurasa wa 132)*

***Zoezi hili lifanywe kibinafsi. Mwalimu awaombe wanafunzi kutunga insha kwa kutumia kiambishi-ngeli- katika usemi wa asili na usemi wa taarifa. Mwalimu asahihishe makosa ya kimaandishi***.

**Mada ni hizi zifuatazo:**

1. Ubaya wa dawa za kulevya katika maisha ya binadamu.

2. Mtu ambaye hasikii ushauri mwema wa wakubwa, hupata hasara kubwa.

# SOMO LA 13: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MJADALA

## 13.1. Ujuzi wa awali/ Utangulizi

Dhana ya mjadala si neno jipya kwa wanafunzi wa kidato cha nne kwa sababu waliligusia katika kidato cha tatu.

## 13.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vihitajiwavyo katika somo hili hutegemea aina ya kila zoezi. Kwa hiyo inambidi mwalimu atarajie zana husika kulingana na mahitaji ya wanafunzi. Mfano wa vifaa vya kupendekezwa ni kama vifuatavyo:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Flipichati na kalamu zake husika
- Michoro mbalimbali yenye dhana ya umbo au funiko.
- Vitabu au majalida kuhusu mjadala.

## 13.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Mwalimu achague mbinu inayofaa kulingana na aina ya zoezi husika. Kwa mfano:

- Mbinu ya tafakari binafsi
- Ushirikiano kwa jozi
- Mbinu ya "waza-jozi-shiriki" kwenye kidokezo, majibu ya ufahamu, n.k.
- Kazi ya kimakundi kuhusu mazoezi ya matumizi ya msamiati wa msingi,
- Mijadala katika zoezi la kusikiliza na kuzungumza.

Tanbihi:

Mwalimu awahudumie kwa upekee wanafunzi wenye mahitaji maalumu kulingana na tatizo walilo nalo.

Kwa mfano:

- Amwache akae mbele yule aliye na tatizo la kutoona vizuri kwenye ubaoni;
- Atumie lugha ya mwili (body language) kwa kumsaidia mwanafunzi aliye na tatizo la kusikia au kusema.

- Utafiti kesi: mbinu hii itumie hasa katika mazoezi ya kubuni hadithi simulizi.

**Zoezi la 1:** (*ukurasa wa 133*)

**Wanafunzi watazame mchoro kutoka kitabu cha mwanafunzi kisha wajadili yanayotendeka kwenye mchoro.**

## 13.4. Majibu

### 13.4.1. Maswali ya Ufahamu

**Wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu katika makundi ya wanafunzi watatu watatu wakiongozwa na mwalimu. Mwalimu atathmini kazi za wanafunzi.**

1.Kiongozi ndiye anawaruhusu washiriki kutoa hoja zao katika mjadala. Hakuna msemaji anayeruhusiwa kutoa hoja bila kumuomba fursa kiongozi wa majadiliano.

2. Malezi ya msingi mtoto huyapata kutoka kwa wazazi wao nyumbani. Nyumbani ndipo mtoto anapopata malezi ya msingi ambayo humulikia na humsaidia kufanikiwa katika maisha yake.

3. Dawa za kulevya husababisha magonjwa mengi na huharibu ubongo wa watoto.

4. Mzazi ana wajibu wa kuwapeleka watoto shuleni kwa sababu ndipo mtoto anapata mwenendo mwema utakaomsaidia maishani mwake.

5. Taifa lilirahisisha watoto wote kusoma ilipochukua uamuzi wa kuanzisha mradi wa elimu kwa wote ambapo kila mtoto anapelekwa shuleni akaendelea na masomo yake mpaka anapomaliza shule za sekondari bila malipo yoyote.

6. Viongozi na walimu hutakiwa kuwapatia watoto maadili mema, kuwaelimisha na kuwasaidia katika urekebishaji wa mienendo mibaya.

7. «Mtoto hutazama kisogo cha mama yake». Msemo huu humaanisha kuwa mzazi ni mfano unaoigwa na mtoto wake. Kwa hiyo, mzazi akiwa na tabia nzuri mtoto naye bila shaka ataathiriwa vizuri na itakuwa kinyume kama mzazi ana tabia zisizopendeza. Kwa maneno mengine watoto huiga tabia za wazazi wao.

8. Mtu haulizwi kitu asichokuwa nacho. Tabia ambayo unayo ndiyo utakayoonyesha watakaokutembelea huwezi kuonyesha tabia nyingine ambayo hauna. Mtu ambaye anafanya kazi yake vizuri hupata zawadi yake na matukio mema kutokana na namna alivyofanya kazi yake. Ukitaka kufanikiwa lazima ujishughulishe. Watu wenye tabia mbaya huzaa mtoto mwenye tabia mbaya pia. Ukifuata mtu mwenye tabia mbaya bila shaka utakuwa na tabia mbaya na ukifuata mtu mwenye tabia nzuri bila shaka utakuwa na tabia nzuri.

9. Watu wengine ambao huweza kuwaathiri vizuri au vibaya watoto ni viongozi wa shule, walimu, ndugu, watumishi wa nyumbani, majirani na wengine ambao hukutana nao.

10. Masomo kutoka mjadala ni haya yafuatayo: kulinda watoto kutumia dawa za kulevya, kuwapeleka watoto shuleni na kufuatilia masomo na mienendo yao kokote wanakoenda, kushirikiana na viongozi wa shule pamoja na walimu katika kuendeleza malezi ya watoto na ninaelewa kwamba kila mtu anaweza kumwathiri mtoto vizuri au vibaya.

### 13.4.2. Msamiati kuhusu Andalio la Mjadala

**Zoezi la 2:** *(ukurasa wa 138)*

**Zoezi hili ni la binafsi, mwalimu awaombe wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia msamiati waliopewa katika sentensi yenye maana. Baada ya hayo waongoze wanafunzi kufanya masahihisho ya maswali waliyoyafanya. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kama hizi:**

1. Kila mwanafunzi katika kundi lake alitoa mchango wake kwa kujibu maswali mbalimbali.

2. Katika maisha ya kila siku elimu ni kitu muhimu sana.

3. Vijana ambao hutumia dawa za kulevya huaribu maisha yao.

4. Sehemu ya nyuma ya kichwa huitwa kisogo.

5. Wazazi wana wajibu wa kulea watoto kwa kuwafundisha maadili mema.

6. Kiongozi wa shule aliwakaribisha wanafunzi alipofika shuleni.

7. Miongoni mwa wahusika wa mjadala kuna kiongozi ambaye kazi yake ni kuongoza washiriki.

8. Tabia ya uzinzi ni ya kupigwa marufuku katika jamii ya Wanyarwanda.

9. Ulevi huwafanya watu wawe masikini.

10. Mitihani ya serikali hutayarishiwa wanafunzi kila mwisho wa mwaka.

**Zoezi la 3:** *(ukurasa wa 138)*

**Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, mwalimu awaombe wanafunzi kuambatanisha maneno yaliyoko katika orodha A na maelezo yaliyo katika orodha B. Mwalimu atathmini kazi walizozifanya wanafunzi katika makundi.**

1) k

2) a

3) f

4) j

5) g

6) i

7) b

8) h

9) d

10) c

11) e

### 13.4.3. Sarufi: Matumizi ya Hali ya Kushurutisha kwa Vitenzi

**Zoezi la 4:** *(ukurasa wa 139)*

**Wanafunzi katika makundi yao, wajadili hali ya sentensi walizopewa katika kitabu cha mwanafunzi wakisaidiwa na mwalimu. Mwalimu arekebishe makosa ya kisarufi wanapowasilisha.**

**Wanafunzi wanaweza kutoa majibu wakisema:**

Sentensi ya 1 na ya 4 zinaonyesha hali ya kuomba wingi; wakati sentensi ya 2 na ya 4 huonyesha hali ya kuomba umoja.

**Zoezi la 5:** *(ukurasa wa 140)*

Zoezi hili ni la mwanafunzi binafsi. Mwalimu awape wanafunzi wakati wa kutosha wa kubadilisha sentensi hizi kutoka hali ya umoja hadi hali ya wingi. Mwalimu arekebishe makosa ya kisarufi. Sentensi zinaweza kugeuzwa ifuatavyo:

1. Sahauni mliyoyaona yaliyowahuzunisha.

2. Boresheni maisha ya wanaoishi duniani.

3. Taarifuni wenzenu wasiohudhuria masomo ya leo.

4. Ruhusuni wanafunzi wale waende zao.

5. Tungeni vifungu vyenye maelezo kamili.

**Zoezi la 6:***(ukurasa wa 140)*

**Kila mwanafunzi binafsi aweke sentenzi hizi katika hali kanushi. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo maalumu na asahihishe makosa yanayojitokeza katika majibu yao.Majibu pendekezo ni kama haya:**

1. Usisome kitabu vizuri/Msisome kitabu vizuri.

2. Usikimbize Simba asimshambulie mtoto/ Msikimbize Simba asimshambulie mtoto.

3. Msiendelee na utafiti kuhusu maendeleo/Usiendelee na utafiti kuhusu maendeleo.

4. Usipende anayekupenda tu.

5. Msichanje watoto wachanga/Usichanje watoto wachanga.

6. Usiwasili haraka kwenye majadiliano/Msiwasili haraka kwenye majadiliano.

7. Usijaribu kueleza mawazo yako waziwazi.

8. Usijibu maswali yote unayoulizwa kwenye mjadala.

9. Usisamehe wanaosababisha kutopata ushindi wa kujinyakulia kombe/Msisamehe wanaosababisha kutopata ushindi wa kujinyakulia kombe.

10. Usifikiri takribani mara mbili kabla ya kutoa hoja yako.

### 13.4.4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 7:** *(ukurasa wa 141)*

**Zoezi hili lifanyiwe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Wanafunzi wasome maelezo kuhusu mjadala kisha wajibu maswali yaliyopendekezwa. Mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma maelezo yaliyomo vitabuni mwao. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi alisoma maelezo yenyewe. Mwalimu asasihishe majibu yao.**

**Majibu pendekezo:**

1. Mjadala ni mazugumzo ambayo yanaweza kufanyika katika makundi madogo au makubwa juu ya jambo fulani maalumu na ambayo yanaweza kuongozwa na mtu mmoja au watu wawili ambao wanazusha mawazo na kuhakikisha ikiwa kuna mwenendo mwema kati ya washiriki wa mazungumzo hayo.

2. Wanaoshiriki katika mjadala ni kiongozi wa mjadala, yeye anatoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa katika mjadala. Washiriki (hadhira) ambao hutoa hoja zao , wanaweza kuunga mkono maoni ya wenzao au kuyapinga kwa minajili ya kutoa michango yao ya kutatua tatizo linalojadiliwa.

3. Mambo ya kuzingatia katika uandalizi wa mjadala:

- Kutumia vizuri muda uliopangwa: lazima kutumia muda vizuri kwa sababu kila mtu anaruhusiwa kutoa hoja yake.
- Kuepuka fujo na kelele: kelele huwafanya watu waliohudhuria mawasiliaono wasielewane ipasavyo.
- Kupaza sauti unapotoa hoja kuhusu mada: anayezungumza anatakiwa kupaza sauti ili asikike na kila mtu aliyehudhuria. Hoja anazotoa huhitajika na kila mshiriki.
- Kutoa maoni kwa madhumuni ya kutimiza lengo la mjadala: katika mjadala, kila mshiriki anahitajiwa kutoa maoni yatakayoangazia wengine kutoa maoni yao.
- Kutumia lugha isiyo ya matusi: matumizi mazuri ya lugha huwa njia mojawapo wa kuheshimia katika majadiliano. Lugha ya matusi hukasilisha wana0taka kutoa hoja zao.
- Kuwaheshimu wengine: heshima ni kitu muhimu katika maisha ya kila mtu, katika mjadala lazima kuheshimiana na kusaidiana ipasavyo ili wawe na mwenendo sawa.
- Kupanga mawazo yako kabla ya kupata fursa: ni lazima kupanga mawazo kabla ya kupewa fursa ya kuzungumza ili utumie muda ipasavyo na lugha inayoeleweka.

**Zoezi la 8:** *(ukurasa wa 142)*

**Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi wanne wanne na awaombe kutafuta katika mjadala maneno yenye maana sawa na maneno yaliyopendekezwa. Mwalimu atathmini kazi zao katika makundi.**

1. kudanganya/**kukumba**

2. tia doa au dosari/**kuathiri**

3. wasaa/**fursa**

4. sharti/**wajibu**

5. muadhamu/**mheshimiwa**

6. mvyele/**mzazi**

7. dola/**serikali**

8. mazungumzo juu ya jambo maalumu/**mjadala**

9. utaratibu wa kufanya jambo kwa hatua ili kufikia lengo linalokusudiwa/mpango

10. funzo/**malezi**

11. mtu aliye hodari wa kusema/**msemaji**

**Zoezi la 9:***(ukurasa wa 142)*

**Mwanafunzi afanye zoezi hili binafsi, mwalimu awaongoze na arekebishe penye makosa.**

1. mtoto

2. kiongozi

3. mlezi

4. jirani

5. ndugu

6. mkurugenzi

7. shule

8. katibu

9. tabia

### 13.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10:***(ukurasa wa 143)*

**Zoezi hili ni la makundi. Wanafunzi wachague mada katika makundi yao kisha wawasilishe waliyoyazungumzia.Mwalimu ahakikishe kwamba mwanafunzi kutoka kila kikundi anawasilisha hoja zake mbele ya darasa huku akirekebisha penye makosa.**

1. Dawa za kienyeji zinasaidiaje katika uboreshaji wa afya nchini Rwanda?

2. Faida au hasara za kuishi katika miji mikubwa.

3. Mafanikio ya elimu ya wasichana kwa kulinganisha na nyakati zilizopitia nchi mwetu.

### 13.4.6. Utungaji

**Zoezi la 11:** *(ukurasa wa 141)*

**Zoezi hili lifanywe na kila mwanafunzi binafsi. Wanafunzi waandike kifungu kwa kufuata kanuni walizopewa katika kitabu cha mwanafunzi na baadaye mwalimu awaongoze na arekebishe kazi zao.**

Ulisikia kuwa kila kukicha taifa letu linashuhudia ongezeko la idadi ya watoto wanaozurura na kuishi mitaani. Andika kifungu chenye aya sita ukitoa maoni yako kuhusu namna serikali na taifa zima linavyoweza kuwasaidia watoto hao.

## 13.5. Muhtasari wa Mada

Mada hii ya nne **"Ukuzaji wa Matumizi ya Lugha Kimazungumzo"** ina masomo makuu manne yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo kama vile: kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, maelezo muhimu, kusikiliza na kuzungumza na utungaji. **Somo la 10** linaeleza maana ya mdahalo, umuhimu wake kwa wanafunzi, tabia zinazotarajiwa kwa washiriki wa mdahalo na matumizi ya vitenzi katika hali shurutishi. **Somo la 11** linaeleza namna ya kuandaa mdahalo, utekelezaji wake na matumizi ya vitenzi vyenye silabi moja. **Somo la 12** linaeleza maana ya mjadala na umuhimu wa mjadala. **Somo la 13** linaeleza namna ya kuandaa mjadala, tofauti kati ya mdahalo na mjadala na uhusiano wake pamoja na matumizi ya vitenzi vya kigeni katika hali shurutishi.

## 13.6. Maelezo ya Ziada

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mwalimu. Sehemu hii inamsaidia mwalimu kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada.

## 13.7. Tathmini ya Mada ya Nne

### A. 1. Uhusiano kati ya mjadala na mdahalo

- Mjadala na mdahalo huhusisha watu wengi wanaojadiliana kuhusu jambo fulani.
- Katika mjadala na mdahalo kuna mada ambayo hutolewa mawazo, na mada hiyo ndiyo ambayo inamulikia mjadala na mdahalo.
- Katika mdahalo na mjadala kuna kiongozi ambaye kazi yake ni kuwasaidia wasemaji kutokiuka mada.
- Mdahalo na mjadala huwa na malengo sawa ya:
- Kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa mjadala na mdahalo,

- Kukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani,
- Kumwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari,
- Kumwezesha mtu kutambua kipaji alicho nacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira,
- Kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha,
- Kumzoeza mtu kusikiliza na kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine,
- Kuwapa watu wasaa wa kuelewana na wengine kutoka maeneo mbalimbali.

**2. Tofauti kati ya mdahalo na mjadala ni hizi zifuatazo:**

- - Tofauti ya kwanza kati ya mdahalo na mjadala ni wahusika. Katika mdahalo kuna mwenyekiti, katibu, wasemaji wakuu wa upande wa utetetezi na upinzani na hadhira lakini kwenye mjadalo kuna kiongozi na hadhira tu,
- - Katika mdahalo kuna wasemaji wakuu wanaotetea au wasiokubaliana na mada lakini kwenye mjadala kila yeyote anayetaka kutoa hoja anaruhusiwa na kiongozi,
- - Kwenye mdahalo kuna pande mbili yaani upande wa utetezi na wa upinzani lakini kwenye mjadala hakuna makundi ya utetezi na upinzani,
- - Mdahalo ni mashindano na mwishoni mwake washindi hupigiwa makofi lakini kwenye mjadala hakuna washindi; kiongozi wa mjadala anatoa suluhisho kutokana na mawazo yaliyotolewa wakati mjadala si mashindano.

**3. Mambo ya kuzingatia katika utekelezaji wa mjadala ni haya yafuatayo:**

- Kutumia vizuri muda uliopangwa,
- Kuepuka fujo na kelele,
- Kupaza sauti unapotoa maoni kuhusu mada,
- Kutoa maoni kwa madhumuni ya kutimiza lengo la mjadala,
- Kutumia lugha isiyo ya matusi,
- Kuwaheshimu wengine,
- Kupanga mawazo yako kabla ya kupata fursa,

**4. Mambo ya kuepuka katika mdahalo ni kama haya yafuatayo:**

- Kupiga kelele,
- Kusababisha fujo,
- Kupoteza muda kwa bure,
- Kutumia lugha yenye matusi,
- Kutoheshimu wenzako,
- Kukejeli amri kutoka kwa mwenyekiti

**B. Wanafunzi wachague mada moja, kisha waandae mdahalo wakisaidiwa na mwalimu. Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi anafanya mdahalo wake mwenyewe na baadaye wawasilishe mbele ya darasa.**

1. Wakoloni walileta mabaya mengi kuliko mazuri.

2. Shule za mabweni ni bora kuliko shule za kutwa.

3. Uzuri wa mtu si urembo bali ni tabia.

4. Kutoa si utajiri bali ni moyo.

**C. Katika makundi yao ya kawaida, wanafunzi wachague mada moja, kisha waandae mjadala wakisaidiwa na mwalimu. Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi anashiriki katika mjadala na anaonyesha kipaji chake katika kutoa hoja.**

1. Manufaa ya michezo kwa mtu binafsi na kwa taifa

2. Madhara na matatizo ya kutumia dawa za kulevya na kushiriki ulevi.

**D. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kutunga kifungu kifupi cha habari wakitumia vitenzi tofauti katika hali ya kushurutisha umoja na wingi. Mwalimu asahihishe vifungu vya wanafunzi huku akisisitizia kwenye matumizi bora ya sarufi.**

**Mazoezi ya Ziada**

### 13.8.1. Mazoezi ya Urekebishaji

*(ukurasa wa 140)*

1.Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo: **uvivu, kutetea,madhara, mwenyekiti, kulevya**

a.Dawa za ……**kulevya**……… huangamiza maisha ya binadamu na nchi kwa

ujumla.

b.Ulevi una……**madhara**….. kwa kazi tunazofanya kwa kuendeleza nchi zetu.

c.Matokeo ya ulevi ni……**uvivu**…., kufukuzwa kazini, uzinifu, ukatili na mengineyo.

d.Mdahalo huhusika na……**kutetea**……. au kupinga fikra za watu kulingana na mada inayohusika.

e.Mjadala unahusu mawasiliano kati ya watu juu ya mada fulani bila kuzingatia uchaguzi wa ……**mwenyekiti**…….na katibu.

### 12.8.2 Mazoezi Jumuishi

Fanya maandalizi ya mdahalo kwa kutoa mambo yanayoweza kuzingatiwa kuhusu mada hii :

- Kilimo bila mbolea ni kasoro kwa maendeleo ya jamii.
- Elimu bora ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya taifa.

### 12.8.3. Mazoezi ya Nyongeza

Fanya kazi zifuatazo kuhusu mdahalo

a)Andaa mdahalo kuhusu moja ya mada zifuatazo:

- Ufugaji ni bora kuliko kilimo katika maendeleo ya jamii.
- Maendeleo ya jamii huchochewa na elimu bila ubaguzi.

# MADA KUU YA TANO: UTUNGAJI

5

## MADA NDOGO: INSHA ZA MASIMULIZI AU ZA KUBUNI

## Uwezo Upatikanao katika Mada

Kumwezesha mwanafunzi kuzingatia mwongozo wa kutunga insha za masimulizi kulingana na mada iliyotolewa na kuzitolea muhtasari darasani kwa njia ya mazungumzo; kuelewa jinsi ya kumnukuu mtu mwingine.

### Ujuzi wa Awali

Katika kidato cha tatu, mada kuu ya nne ilizungumzia "Uimarishaji wa stadi ya uandishi na masimulizi kupitia lugha ya Kiswahili". Mojawapo wa stadi zilizotarajiwa kwa wanafunzi kulikuwa na stadi ya kutunga insha fulani kulingana na kichwa au mada iliyotolewa.

Wanafunzi hawa walifundishwa sifa za aya na namna ya kuandika aya nzuri. Pia, walifundishwa kufanya uchambuzi wa insha iliyotungwa wakibainisha mambo makuu yanayojitokeza katika insha hiyo na kisha kutoa maoni yake kuhusu mada au swala linalojadiliwa katika insha.

Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha, kuandika, kuzungumza na katika mazoezi au kazi na sarufi; mwalimu anawaongoza wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia maswala mtambuka yafuatayo:

### 1. Mafunzo kuhusu Amani na Maadili Mema

a. Wanafunzi wanapotunga vifungu lazima kuingiza masomo ya kuwashauri kuishi kwa amani.

b. Kwa kutunga sentensi, mwalimu awaongoze kutunga sentensi zenye mafunzo yanayohusu amani na maadili mema.

### 2. Mila na Desturi na Kuzalisha kwa Viwango

Kwa kufanya kazi yoyote,  kama kuandika inafaa kuchunguza kama unafuata taratibu za kuandika.

### 3. Elimu Jumuishi

Wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu, wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza, na kadhalika.

Kumbuka kuwa wanafunzi wenye matatizo kama haya ni kama wengine; walikuja shuleni ili wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima wewe mwalimu uwasaidie ipasavyo.

### 4. Elimu kuhusu Afya ya Uzazi

Katika vifungu au katika mifano ya sentensi, mwalimu kwa kutumia lugha anawasaidia wanafunzi kuelewa matumizi ya kondomu na sababu za kuitumia kama kujikinga ukimwi na kuzaa watoto ambao una uwezo  wa kutimiza huduma zote kwao.

### 5. Mazingira na Maendeleo Endelevu

Mwalimu kupitia mazoezi ya msamiati na sarufi, anaweza kueleza umuhimu wa kuifadhi mazingira kwa maisha ya watu.

### 6. Usawa wa Jinsia

a. Mwalimu katika mifano yote, ni lazima kutoa mifano inayoonesha usawa wa jinsia;

b. Katika mazoezi ya kutunga sentensi, ni vizuri kutunga sentensi ambazo zinaeleza na zinatoa maelezo kuhusu usawa wa jinsia;

c. Kazi katika makundi, ni vizuri kupanga wasichana na wavulana katika kundi moja ili darasani pasiwe na kundi la jinsia moja.

### Mwongozo kuhusu Zoezi la Utangulizi wa Mada

- Kwa kutangulia mada, mwalimu atauliza maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua kuhusu mada hii;
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia masomo tofauti, mazoezi, vifungu, na kazi nyingine zilizotaarishwa kwenye mada hii.

## Orodha ya Masomo na Tathmini

| Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| 1. Maana ya insha | Maarifa na ufahamu: kueleza maana ya insha za kubuni au za masimulizi na kueleza usemi wa asili.<br><br>Stadi: kusoma insha mbalimbali za masimulizi kutoka vitabu tofauti na kuzifanyia mhadhara darasani.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kufuata maadili mema ya kuwa na adabu, usafi, kupigana na wivu, uvivu, ukatili, uzinifu, ulevi, ujinga, umasikini. | 7 |
| 2. Aina za insha | Maarifa na ufahamu: kutofautisha aina za insha mbalimbali na kueleza usemi wa taarifa.<br><br>Stadi: kutayarisha na kutoa muhtasari wa insha bila kupotosha ukweli wa mwandishi.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kujivunia nchi yake. | 7 |
| 3. Insha za masimulizi | Maarifa na ufahamu: kukumbuka sehemu za kuzingatia katika utungaji wa insha na kubainisha mabadiliko yaliyopo toka usemi wa asili kwenda usemi wa taarifa.<br><br>Stadi: kutunga insha ya masimulizi kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kuridhika na kazi ya ubunaji katika maisha yake. | 8 |
| Tathmini ya mada | | 2 |
| Vipindi vyote vya mada ya 5 | | 24 |

# SOMO LA 14: MAANA YA INSHA

## 14.1. Utangulizi/Marudio

Somo hili linajishughulisha na «Maana ya insha». Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu mdahalo kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

## 14.2. Vifaa vya kujifunzia

Ili Mwalimu aweze kufanikisha somo lake na kukidhi malengo ya somo lake, mwalimu atatafuta vifaa vya ufundishaji ambavyo vitamsaidia ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo lake. Mwalimu atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Michoro au picha za maeneo mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule na upatikanaji wa vifaa mbalimbali. Wakati mwalimu hatakuwa na vifaa vyovyote kutokana na sababu mbalimbali shuleni kwake, ajibunie yeye mwenyewe vifaa ambavyo vitamsadia kufanikisha somo lake.

## 14.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufikia malengo ya somo lake. Mbinu hizoni hizi zifuatazo:

- **Kazi katika makundi ya wanafunzi:** Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, watatu watatu au wane wanne. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kuzunguka darasani kuangalia na kutoa mchango wake inapohitajikwa. Uzingatizi wa jinsia katika uundaji wa makundi ni kitu muhimu sana. Kazi katika makundi itilie mkazo kwa kusaidia wanafunzi kushirikiana na wenzao katika ujifunzaji wao.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali yeye binafsi. (Asome kifungu cha habari mwenyewe au afanye zoezi mwenyewe).

- **Maswali na majibu:** Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzake iwezekanavyo. Mwalimu ajaribu kuweka maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati wanafunzi na wanafunzi wake. Mwalimu awasaidie wanafunzi kujibu maswali ambayo wanafunzi wote wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali na wao wamjibu, na vile vile wanafunzi wamuulize mwalimu na wanafunzi wengine majibu, mwishoni mwalimu naye atoe majibu sahihi kwa kuwakosoa.

- **Maelezo ya mwalimu:** Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake, kisha atambuwe ujuzi unaohitaji maelezo yake binafsi. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee vya kutosha wanafunzi wake somo kwa kutilia mkazo kwenye kasoro alizozitambua. Majadiliano kati ya wanafunzi itakuwa njia bora katika ufundishaji. Mwalimu awapatie fursa ya kujailiana kati yao.

## 14.4 MAJIBU

**Zoezi la 1:** (ukurasa wa 147)

**Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuunda makundi ya wanafunzi wawili wawili. Wanafunzi wajibu maswali yapatikanayo katika kitabu cha wanafunzi na mwalimu awachangamshe kidogo hivi akielekeza maswali yake kwenye somo jipya. Baadaye, mwalimu awaambie wanafunzi waendelee kujibu maswali.**

### 14.41. Maswali ya Ufahamu

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi wasome kifungu walichopewa kisha wajibu maswali husika. Ikiwa wanahitaji msaada mwalimu awasaidie.**

**Majibu yanayopendekezwa:**

1.Tarakilishi ni chombo cha kiteknolojia chenye uwezo wa kupokea na kukusanya taarifa, na halafu kuzishughulikia kulingana na matarajio ya wanaoitumia.Katika insha kuhusu tarakilishi wanatuelezea kwamba chombo hiki kina uwezo wa kutoa matokeo ya kazi na kuelezea kuhusu namna kazi hiyo ilivyoendeshwa au jinsi kitu kilichofanyika. Tarakilishi ina uwezo wa kufanya mambo mengi muhimu kwa muda mfupi na kwa uhakika.

2.Tarakilishi huchukuliwa kama rafiki katika jamii ya leo kwa sababu kifaa hiki huwa

karibu naye katika maandalizi na utekelezaji wa kila jambo analotaka kutenda maishani mwake.

3.Mifano inayoonyesha jinsi tarakilishi hutumia muda mfupi kwa kufanya kazi ni kama vile:

a.Watu wanapofanya hesabu ngumu na takwimu changamani hupata matokeo au majibu kwa muda mfupi sana kuliko wanapotumia vifaa vingine.

b.Mtumiaji wa tarakilishi anapofanya makosa wakati wa matumizi yake katika kazi fulani, usahihishaji huwa rahisi kama maandalizi yake yalifanyiwa kwa tarakilishi na kuhifadhiwa vizuri.

4.Ndiyo, tarakilishi ina  mchango mkubwa katika uboreshaji wa afya ya watu kwa sababu chombo hiki humwezesha binadamu kufanikisha kazi zake katika nyanja mbalimbali za maisha yake kama vile uwanja wa elimu, udaktari, uchapishaji wa vitabu, kilimo, ufugaji, urubani, biashara, unahodha, utafiti na kadhalika.

5.Tarakilishi katika mawasiliano hutumiwa sana kuwasiliana na watu mbalimbali kwa mfano rubani wakati anaendesha ndege huwasiliana na wasafiri au wafanyakazi wengine wanaomwelekeza sehemu za kupitia kwa kutumia chombo hiki. Wafanyakazi wenzake ili kumjulisha hali ya hewa na mambo mengine muhimu yanayohitajika hutumia chombo hiki. Kitu kingine maishani mwetu, tunapotaka kujua habari za marafiki ambao wako mbali tunakitumia chombo hiki na wakati huu mtandao utakuwa sharti ili kufanikisha kuzipokea au kuzituma habari.

6.Kisanduku cheusi hiki husaidia kupokea na kuhifadhi taarifa zote zinazohusiana na safari ya ndege kiasi kwamba jambo fulani kama vile ajali au maafa yakitokea, wachunguzi na watafiti wakitumie chombo hiki kujua sababu za ajali iliyotokea.

7.Mifano ya kazi ambazo hufanywa na tarakiliishi.

a.Tarakilishi husaidia kiasi katika utafiti;

b.Tarakilishi husaidia madaktari kuchunguza hali ya wagonjwa kama vile kumwelekeza kwenye sehemu inayo shida, tena huwasaidia katika upasuaji wanapotaka kumtibu mgonjwa;

c.Tarakilishi husaidia sana katika mawasiliano kati ya watu kwa kupashana habari;

d.Tarakilishi husaidia kuandika na kuhifadhi matokeo ya  utafiti fulani;

e.Tarakilishi husaidia kulinda usalama wa ndege angani au meli baharini kwa kupokea au kutuma habari mahsusi;

f.Tarakilishi husaidia sana katika upande wa teknolojia mpya ya kuendeleza mataifa mbalimbali;

g.Tarakilishi husaidia katika uvumbuzi wowote unaohitaji uchunguzi kama vile kutafuta takwimu na huwapa mchango mkubwa wa kusahihisha makosa yanayoweza kujitokeza.

8.Kwa maoni yangu tarakilishi ni muhimu sana maishani mwetu kwa sababu zifuatazo:

a.Tunapoitumia tarakilishi tunapata maarifa muhimu yahusuyo masomo tunayoyasoma;

b.Tarakilishi ni chombo muhimu kwa wanafunzi kwani hutuzowesha jinsi tunavyoweza kufanya utafiti kwa urahisi;

c.Tarakilishi ni chombo kinachowasaidia wanafunzi kupumzika wakati wanasikia uchovu fulani;

d.Tarakilishi ina michezo, miziki na filamu ya kuwapumzisha na kuwafanya wanafunzi wasizururu zururu;

e.Tarakilishi huweza kuendeleza masomo ya wanafunzi kwa kuwajulisha nchi ambazo wanaweza kuendeleza masomo yao kwa urahisi na kupokea misaada ya masomo.

### 14.4. 2. Msamiati

**Zoezi la 2:** (ukurasa wa 149)

**Mwanafunzi afanye zoezi binafsi. Mwalimu amwelekeze mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno aliyoyapewa. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wote waandike sentensi walizotunga ubaoni na washirikiane kusahihisha makosa ya kimaana, kimsamiati na kimaandishi. Ikiwa msaada unahitajika mwalimu awasaidie.**

**Sentensi zinazopendekezwa ni kama hizi zifuatazo:**

1.Baba yangu alinielezea kwamba umoja wa wananchi ni nguzo 2.muhimu sana katika ujenzi wa nchi kimaendeleo.

Sentensi:

a.Uandishi wa insha hulazimisha mwandishi kutoa hoja zake kimantiki ili kumshawishi hadhira.

b.Tunapotoa fikra zetu wakati wa majadiliano, ni lazima kuangazia mantiki kwa madhumuni ya kuridhisha hadhira tunayo.

**3.Intaneti** ni njia mojawapo ya kuwahusisha watu wanaoishi mbali au karibu kwa kuwaweka karibu na kuwashirikisha katika mawasiliano kwa urahisi.

4.**Huduma** za utabibu leo hii ni ghali sana kiasi kwamba watu wasio na bima ya matibabu hushindwa kugharamia..

5.Mwanafunzi anapomudu matumizi ya tarakilishi hufanikisha masomo yake kwa urahisi.

6.Ufugaji na kilimo ni nguzo muhimu sana katika maendeleo ya jamii anamoishi.

7.Atakayeonyesha hamu kubwa ya kujiendeleza ni jukumu ya taifa kumchochea ili naye atoe mchango wake katika ujenzi wa taifa lake.

8.**Uchapishaji** wa vitabu ni kazi inayohitaji muda wa kutosha na fedha nyingi.

**Zoezi la 3:** (ukurasa wa 149)

**Zoezi hili ni la kibinafsi, kila mwanafunzi afanye zoezi yeye binafsi kukamilisha sentensi ili ziwe na maana sahihi kwa kutumia maneno aliyoyapewa katika kitabu cha mwanafunzi. Mwalimu achunguze kuhakikisha kwamba kazi iko inafanyika vyema. Mwalimu awaombe wanafunzi kuwasilisha matokeo ya zoezi kisha asahihishe makosa yatakayojitokeza.**

Majibu yanayopendekezwa:

Tarakilishi

nguzo

utabibu

mantiki

Urubani, unahodha

kuhifadhi

huchochea

hitilafu

mishipa

Ufugaji

**Zoezi la 4:** (ukurasa wa 150)

**Zoezi hili lifanyike katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Mwalimu awaombe wanafunzi kuhusisha maneno ya sehemu A na maana zake katika sehemu B. Mwalimu asahihishe makosa yatakayojitokeza kuhusu matumizi ya lugha.**

b.

g.

f.

h.

e.

c.

a.

d.

### 14.4.3. Sarufi: Matumizi ya Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa

**Zoezi la 5:** (ukurasa wa 151)

Wanafunzi wasome maelezo waliyopewa wakiwa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kisha wajadiliane kuhusu alama zinazohitajika kutumiwa katika sentensi zinazopatikana katika kitabu cha mwanafunzi na baadaye wawasilishe matokeo ya majadiliano kati yao kuhusu alama hizo.

**Majibu pendekezo:**

1.“Ninakwenda nyumbani.” Alisema mwanafunzi.

2.“Huyu ni ng’ombe mnene kabisa” Muhire alisema kwa mshangao.

3.“Utatoka hapa saa ngapi?” Baba aliniuliza.

4.“Ninampenda sana Mungu” Maombi anaeleza.

5.“Rafiki wangu ana ulemavu wa mguu” Kampire alituambia.

**Zoezi la 6:** (ukurasa wa 150)

**Katika kundi la wanafunzi wanne wanne, mwalimu awaombe wanafunzi kuunda sentensi sahihi kwa kuiga sentensi hapo juu kwa kutumia usemi**

**halisi. Mwalimu awaombe wanafunzi kuwasilisha matokeo ya makundi na kusahihisha makosa ya kisarufi na kimsamiati. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye shida yoyote na wenye ulemavu.**

**Mfano:** "Leta kitabu hicho hapa mbele" Mwalimu alisema.

### 14.4.4. Matumizi yaLugha: Maana ya Insha na Sifa zake

**Zoezi la 7:** (ukurasa wa 152)

**Wanafunzi wasome maelezo muhimu katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kuhusu maana ya insha, kisha wajadiliane kuhusu maswali yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi na baadaye wawasilishe majadiliano yao wakisaidiwa na mwalimu.**

**Majibu pendekezo:**

1.Insha ni mtungo wa kinathari unaozungumzia suala au kusimulia kisa fulani.

2.Insha nzuri inapaswa kuzingatia sifa zifuatazo:

a.Insha nzuri inapaswa kuwa sahihi kisarufi;

b.Lazima suala linalozungumziwa au yaliyomo katika insha yahusishwe na kichwa cha insha;

c.Insha inapaswa kuepuka utata. Yaani kuwepo kwa maana nyingi. Pasiwepo na kauli au sentensi ambazo hazionyeshi uhusiano wazi na sentensi nyingine;

d.Lazima insha iwe na utangulizi mzuri unaojitokeza wazi pamoja na mwisho ambao unadhihirika waziwazi;

e.Insha inapaswa kuwa na urefu wa kutosha. Isiwe ndefu sana na fupi kupita kiasi;

f.Insha haipaswi kuwa mkusanyo wa nukuu au maneno ya waandishi wengine isipokuwa pale ambapo mwandishi ameweka wazi kuwa anatumia maneno ya wengine;

g.Mwisho, insha ni sharti iwe na mvuto yaani uwezo wa kumvutia msomaji.

3.Insha yoyote huwa na muundo. Muundo huo huwa:

a.**Kichwa:** Hii ndiyo mada ya insha au kinachozungumziwa. Kichwa hakipaswi kuwa na maneno mengi.

b.**Utangulizi:** Sehemu hii hutanguliza insha. Sehemu hii huwa na aya moja ambayo haina mistari mingi (labda minne). Hupaswa kuwa na mvuto kwa msomaji na

kutoa mwelekezo wa insha yenyewe.

c.**Mwili au sehemu kuu**: Hii huwa ndiyo hasa insha yenyewe. Mwili wa insha huundwa na aya zinazoendeleza mada ya insha. Kila aya lazima ichangie katika kuliendeleza wazo kuu. Ni vyema kuhakikisha kuwa pana muungano ulio wazi kutoka aya moja hadi nyingine.

d.**Hitimisho:** Ni sehemu ya mwisho wa insha. Katika sehemu hii mwandishi hurudilia kwa ufupi yale aliyoyaelezea katika insha yenyewe.

4.Ni katika kiini au mwili wa insha ambapo mwandishi hulifafanua kwa mapana swali linaloshughulikiwa kwa kutoa mifano mwafaka na inayoendana na hali halisi.

**Zoezi la 8:**(ukurasa wa 151)

**Zoezi hili lifanyike katika makundi ya wanafunzi watano watano. Wanafunzi wajadiliane kuhusu mada walizopewa na kila kundi liwasilishe kazi yao. Mwalimu arekebishe makosa ya kimazungumzo yatakayojitokeza. Mwalimu ahakikishe kwamba amewashirikisha wanfunzi wote.**

**Mada ni hizi zifuatazo:**

**1. Utawala Bora**

Mambo haya yazingatiwe katika utungaji:

- Kupigania uhuru wa wananchi,
- Kuimarisha umoja wa wananchi,
- Kuchochea na kuendeleza uchumi wa wananchi,
- Kuimarisha maisha bora ya wananchi,
- Kupendekeza maandalizi ya miradi mbalimbali ya kiuchumi na utekelezaji wa miradi husika kwa kukidhi maendeleo ya jamii.

**2. Umoja wa Jamii**

Mambo yafuatayo yazingatiwe katika utungaji:

- Kuimarisha ushirikiano mwema kati ya wananchi,
- Kuelimisha jamii husika,
- Kuimarisha utawala bora,
- Kuchochea mawasiliano mema kati ya jamii,

- Kushirikiana katika utatuzi wa matata yanayojitokeza katika jamii husika,
- Kuunda mashirika ya kiuchumi,
- Kuheshimu haki za binadamu,
- Kufikiria na kuheshimu muktadha wa kijinsia,
- Kudumisha amani na usalama katika jamii,
- Kupiga marufuku umaskini na ubaguzi wowote, na kadhalika.

### 3. Afya ya Watoto

Mambo yafuatayo yazingatiwe katika utungaji kuhusu mada hii:

- Mtoto hupaswa kutunzwa kiafya, kijamii,
- Kufuatilia mwenendo mwema wa mtoto popote apo,
- Kumuelimisha mtoto,
- Kutetea haki za mtoto.

### 14.4. 5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 11:** (ukurasa wa 153)

**Zoezi hili lifanywe kibinafsi. Mwalimu awaombe wanafunzi kudokeza mambo yanayoweza kujitokeza wanapoombwa kufanya insha kuhusu mada hapo chini kwa kutumia usemi wa asili. Mwalimu asahihishe makosa ya kimaandishi.**

**Mada ni hizi zifuatazo:**

3.Nafasi ya Teknolojia Mpya katika Maendeleo ya Kilimo na Ufugji.

4.Umuhimu wa Kompyuta katika Biashara Mbalimbali.

5.Umuhimu wa Kompyuta katika Michezo na Burudani

### 14.4.6. Kuandika

**Zoezi la 10:** (ukurasa wa 153)

**Wanafunzi wafanye zoezi hili kwa binafsi. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kutunga insha kuhusu mada zinazopatikana katika kitabu cha mwanafunzi wakizingatia sehemu kuu za insha.Wananafunzi wakumbuke kutumia usemi wa asili katika insha watakazotunga.**

"Umoja wa Afrika ni Msingi Mhimu kwa Maendeleo ya Afrika".

**Yazingatiwe mambo haya katika utungaji:**

- Kukuza maendeleo,
- Kukuza demokrasia barani Afrika,
- Kudumisha amani na usalama barani Afrika,
- Kuzuia ueneaji wa silaha barani Afrika,
- Kukuza haki za binadamu,
- Kuimarisha ushirikiano baina ya Waafrika wote.

# SOMO LA 15: AINA ZA INSHA

## 15.1. Ujuzi wa Awali/Utangulizi

Zipo aina mbalimbali za insha ambazo huweza kuandikwa. Pana umuhimu wa kuzijua aina hizi kwa kuwa kila moja ina sifa zake, matarajio yake, mipaka yake na wasifu wake. Mwanafunzi anayetaka kuandika insha nzuri lazima azielewe sifa hizo, matarajio hayo, mipaka hiyo na wasifu huo. Kusoma somo hili si mara ya kwanza kwa wanafunzi wa kidato cha nne. Waligusia utungaji katika kidato cha pili na kidato cha tatu. Somo lililotangulia lilizungumzia zaidi maana ya insha na likatilia mkazo insha ya masimulizi.

## 15.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vifuatavyo huweza kutumiwa na mwalimu wakati wa kufundisha somo hili:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Michoro tofauti inayohusiana na somo,
- Ubao
- Karatasi manila

Mwalimu achague vifaa vingine husika kulingana na muktadha. Ajaribu kuwa mbunifu katika ufundishaji wake.

## 15.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika ufundishaji wa somo hili, mwalimu atumie mbinu zifuatazo:

- Kazi ya kibinafsi: kazi fulani lazima zifanywe na mwanafunzi akiwa pekee. Hali hii itakuwezesha kutathmini hatua ambazo kila mwanafunzi amepiga katika upatikanaji wa ujuzi na maarifa. Kazi nyingi zinazohusu kuandika au kuchora hufanywa na wanafunzi binafsi.kupitia njia hii, unaweza kuchunguza maandishi ya kila mwanafunzi au uwezo wao wa kuchora na kufasiri maneno. Pia, unaweza kupima uwezo wao wa kusoma au kutamka maneno fulani.

- Kazi za kimakundi: wanafunzi washirikishwe katika kazi za vikundi na kuwasilisha kazi zao mbele ya darasa. Mwalimu, hakikisha kuwa umepitia kazi fulani ya vikundi unapojiandaa kwa somo. Kazi hiyo ioane na ujuzi unaotarajiwa kupatikana mwishoni mwa kipindi husika na uwaelekeze wanafunzi vilivyo ili wafikie ujuzi huo.

- Mjadala: katika somo hili wanafunzi wafanye mijadala ili kukuza stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu, hakikisha kuwa umetenga muda wa kupata ripoti ya yaliyojadiliwa au kutathmini ujuzi waliotarajiwa kuupata

kwa kuwapa shughuli fulani. Hakikisha kuwa kila kikundi kimepata nafasi ya kutosha kuwasilisha ripoti zao au kutathminiwa.

- Fikiri-jozi-shiriki: Baada ya maoni tofauti kutoka kwa wanafunzi, mwalimu anapata habari juu ya ujuzi wa awali wanafunzi wake walio nao kuhusu somo hili. Mwalimu asahihishe zoezi hili pamoja na kusahihisha makosa ya kisarufi, kimsamiati na kimatamshi yaliyojitokeza.

**Zoezi la 1:** (ukurasa wa 154)

Wanafunzi wajibu maswali haya wakiongozwa na mwalimu pale ambapo itaonekana hawakuelewa namna ya kuyajibu

## 15.4. Majibu

Kusoma naUfahamu

Huu ni mwanzo wa somo lenyewe. Ni lazima wanafunzi wapewe muda wa kutosha wa kusoma matini yenyewe, kila mwanafunzi pekee yake na kwa kimya. Halafu baadhi yao wataombwa kusoma (mmoja akisoma aya moja), huku mwalimu akisahihisha makosa ya kusoma (kama ya kimatamshi) yanayojitokeza. Matumizi ya alama za uakifishaji kama alama ya hisia yazingatiwe ipaswavyo.

### 15.4.1. Maswali ya Ufahamu

Maswali ya ufahamu yajibiwe katika makundi madogo madogo ya wanafunzi. Baadhi yao wataombwa kutoa majibu, kwa mfano mwanafunzi mmoja kutoka kundi moja akatoa jibu la swali moja. Jibu la kundi likiwa si sahihi, mwalimu ataomba kundi jingine kutoa jibu sahihi.

Yafuatayo ni majibu yanayoweza kutolewa na wanafunzi:

1.Mwandishi anaisifu nchi ya Rwanda kwa sababu ya uzuri wake. Uzuri huo huonekana katika sehemu tofauti: barabara safi, majengo safi na mazingira ya kuvutia.

2.Serikali ya Rwanda imetilia mkazo mambo ya usafi na uhifadhi wa mazingira katika nyanja tofauti za maisha ya kila siku ya raia. Hali hii ni mfano mzuri kwa nchi zote kuiga.

3.Miti hurembesha milima yetu na hutusaidia kupata upepo mwanana. Si hayo tu, baadhi ya miti huzaa chakula cha watu na wanyama, hutumiwa kutengenezea vifaa mbalimbali na husaidia ardhi kupambana na mmomonyoko.

4.Jiji la Kigali limeneemeshwa na barabara zake zilizopakwa lami, alama nyeusi pembezoni,na maua yanayoleta harufu nzuri. Miti inayopatikana mjini pote hutuletea hewa nyororo. Wakati wa usiku taa huwashwa kote.

5.Vitendo vinavyofanywa wakati wa Umuganda ni kama vile kuchimba mifereji ya maji,

kuwajengea nyumba watu wasio na uwezo, kupanda miti, kuwachimbia vyoo watu maskini, kufyeka vichaka, kufagia na kuziba vidimbwi vya maji, pamoja na kuzoataka zote ili zitupwe jalalani.

6.Kila wanapofika nchini Rwanda wageni hushauriwa kuzingatia mambo ya usafi.

7.Vitendo viwili ambavyo haviruhusiwi kulingana na desturi ya wananchi wa Rwanda ni kama kulia chakula njiani au barabarani na kuenda haja pahali pasipostahili.

8.Kutembea bila viatu huweza kuhatarisha usalama wa miguu: mtu anaweza akaumwa na wadudu kama nyoka. Pia mtu anaweza akaambukizwa na ugonjwa kwa sababu ya uchafu unaopatikana katika mazingira. Si hayo tu ; asiyevaa viatu anaweza kuumizwa na vifaa kama chupa,n.k.

9.Kipindupindu ni mojawapo ya ugonjwa unaosababishwa na uchafu.

10. Kifungu hiki kinatufundisha kwamba usafi wa mazingira ya mahali tunapoishi huchangia kuipenda nchi yetu. Kuzingatia mambo ya usafi huchangia mno kuwa na afya nzuri, na tukiwa na afya nzuri tutaifurahia na kuisifu nchi yetu Rwanda.

### 15.4.2. . Msamiati

**Zoezi la 2**:(ukurasa wa 156)

Katika zoezi hili, mwanafunzi anaombwa kutoa maana ya kila neno tu. Zoezi hili linaweza kufanywa na mwanafunzi binafsi au makundi ya wanafunzi. Bila shaka makundi tofauti yatatumia maneno tofauti kwa kutoa maana za maneno waliyopewa.

1. Fahari: jambo au kitu cha sifa cha kujivunia kwa watu.

2.Ughaibuni: nchi za mbali

3.Kuvutia: kupendeza

4. Mwanana: shwari, tulivu

5. Pembezoni: pembeni mwa; kandokando ya.

Zoezi la 3:*(ukurasa wa 156)*

Zoezi hili ni gumu kidogo kuliko lililolitangulia. Linahusu mambo mawili: kujua maana za maneno watakayotungia sentensi na kuzitunga sentensi zenyewe. Zoezi hili lifanyiwe katika makundi. Wasimamizi wa makundi watapewa fursa ya kusomea sentensi zao makundi mengine, huku mwalimu akisahihisha makosa ya kimatamshi au ya kisarufi yatakayojitokeza.

Hii ni mifano ya sentensi zinazopendekezwa:

1.Barabara zikipakwa lami zitachangia uendelezaji mwema wa biashara.

2.Pundamilia si mnyama anayefugwa kama punda.

3. Mjini Kigali kuna mabango mengi yanayozungumzia usafi.

4. Baadhi ya watu wanaohudhuria umuganda huombwa kufyeka nyasi.

5.Magubiko yasiyoharibu mazingira ndiyo yanaruhusiwa kutumiwa siku hizi nchini Rwanda.

**Zoezi la 4:**(ukurasa wa 156)

Hii nayo ni sehemu ya msamiati uliotumiwa katika kifungu cha ufahamu na ni lazima wanafunzi wajue maana za maneno waliyopewa (katika kundi B) na walinganishe maana walizopewa (katika kundi A) na matumizi yake katika kifungu. Zoezi hili lifanyiwe katika makundi chini ya uangalifu wa mwalimu.

1.→f

2.→i

3.→a

4.→j

5.→h

6.→c

7.→e

8.→g

9.→b

10.→d

### 15.4.3. Sarufi

**Zoezi la 5**:(ukurasa  wa 157)

Mwalimu achunguze kwa kuhakikisha ikiwa sentensi ya kwanza ni ya usemi halisi, na ya pili katika usemi taarifa. Hili ni zoezi linalotangulia sarufi kuhusu USEMI WA TAARIFA. Katika somo lililotangulia hili (somo la 14), wanafunzi tayari walielimishwa kuhusu usemi wa asili. Lengo la zoezi hili ni kuwasaidia wanafunzi kuona kwamba kuna mabadiliko yanayojitokeza tunapoiandika sentensi kutoka kwenye usemi asili hadi usemi taarifa. Ifuatayo ni mifano zaidi:

1. “Usalama unatiliwa mkazo kwa kuimarisha amani nchini.” Mtalii aliwaelezea wengine.

2. Mtalii aliwaelezea wengine kwamba usalama ulitiliwa mkazo kwa kuimarisha amani nchini.

**Zoezi la 6:** (ukurasa 158)

Kupitia zoezi hili, mwanafunzi tayari anaingizwa katika matumizi yenyewe ya sarufi hii. Inapendekezwa zoezi hili lifanyiwe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu: mwalimu mkuu, mzazi na mtoa taarifa ya mazungumzo yaliyokuwepo kati ya mwalimu mkuu na mzazi. Hii ni taarifa ya mazungumzo hayo:

1. Mwalimu Mkuu alimwuliza mzazi jina la mtoto wake.

2. Mzazi akajibu kwamba yeye ni babake Yohana.

3. Mwalimu Mkuu aliendelea kusema kuwa Yohana alikuwa mwanafunzi wake mzuri sana ambaye anazingatia mambo ya usafi shuleni.

4. Mzazi alikubaliana na maoni ya Mwalimu Mkuu na kuhakikisha kwamba na hata nyumbani Yohana alikuwa hivyo. Halafu akaomba nafasi ya mdogo wake Yohana katika kidato cha nne.

5. Mwalimu Mkuu akamwuliza mzazi mahali mtoto wake alipokuwa akisomea.

6. Mzazi alijibu kwamba alikuwa akisoma kwenye Shule ya Sekondari ya Rukomo.

7. Mwalimu Mkuu aliendelea kwa kumwuliza mzazi sababu ya kumhamisha kutoka huko.

8. Mzazi alijibu kwa kusema kwamba angependa [mtoto wake] asomee karibu na nyumbani kwao.

**Zoezi la 7:** (ukurasa 159)

Sentensi za usemi asili katika zoezi hili ni za mazungumzo/matumizi ya kila siku. Ni zoezi linaloweza kufanywa na wanafunzi wawili wawili. Mmoja kati yao atasomea darasa sentensi moja watakaokuwa wameiandika. Zifuatazo ni sentensi zenyewe katika usemi taarifa.

1. Mwalimu aliwaambia wanafunzi wajitayarishe kutunga insha.

2. Mwalimu alisema kwa sauti kubwa kwamba alikuwa anataka darasa hilo lisafishwe kila asubuhi.

3. Waziri wa utamaduni aliwahamasisha wanafunzi wa chuo kikuu kujivunia utamaduni wao.

4. Mkuu wa kijiji aliwaambia raia wenzake kutoa maoni yao kuhusu jambo lililokuwa linazungumziwa wakati huo.

5. Baada ya umuganda Katibu Mtendaji wa tarafa yetu alitwambia kwamba nduli huyo – kipindupindu – tutamshinda tu na kumtokomeza iwapo tutatumia kinga zote za kujiepusha na uchafu wa mazingira yetu.

6. Askari mmoja alisema kwamba hairuhusiwi kuwinda na kuwauwa wanyamapori.

7. Mtalii kutoka Uingereza alishangaa na kusema kuwa hajaona nchi safi kama Rwanda.

8. Afisa wa Uhamiaji aliwaambia watalii kuzingatia taratibu za usafi kama zilivyopangwa na serikali yetu.

9. Mwalimu mkuu aliwaambia wanafunzi hodari kwamba hali ya hewa ingekuwa nzuri wangetembelea Mbuga ya wanyama ya Akagera.

10. Meya wa wilaya aliwahamasisha raia wake kutoa mchango wao ili wajenge nchi yao.

### 15.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 8:**(ukurasa wa 159 )

Maelezo yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi kuhusu aina za insha ni mafupi. Hapa si lazima kuingilia undani kila aina kwa sababu wanafunzi wa kidato hiki ni wa mchepuo usiokuwa wa lugha. Somo la 14 limesisitizia insha za maelezo, wakati ambapo somo hili (la 15) linasisitizia insha za wasifu. Somo la 16 litazungumzia mengi kuhusu insha za masimulizi.

Hata hivyo, ni lazima wanafunzi wawe na ujuzi wa jumla kuhusu aina nyingine za insha. Wakiuliza maswali kuhusu aina yoyote ya insha baada ya kusoma, mwalimu awe tayari kuyajibu.

Maswali: Haya ni maswali ya kutathmini ikiwa wanafunzi wana ujuzi wa jumla kuhusu aina za insha. Yajibiwe katika makundi na majibu yawasilishwe darasani. Haya ni majibu yanayopendekezwa.

1. Insha ni mtungo wa kinathari ambao unajigawa katika aina mbalimbali. Ni utungo wenye sentensi nyingi zilizopangwa katika aya, zenye kuzungumzia mada moja.

2. Aina za insha ni hizi zifuatazo: Insha za wasifu, Insha ya mjadala/mdahalo, Insha fafanuzi, Insha ya methali, Insha ya mdokezo, Insha za picha, Insha ya mawazo au ya kubuni, Insha ya kitawasifu, Insha ya kitaaluma, Insha elezi/ya maelezo na Insha ya masimulizi.

3. Kifungu cha habari "Nchi Yetu" ni insha ya wasifu kwa sababu inachora picha ya kitu kinachozungumziwa. Katika insha hii, msanii anaonyesha waziwazi hisia zake. Ndani mwa insha hii kuna usanii.

4. Insha ya maelezo huwasilisha sifa za vitu, watu, hali, matendo, mahali au hata sherehe uliyohudhuria. Inalenga kutoa picha ya kitu katika akili zetu jinsi ambavyo kinamdhihirikia anayekiona.Mwandishi wake anahitaji kwanza kabisa kukusanya habari za kina kuhusu jambo analoliandikia. Hategemei tu yale ambayo yanaonekana kwa macho bali pia aina nyingine za hisi kama vile kugusa, kuonja, kunusa, kusikia na kadhalika wakati insha ya wasifuhuchora picha ya kitu kinachozungumziwa. Katika insha hii, msanii anaonyesha waziwazi hisia zake. Ndani mwake kuna usanii.

5. Umuhimu wa kujifunza utungaji wa insha:

- Utungaji wa insha huwezesha watu kutoa maelezo, mawazo au maoni kwa njia ya maandishi au mazungumzo

- Utungaji wa insha huwezesha utumiaji wa lugha fasaha, sanifu na uwezo wa kujieleza kwa njia ya maandishi au mazungumzo.

- Utungaji wa insha huwezesha kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu maisha yetu ya kila siku. Kupitia njia ya utungaji, watu hupata taarifa kuhusu vitu mbalimbali vinavyozunguka maisha yao ya kila siku.

- Utungaji wa insha hutumika kuelimisha, kukosoa na hata kuonya. Maandishi au mazungumzo (masimulizi) yanayotokana na utungaji huweza kuakisi hali halisi ya maisha ya jamii, na hivyo ikawa ni kama kioo cha kujitazama na kujirekebisha.

- Utungaji wa insha, hususan unaotokana na kazi za fasihi hutumika kuburudisha jamii. Hadithi na tanzu nyingine za fasihi zinazotokana na utungaji huburudisha, huliwaza na kufurahisha jamii.

- Utungaji wa insha hutumika kukuza lugha kwa njia ya mazungumzo au maandishi. Mzungumzaji na msikilizaji hupata ufundi wa kujieleza zaidi kupitia utungaji, hali kadhalika, mwandishi na msomaji hupata ufundi wa kujieleza pia.

**Zoezi la 9:**(ukurasa 162)

Maneno yaliyoandikwa kwenye mraba ni maneno yanayohusu mazingira na usafi na yalitumiwa katika kifungu cha ufahamu. Wanafunzi wayagundue katika makundi yao kisha wayaandike

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | C | H | A | F | U | Z | I | U | H |
| P | S | K | K | M | N | I | O | O | E |
| E | Y | A | B | A | Z | W | K | F | W |
| P | E | M | F | Z | M | A | W | B | A |
| O | D | I | Y | I | A | L | E | F | R |
| I | C | L | E | N | U | M | I | T | I |
| K | P | I | K | I | A | K | P | V | R |
| W | V | M | E | R | U | O | U | Y | L |
| I | H | A | O | A | W | I | G | A | H |
| N | Y | A | S | I | N | M | V | U | A |

**Zoezi la 10:** (ukurasa 162)

Hizi ni nyanja za kiutawala nchini Rwanda. Ingawa hazikuzungumziwa katika kifungu cha ufahamu, ni vizuri mwanafunzi ajue namna zinavyoitwa katika Kiswahili kwa sababu zina nafasi yake katika maisha ya kila siku ya Wanyarwanda. Huduma nzuri zinazotolewa na nyanja hizo ndizo huifanya "nchi yetu" kuwa nchi inayopendeza. Zoezi hili lifanyiwe katika makundi.

1. Wizara ya Mazingira na Mali ya Asili.

2. Wizara ya Miundo mbinu.

3. Wizara ya Afya.

4. Wizara ya Kilimo na Ufugaji.

5. Wizara ya Ulinzi.

Zoezi la 11: (ukurasa 160)

Maneno yaliyotumiwa katika zoezi hili ni maneno yanayohusu mazingira na insha za wasifu. Kutenganisha neno na maneno mengine yasiyohusiana nalo kunahitaji kujua maana za maneno yote katika zoezi. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi hawatoi majibu kwa nasibu tu. Hapa anaweza akawauliza sababu ya jibu lao.

1. mimea

2. mwindaji

3. nyumba

4. kutukana

5. nahodha

**Zoezi la 12**: (ukurasa 163)

Sentensi katika zoezi hili zina maana, lakini zimepangwa hovyo. Zikiachwa namna hiyo, ujumbe wa insha utapotea. Kazi ya mwanafunzi hapa ni kuonyesha ni ipi ya kwanza, ya pili, n.k. ili ujumbe upatikane. Hili ni zoezi linaloweza kufanywa na mwanafunzi binafsi. Sentensi zipangwe namna hii:

1. Nyangumi anaposikia njaa, hutafuta sehemu yenye kundi la samaki.

2. Kisha, hupanua mdomo wake mkubwa.

3. Baada ya hapo, humeza maji mengi pamoja na samaki.

4. Akishameza maji na samaki,hufunga mdomo wake.

5. Akishafunga mdomo, husukuma nje maji aliyoyameza kupitia chujio lililoko mdomoni.

6. Ndipo samaki hubaki ndani.

15.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 13:** (ukurasa 163)

Hii si mara ya kwanza kwa wanafunzi kuzungumzia mambo ya "usafi" na "uhifadhi wa mazingira". Tayari katika somo la pili (kitabu cha mwanafunzi) walizungumzia "usafi hospitalini" na wa mazingira kwa jumla na umuhimu wake. Umuhimu wa zoezi hili ni kumwezesha mwanafunzi kujieleza kimazungumzo. Baadhi ya wanafunzi wajadili mada ya kwanza, wengine ya pili. Zoezi hili litayarishiwe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili.

i. Mambo muhimu yafuatayo yazingatiwe na wanafunzi wanapozungumzia umuhimu wa usafi: kuzuia maradhi yanayosababishwa na ukosefu wa usafi. Wataje maradhi wanayoyajua na namna husababishwa na ukosefu wa usafi.

ii. Wanapozungumzia namna ya kuhifadhi mazingira yetu, angalau waeleze vitendo kama: kupanda miti, kutochafusha maji ya mito, kutotupa taka ovyo, kutumia vyoo safi tunapotaka kwenda haja, kuwalinda wanyamapori wasije wakauliwa ovyo, n.k.

## 15.4.6. Utungaji

**Zoezi la 14:** (ukurasa 163)

Hili ni zoezi la kuandika insha ya wasifu. Kwa hiyo linamsaidia mwanafunzi kujenga ustadi wa kisanii. Mwalimu atakaposahihisha kazi ya kila mwanafunzi, ahakikishe ikiwa wamefahamu

upekee wa insha ya wasifu ukiilinganisha na aina nyingine za insha. Mambo muhimu kuhusu insha ya wasifu yazingatiwe:

i. Insha ya wasifu huchora picha ya kitu kinachozungumziwa.

ii. Insha ya wasifu huonyesha waziwazi hisia za msanii.

iii. Mtungaji wa insha ya wasifu ana uwezo wa kubadilisha mtazamo wetu kuhusu vitu ambavyo tunaviona ni vya kawaida, tukaviona katika mtazamo tofauti kabisa.

iv. Katika insha za wasifu kuna usanii, yaani insha ya wasifu ina mdundo wa kiushairi.

# SOMO LA 16: UTUNGAJI WA INSHA ZA MASIMULIZI

## 16.1. Utangulizi/Marudio

Mwalimu aanze somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi wake. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu ajue hali za wanafunzi na baadaye awaulize maswali machache kuhusu somo lililopita. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kujibu maswali hayo na kuwachangamsha kidogo hivi akielekeza maswali yake kwenye somo jipya.

***Baadaye, mwalimu aunde makundi kisha awaambie wanafunzi kutazama mchoro kwa makini na kuzungumzia kinachoendelea kwenye mchoro wenyewe.***

Mwalimu anaweza akaanza na swali lifuatalo: Tazameni michoro hapo juu kisha mtoe maoni yenu kuhusu kile kinachoendelea kwenye mchoro huo.

## 16.2. Vifaa vya Kujifunzia

Kwa minajili ya kuweza kufikia kwenye malengo ya somo, mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo lake. Mwalimu atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Michoro au picha za maeneo mbalimbali,
- Ubao,
- Chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule na upatikanaji wa vifaa mbalimbali. Mwalimu kwa ubunifu wake anaweza kuandaa vifaa mbalimbali vya kumsaidia kufanikisha somo lake.

## 16.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake hivi akitilia mkazo mbinu zifuatazo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne. Ni vizuri kutozidi idadi ya watu watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelea kuchunguza kwa makini namna kazi inafanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa

msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana. Baada ya kazi, mwalimu aombe makundi kuwasilisha matokeo kwa darasa. Kazi ya kushirikiana inahakikisha kuwa ujifunzaji unatawaliwa na utendaji wa watu, unakuwa hai na shirikishi na wenye kuzingatia ushirikiano. Mbali na kazi za kushirikiana zilizopo kwenye kitabu cha mwanafunzi, unaweza kubuni na kuwapatia wanafunzi kazi mbalimbali za kufanya au kwa ajili ya majadiliano ya papo kwa papo.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake. (Asome kifungu cha habari mwenyewe au afanye zoezi mwenyewe).

- **Maswali na majibu:** Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzake iwezekanavyo. Mwalimu ajaribu kuweka maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati yake na wanafunzi ama wanafunzi na wanafunzi. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wote wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali na wao wamjibu, na vile vile wanafunzi wamwulize mwalimu na wanafunzi wengine majibu, mwisho wake mwalimu naye atoe majibu yake.

- **Maelezo ya mwalimu:** Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake, kisha atambuwe ujuzi unaohitaji maelezo yake binafsi. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee vya kutosha wanafunzi wake somo kwa kusisitizia kasoro aliyoitambua. Ni vizuri kufanya hivi kwa kuwapa pia wanafunzi fursa ya majadiliano kuhusu maelezo yake.

**Zoezi la 1:**(ukurasa wa 164)

***Wanafunzi watazame michoro katika kitabu cha mwanafunzi kisha wajadili wanayoyaona kwenye mchoro na kuonyesha uhusiano uliopo kati ya michoro hiyo miwili. Mwalimu awaelekeze na awasaidie kufanya ugunduzi.***

## 16.4. Majibu

### 16.4.1. Maswali ya Ufahamu

***Maswali haya yafanyiwe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kifungu cha habari na baadaye wajibu maswali. Mwalimu awaongoze na asahihishe majibu watakayotoa.***

1. Wazazi wanapokaribia mwanzo wa masomo ya watoto wao huanza kujiandaa kwa kutimiza wajibu wao kwa kuandaa mahitaji yote muhimu kwa ajili ya watoto wao watakapoenda shuleni. Wakati huu wazazi huwanunulia watoto vifaa na vitu vingine vya kutumia shuleni na kuwalipia karo za shule.

2. Mwanafunzi anayezungumziwa katika kifungu hiki alikuwa ameanza kidato cha nne shule za Sekondari.

3. Babake ndiye alimsindikiza mwanafunzi hadi shuleni.

4. Baba yake alimshauri kusoma kwa bidii na kutumia muda wake wa kusoma ipasavyo, kujiepusha na tabia mbaya za vijana, kutojiingiza katika makundi ya wanafunzi wabaya ambao hawazingatii maonyo na mawaidha ya wazazi wao na walimu.

5. Mwanafunzi anayezungumziwa katika kifungu hiki ni mtiifu na mchangamfu.

6. Walipoingia ndani ya basi mwanafunzi alifurahishwa na kutazama miti na mimea ya aina mbalimbali iliyokuwa imepandwa kando kando ya barabara kubwa yenye lami na taa kubwa ambazo zilitoa mwangaza wa kutosha wakati wa usiku.

7. Kinachoonyesha kwamba mwanafunzi huyu alipokewa vizuri mara tu alipofika shuleni ni wakati alipopiga hodi ofisini na akapokelewa kwa mikono miwili kisha akasajiliwa na akapewa kitanda cha kulalia.

8. Mwanafunzi alipofika bwenini alishangaa sana kuona vitanda vingi katika ukumbi mkubwa ambapo kila kitanda kilikuwa na sehemu mbili za kulala, moja chini nyingine juu yake.

9. Wanafunzi wakati wa jioni walipewa chakula kizuri ambacho ni wali, maharage, mboga na matunda.

10. Walipoingia darasani mwanafunzi huyu alichukua daftari lake la somo la Kiswahili akaanza kupitia masomo yote waliyojifunza katika kidato cha tatu alipokuwa akisomea.

11. Wanafunzi walitakiwa kulala saa tatu za usiku.

### 16.4.2 Msamiati

**Zoezi la 2:**(ukurasa wa 166)

***Mwalimu aambie kila mwanafunzi kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno aliyopewa. Baadaye, mwalimu awaombe kuandika sentensi walizotunga ubaoni ili asahihishe makosa ya kimsamiati.***

***Mifano ya sentensi zinazopendekezwa ni kama hizi zifuztazo:***

1. Kabla ya kila mhula kuanza, wanafunzi na wazazi wao wanapaswa ***kujiandaa*** vya kutosha ili wasije wakapata usumbufu baadaye.

2. Haiwezi kuvumiliwa asikari ***kusaliti*** nchi yake.

3. Kijana huyu hana akili: amekubali ***kuuza*** lile shamba alilorithi kutoka kwa wazazi wake.

4. Wanafunzi wasiotaka kusoma kwa ***bidii*** hawafaulu mitihani.

5. Wale waliokuwa na ***tabia*** za kutowaheshimu wengine hupoteza marafiki.

6. Mwanafunzi huyu ana ***maadili;*** kila mtu shuleni anampenda.

7. Tulipokutana amenitakia ***heri na fanaka*** kwa mwaka mpya.

8. "Tulikutania kwenye ***ukumbi*** wa shule." Mwalimu Mkuu aliwambia wazazi.

9. Kila mwanafunzi ***anapaswa*** kusajili ***katika ofisi hii hapaa*** ili asaidiwe.

10. Haionekani vizuri kwa watoto ***kuashiria*** watu wakubwa wanapohitaji usaidizi.

**Zoezi la 3:** (Ukurasa wa 167)

***Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wanafunzi watumie mshale kwa kuunganisha maneno na maana zake. Mwalimu awasaidie na atathmini majibu ya wanafunzi.***

1. -c

2. - j

3. - g

4. - k

5. -i

6. -a

7. - h

8. - e

9. -b

10. - f

11. -d

**Zoezi la 4:**(ukurasa wa 167)

***Wanafunzi wajiunge na wengine ili watambue maneno haya katika kifungu. Mwalimu asahihishe majibu ya wanafunzi.***

**1. wazazi**

**2. maadili**

**3. jioni**

**4. mkurugenzi**

**5. hodi**

**6. kwaheri**

**7. godoro**

**8. kupokelewa kwa mikono miwili**

### 16.4.3 Sarufi: Usemi wa Asili na Usemi wa Taarifa

**Zoezi la 5:** (Ukurasa wa 168)

***Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, watazame sentensi wanazopewa kisha watoe maoni yao kuhusu muundo wake. Mwanafunzi mmoja awasilishe waliyoyazungumzia katika kundi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameshiriki katika kundi. Mwalimu akosoe majibu ya wanafunzi na awaelekeze katika mawasilisho yao.***

***Jibu pendekezo:***

Muundo wa sentensi hapo juu unaonyesha kwamba kauli ya moja kwa moja kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji haikufanyiwa mageuzi yoyote. Sentensi hizi zinaonyesha maneno yanayotamkwa na mtu yakiwa katika hali yake ya kwanza au asili.

**Zoezi la 6:** (Ukurasa wa 169)

***Mwalimu awaambie wanafunzi kufanya zoezi hili binafsi. Wanafunzi waweke alama zinazokosekana katika sentensi. Mwalimu awakumbushe matumizi ya alama katika usemi wa asili.***

1. “Alitoka mjini Kigali.” Kamariza alisema.

2. “Umewezaje kuubeba mzigo huu peke yako?” Mama aliniuliza.

3. “Utarudi kesho?” Mama yake alitaka kujua.

4. “Malizeni kazi mliyopewa!” Mwalimu alituamrisha.

5. “Mtahitaji vikombe vingapi vya chai?” Mwenye hoteli alituuliza

**Zoezi la 7:** (Ukurasa wa 169)

***Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wazungumzie muundo wa sentensi. Mwalimu awaelekeze na awasaidie kurekebisha makosa.***

***Jibu pendekezo:*** Muundo wa sentensi hapo juu unaonyesha kwamba:

- Alama za kufungulia au kufungia maneno yaliyotamkwa hazitumiwi.

- Alama ya kuuliza na ya mshangao hazitumiwi.
- Maneno ***"kuwa"*** au "***kwamba"*** hutumiwa.

Sentensi hizi zinaonyesha maneno ambayo yalizungumzwa na mtu mwingine bila ya kubadilisha, kupunguza au kuongeza maana ya jambo analotaka kulitolea maelezo.

### **Zoezi la 8:** (Ukurasa wa 172)

***Kila mwanafunzi abadilishe sentensi katika usemi wa taarifa. Mwalimu awarekebishe kwa kufuata mabadiliko yanayohitajika katika usemi wa taarifa. Majibu yaundwe kama mifano ifuatayo:***

1. Riziki alieleza kuwa alimruhusu kujenga nyumba nyingine.

2. Mchumba wake alimuuliza ikiwa anampenda au hampendi.

3. Yeye alijiuliza sababu hakusema chochote siku ile kipindi kile.

4. Uwera ananiambia kwamba Gasore angemtembelea siku ambayo ingefuata asubuhi.

5. Mwalimu alisisitiza kuwa hakuona sababu yoyote ya kumsumbua.

6. Wakulima walisema kwamba hawangekuwa na mvua ya kutosha mwaka ule.

7. Mwalimu alituarifu kuwa jua ni gimba kubwa lenye nuru kali lililoko angani ambalo hutoa mwanga na joto.

8."Tafadhali, msivute bangi kamwe kwani ni hatari kwa afya yenu" Mwalimu mkuu aliwashauri wanafunzi kuwa wasivute bangi kamwe kwani ni hatari kwa afya yao.

### **Zoezi la 9:** (Ukurasa wa 172)

***Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaombe kugeuza sentensi walizopewa katika kitabu cha mwanafunzi ziwe katika usemi halisi. Mwalimu asahihishe majibu ya wanafunzi. Majibu yatolewe kwa kufuata njia hii:***

1. Baba alituahidi "Nitawapeleka mjini kutembea mtakaposhinda mtihani mwaka kesho."

2. Katibu alitangaza "Kutakuwa na mkutano wa wanachama wote ambao wanakuwa wamesajiliwa mwezi huu Jumanne ijayo."

3. "Kuna umuhimu kuwatii wazazi wao kwani hili litaongeza siku zao duniani." Mshauri aliwasisitizia watoto.

4. Kiranja aliuliza "Kwa nini Afida kuchelewa darasani siku hii."

5. Mwenye hoteli aliuliza "Mnahitaji vikombe vingapi vya chai?"

6. “Nitafaulu katika somo la Kiswahili.” Mwanafunzi alimwambia.

7. Mkuu wa shule alitahadharisha “Msiharibu miti wanafunzi!”

8. “Sote mwende uwanjani kushangilia timu yenu.” Mwalimu alisema.

9. Kasisi alimshauri “Kazimoto acha tabia zako za ulevi.”

10. “Anayenitesa si adui yangu bali ni rafiki yangu wa karibu.” Chapakazi alisema.

### 16.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 10 :** (Ukurasa wa 173)

***Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi wanne wanne, wanafunzi wasome maelezo muhimu kuhusu insha katika kitabu cha mwanafunzi na baadaye wajibu maswali na kuyawakilisha. Mwalimu waongoze kufanya mawasilisho na akosoe makosa yatakayojitokeza wanapowasilisha.***

**Majibu pendekezo:**

1. Utangulizi ndio sehemu muhimu katika mtungo wowote wa insha kwa sababu:

- Ndiyo sehemu ambayo inampa mtu habari kamili ya mada inayozungumziwa,

- Utangulizi mzuri hufafanua malengo ya insha na jinsi malengo hayo yatakavyofikiwa,

- Utangulizi mzuri pia humfanya msomaji avutiwe na yale yatakayojadiliwa katika insha nzima.

2. Sehemu kuu za insha ni tatu, ambazo ni utangulizi, kiini na kimalizio

- Utangulizi hupaswi kuwa mrefu sana au wa kuchosha. Aya moja fupi inatosha. Iwapo sehemu hii haikuandikwa kwa ufasaha ufaao, inaweza kumfanya msomaji akose hamu ya kuendelea kuisoma insha hata ingawa insha inaweza kuanza kuvutia hapo baadaye.
- Sehemu ya kiini hutoa ufafanuzi na maelezo kuhusu kichwa au hoja. Aghalabu sehemu hii huwa ndefu na yenye aya nyingi za urefu tofauti.
- Katika sehemu ya kimalizio, mwandishi hujaribu kusisitiza hoja zote muhimu ambazo zimejadiliwa na kutoa msimamo wa insha yenyewe kuhusu jambo lililojadiliwa. Mwisho wa insha huonyesha uhusiano uliopo kati ya utangulizi na maelezo yaliyomo katika mwili. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua.

3. Yapo mambo kadhaa ya kuzingatia wakati wa uandishi wa insha. Mambo hayo ni pamoja na:

- Kutambua ni mada gani ya kuandikia insha na kuielewa vema,

- Kupanga mawazo katika mtiririko wa fikra zilizopangwa ili kujenga insha zenye kukubalika,

- Kutumia lugha yenye usahihi wa maneno na inayoeleweka,

- Kufuata taratibu za kuendesha uandishi. Kwa mfano, matumizi ya alama za uandishi, aya, herufi kubwa na herufi ndogo,

- Kupanga insha katika muundo wake, yaani kichwa, utangulizi, kiini na hitimisho.

i) Kichwa cha habari cha insha ni maneno machache, takribani matano, ambayo ndiyo jina la insha. Kichwa cha habari huandikwa juu, katikati kwenye ukurasa wa kwanza wa insha. Mara nyingi, huandikwa kwa herufi kubwa na hubeba wazo kuu la insha.

ii) Utangulizi wa insha ni sehemu ya mwanzo yenye urefu usiozidi aya moja. Utangulizi hudondoa kwa ufupi kabisa kile kinachoelezwa kwenye insha.

iii) Kiini cha insha;hii ni sehemu tunayoweza kusema ndiyo insha yenyewe. Kwenye kiini ndipo ufafanuzi wote hutolewa. Ufafanuzi huu hupangwa katika aya moja au zaidi. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua.

iv) Hitimisho la insha; hii ni sehemu ya mwisho ya insha ambayo nayo haizidi aya moja. Katika sehemu hii, mwandishi anaweza kurejeakwa ufupi sana yale aliyozungumzia kwenye insha yake, anaweza kuonyesha msimamo wake, anaweza kutoa mapendekezo, au kuwahimiza walengwa wake kuchukua hatua fulani.

### 16.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 11:** (Ukurasa wa 175)

***Zoezi hili lifanyiwe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, wanafunzi wachague mada ya kuzungumzia mbele ya darasa wakifuata muundo wa insha. Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi katika kundi ametoa maoni yake kuhusu mada.***

1. Harusi

Maneno haya ni muhimu kutumika: waalikwa, vyakula na vinywaji, mazingira na hali ya hewa.

2. Mchezo uliohudhuria

Mambo haya yaingizwe katika mazungumzo: Rejesta za mpira, dhana ya michezo katika kujenga afya.

### 16.4.6 . Utungaji

**Zoezi la 12:** (Ukurasa wa 175)

***Wanafunzi wafanye zoezi hili kwa binafsi. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kutunga kuhusu mada zinazopatikana katika kitabu cha mwanafunzi wakizingatia sehemu kuu za insha.***

1. Watoto Wawe na Uhuru wa Kuchagua Dini Wanayoitaka.

2. Rafiki yako anayesoma katika kidato cha tano amefukuzwa shuleni kwa sababu anatumia dawa za kulevya na kushiriki ulevi. Simulia kilichoendelea.

## 16.5.Muhtasari wa Mada

Mada hii ya tano ***"Utungaji"*** ina masomo makuu matatu yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo kama vile: kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, maelezo muhimu, kusikiliza na kuzungumza na utungaji. ***Somo la 14*** linaeleza maana ya insha za kubuni au za masimulizi na kueleza usemi wa asili. ***Somo la 15*** linaeleza aina za insha kwa kujikita zaidi kwenye insha za wasifu kama mfano na maelezo kuhusu usemi wa taarifa. Somo la 16 linaeleza sehemu za kuzingatia katika utungaji wa insha na kubainisha mabadiliko yaliyopo toka usemi wa asili kwenda usemi wa taarifa.

## 16.6. Maelezo ya Ziada

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mwalimu. Sehemu hii inamsaidia mwalimu kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada.

## 16.7. Tathmini ya Mada ya Tano

***Kazi hii ni ya kila mwanafunzi binafsi. Mwalimu awaombe wanafunzi kuendeleza insha kwa kufuata kanuni walizopewa katika kitabu cha mwanafunzi. Mwalimu awasaidie na awaongoze. Insha inaweza kuendelezwa kama mfano ufuataao:***

**NAFASI YA WANAWAKE KATIKA KUENDELEZA UCHUMI WA NCHI YETU**

## 16.8. Mazoezi ya Ziada

### 16.8.1. Mazoezi ya Urekebishaji

Chagua neno sahihi kukamilisha sentensi hizi

1. Nilikuwa mgonjwa lakini sasa nime…………….. (poa, powa, pona)

2. Sipendi maneno ya …………………….. na watu wengine bila sababu. (kuzuzuza, kuzuliwa, kuzuzuliwa)

### 16.8.2. Mazoezi Jumuishi

Chagua neno moja lililo kinyume cha lile lililoandikwa kwa herufi za mlazo:

1. Anataka kuongeza hisa zake katika shirika lile. (zidisha, toa, punguza)

2. Kazi waliyoifanya inaonyesha hekima waliyo nayo. (busara, upumbavu, maarifa)

3. Ni kazi ngumu kumuumba binadamu. (kumharibu, kumuumbua, kumtengeneza)

### 16.8.3 Mazoezi Nyongeza

Andika insha fupi kuhusu:

1. Mambo yanayosababisha uchafuzi wa mazingira.

2. Hatua zinazofaa kuchukuliwa na walimwengu ili kusafisha mazingira.

## MAREJEO


ABDILAHI, N. (1974).Tamrini za Kiswahili: Kitabu cha pili, Nairobi, Oxford University Press.

Co-Publishing Committee (1987). Hadithi za kwetu, Nairobi, Co-Publishing Committee.

Kitula, K. (2014). Taaluma ya Uandishi. The Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi, Kenya.

Mdee, J. S. ,K. Njogu, A. Shafi (2011). Kamusi ya Karne ya 21. Longhorn Publishers (K) Ltd. Nairobi, Kenya.

MINEPRISEC (1982).Ikinyarwanda: Gusoma no Gusesengura Imyandiko, Kigali.

Mlaga. W. K. (2017). Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21. Heko Publishers Ltd. Dar es salaam.

MUJAKI, A.& KIZZA, G.G.(2000). MK Kiswahili kwa shule za msingi: Kitabu cha Kwanza-Darasa la Nne, Kiongozi cha Mwalimu, MK Publishers (U) Ltd, Kampala.

NDAYAMBAJE, L.& NIYIRORA E. (2012), Kiswahili Sanifu kwa Shule za Sekondari kidato cha Nne. Tan Prints (India) Pvt.Ltd.

NGUGI WA THIONG'O. (2003). Siri na Hadithi Nyingine. East African Publishers Ltd. Nairobi

NICKY STANTON (1996). Mastering Communication, Hampshire, Macmillan MasterSeries.

NIYOMUGABO, C. (2013). Mafunzo ya Kiswahili: Mwongozo wa Mwalimu, Kidato cha 5, Kigali, Fountain Publishers Rwanda Ltd.

NKWERA V. M. F. (1978) Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo,. Tanzania Publishing House Dar-es-Salaam.

Ntawiyanga S., na Kinya J.M. (2015). Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 2, Longhorn Kenya Ltd; Nairobi

Ntawiyanga S., Muhamud A, Kinya J.M na Sanja L (2018). Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 3, Longhorn Kenya Ltd; Nairobi.

Rwanda Education Board (2015). Muhtasari wa somo la Kiswahili kidato cha 4-6 Michepuo mingine. Kigali-Rwanda.

Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari (1987).Kitabu cha Kiswahili III A, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari.

Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari (1987).Kitabu cha Kiswahili III B, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari.

Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari, Kitabu cha Kiswahili IV-VA, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari, Novemba 1987

TUKI (2006). English-Swahili Dictionary (3rd Edition). Dar-es-Salaam,

Tanzania.
Wamitila K.W. (2007). Mwenge wa Uandishi. Mbinu za Insha na Utunzi. Vide˜Muwa Publishers Limited. Nairobi, Kenya.